# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA MWAKA 2004
# (NA.20 YA 2004)

**THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT ACT, 2004**

---

**KISWAHILI TRANSLATION**

---

**NOTICE**

---

**(Made under Section 233)**

Notice is hereby given that the following publication is the Kiswahili translation of the Environmental Management Act, 2004

DAR ES SALAAM
… October, 2005

A.D. NTAGAZWA
*Minister of State,*
*Vice President's Office, Environment*

**SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**
**YA MWAKA 2004**

**YALIYOMO**

*Fungu* *Jina*


**SEHEMU YA I**
**MASHARTI YA UTANGULIZI**

1. Jina.
2. Tarehe ya Sheria kuanza kutumika.
3. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA II**

**MISINGI YA JUMLA**

4. Haki ya kuwa na mazingira safi, salama na ya kiafya.
5. Haki ya kufungua mahakamani madai kuhusu mazingira.
6. Wajibu wa kulinda mazingira.
7. Misingi ya usimamizi wa mazingira.
8. Jukumu la kutekeleza misingi ya mazingira.
9. Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya mazingira.
10. Siku ya mazingira.

**SEHEMU YA III**
**UTAWALA NA MUUNDO KIASASI**

***(a) Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira***

11. Kuanzishwa kwa Kamati na wajumbe wake.
12. Kazi za Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira.

*(b)* ***Waziri Mwenye Dhamana ya Mazingira***

13. Mamlaka ya Waziri.

### *(c) Mkurugenzi wa Mazingira*

14. Mkurugenzi wa Mazingira.

15. Kazi za Mkurugenzi wa Mazingira.

### *(d) Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira*

16. Baraza.
17. Lengo la kuanzishwa kwa Baraza.
18. Kazi za Baraza.
19. Bodi ya Baraza.
20. Uendeshaji wa shughuli na masuala ya Baraza.
21. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.
22. Watumishi na waajiriwa wa Baraza.
23. Mamlaka ya jumla ya Baraza.
24. Mamlaka ya Baraza kwa mawakala wengineo.
25. Mamlaka ya Baraza katika kuhakikisha utekelezaji wa Sheria.
26. Kukasimu madaraka kwa vyombo vingine.
27. Lakiri ya Baraza.
28. Kinga kwa Bodi, wajumbe, n.k., kutowajibika binafsi.
29. Mgongano wa maslahi.

### *(e) Wizara za kisekta*

30. Kuanzishwa kwa sehemu ya mazingira katika kila sekta.
31. Kazi za sehemu ya mazingira katika kila sekta.
32. Kuwasilishwa kwa taarifa za Wizara za kisekta.
33. Uteuzi wa mratibu wa mazingira kisekta.

### *(f) Sekretarieti ya Mkoa*

34. Uratibu wa usimamizi wa mazingira kimkoa.
35. Uteuzi wa mtaalamu wa usimamizi wa mazingira wa mkoa.

### *(g) Mamlaka za Serikali za Mitaa*

36. Majukumu ya Ofisa Usimamizi Mazingira wa Serikali za Mitaa.

37. Kamati za Kudumu za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

38. Kamati za Kudumu za Miji, Kata, Vijiji na Vitongoji.

39. Uteuzi wa Ofisa Msimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji.

40. Kazi za Ofisa Msimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji.

41. Madaraka ya jumla ya Kamati za Usimamizi wa Mazingira za Jiji, Manispaa, Wilaya, Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji.

## SEHEMU YA IV
## UANDAAJI MIPANGO YA MAZINGIRA

42. Mipango Tekelezi ya Mazingira ya mamlaka ya serikali za mitaa.

43. Mipango Tekelezi ya Mazingira kisekta.

44. Mipango Tekelezi ya Mazingira kitaifa.

45. Kanuni za kuandaa, kukubali na kutekeleza mipango tekelezi ya mazingira.

46. Ushirikishwaji wa umma katika kuandaa Mpango Tekelezi wa Taifa wa Mazingira.

## SEHEMU YA V
## USIMAMIZI WA MAZINGIRA

### *(a) Maeneo ya Mazingira Lindwa*

47. Tangazo la Maeneo ya Mazingira Lindwa.

48. Mpango wa ulinzi wa mazingira lindwa na usimamizi wa mifumoikolojia kwa ajili ya Maeneo ya Mazingira Lindwa.

### *(b) Mipango ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maeneo Lindwa ya Taifa*

49. Mipango ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maeneo Lindwa ya Taifa.

### *(c) Hifadhi na Ulinzi*

50. Usimamizi wa matumizi ya ardhi.
51. Maeneo ya mazingira nyeti.
52. Utambuzi wa maeneo ya mazingira nyeti.
53. Masharti ya hifadhi ya mazingira kwenye ardhi ya Vijiji.
54. Kutangazwa mito, maziwa au miambao ya maziwa na fukwe lindwa.
55. Ulinzi na usimamizi wa mito, miambao ya mito, maziwa au miambao ya maziwa na fukwe.
56. Tangazo la ardhi oevu lindwa.
57. Kuzuia shughuli za binadamu kwenye baadhi ya maeneo.
58. Hifadhi ya milima, vilima na mandhari.
59. Kuendeleza usimamizi wa mazingira ya pwani.
60. Masharti ya mazingira katika sheria za maji.
61. Waziri anaweza kushauri kuhusu umwagaji wa majitaka.
62. Ushauriano kuhusu umwagaji wa vichafuzi.
63. Usimamizi wa rasilimali za misitu.
64. Uendelezaji hifadhi ya nishati.
65. Uendelezaji wa hifadhi ya rasilimali za uvuvi na wanyamapori, n.k.
66. Hifadhi ya bioanuwai.
67. Hifadhi ya bioanuwai mahali asilia.
68. Hifadhi ya bioanuwai mahali pasipo asilia.
69. Kanuni za kuendeleza, kushughulikia na kutumia Viumbe Vilivyobadilishwa Nasaba Kijeni na mazao yake.
70. Usimamizi wa mbuga.
71. Miongozo ya mipango ya matumizi ya ardhi.
72. Wajibu kuhusu matumizi endelevu ya ardhi.
73. Kulinda urithi asilia na wa kiutamaduni.
74. Hifadhi ya angahewa.
75. Hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.
76. Usimamizi wa mazingira ya kazi na maunzi, na michakato hatari.
77. Mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kuhusu vichafuzi dumufu vya kikaboni.
78. Taratibu za awali za kibali kwa ajili ya baadhi ya kemikali hatari na viuavisumbufu.

79. Ukuzaji wa uzalishaji bora na matumizi endelevu ya bidhaa na huduma.

***(d) Nyenzo za Kiuchumi***

80. Motisha na nyenzo za kiuchumi kwa ajili ya kulinda mazingira.

## SEHEMU YA VI
## TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA NA TATHMINI NYINGINEZO

81. Wajibu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
82. Kanuni na miongozo ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
83. Wataalamu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
84. Kutolewa hati si kinga dhidi ya mashtaka ya kisheria.
85. Kubaini mawanda ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
86. Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
87. Mapitio ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
88. Kutembelea eneo kwa nia ya kufanya uhakiki unaohusu mapitio ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
89. Ushirikishwaji wa umma katika Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
90. Mkutano wa kutoa taarifa kwa umma na kupata maoni ya umma.
91. Mapendekezo ya Baraza kuhusu Taarifa ya Tathmini ya Athari.
92. Waziri kukubali au kukataa Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
93. Kufuta leseni iwapo Tathmini ya Athari kwa Mazingira itakataliwa.
94. Kukasimu madaraka ya kuidhinisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
95. Rufaa dhidi ya uamuzi wa Waziri kuhusiana na Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
96. Utunzaji wa kumbukumbu za maamuzi kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
97. Kutakiwa kufanyika upya utafiti wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
98. Kosa la kukiuka Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
99. Upelembaji wa hali ya mazingira.

100. Upelembaji wa uzingatiaji wa maelekezo ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.
101. Uhakiki wa mazingira.
102. Urejeshaji wa mazingira ya eneo la mradi au baada ya shughuli kufungwa.
103. Tathmini nyinginezo.

**SEHEMU YA VII**

**TATHMINI YA MAZINGIRA KIMKAKATI**

104. Tathmini ya Mazingira Kimkakati kuhusu miswada, kanuni, sera, mikakati, programu na mipango.
105. Tathmini ya mazingira kimkakati ya shughuli za madini, mafuta, umeme wa nishati ya maji na mipango ya miradi mikubwa ya maji.

**SEHEMU YA VIII**

**UZUIAJI NA UDHIBITI WA UCHAFUZI**

106. Uzuiaji wa uchafuzi kwa ujumla.
107. Mamlaka ya Waziri kutunga kanuni za kuzuia na kudhibiti uchafuzi.
108. Uzuiaji na udhibiti fungamanishi wa uchafuzi.
109. Kuzuia uchafuzi wa maji.
110. Kuzuia umwagaji wa dutu hatari, kemikali, mafuta n.k.
111. Wajibu wa kuwa na taarifa za mabadiliko ya kiteknolojia.
112. Wajibu wa kutoa taarifa ili kuzuia uchafuzi.
113. Notisi ya kuzuia aina ya mchakato au shughuli zilizoagizwa.

**SEHEMU YA IX**

**USIMAMIZI WA TAKA**

***(a) Usimamizi wa Taka Ngumu***

114. Wajibu wa mamlaka ya serikali za mitaa kusimamia na kupunguza taka ngumu.
115. Utupaji wa taka ngumu kutoka kwenye masoko, maeneo ya biashara na asasi.
116. Uwekaji wa taka ngumu kutoka viwandani.

117. Ukusanyaji taka ngumu kwenye maeneo ya mijini na vijijini.

118. Vituo vya taka vya muda.

119. Hatua ya mwisho ya utupaji wa taka ngumu.

***(b) Usimamizi wa Takataka***

120. Ufafanuzi kuhusu usimamizi wa takataka.

121. Udhibiti wa takataka kwenye maeneo ya umma.

122. Wamiliki wa ardhi binafsi kuondoa takataka.

*(**c) Usimamizi wa taka vimiminika***

123. Utupaji wa taka vimiminika katika eneo zilipozalishwa.

124. Usafirishaji na utupaji wa taka vimiminika.

125. Jinsi ya kufua taka vimiminika.

126. Utupaji wa taka vimiminika.

127. Udhibiti na upelembaji wa mifumo ya maji taka.

128. Taka vimiminika viwandani.

129. Usimamizi wa maji ya mvua.

*(d**) Usimamizi Gesi Taka***

130. Gesi taka kutoka majumba ya makazi.

131. Udhibiti wa gesi taka za viwandani.

132. Gesi taka na taka chembechembe kutoka kwenye magari.

***(e) Usimamizi wa Taka zenye Madhara***

133. Uingizaji nchini wa taka zenye madhara.

134. Wajibu wa mamlaka ya serikali za mitaa kuhusiana na taka zenye madhara.

135. Usafirishaji wa taka hatari.

136. Tathmini ya Athari kwa Mazingira kuhusu taka zenye madhara.

137. Utupaji wa mwisho wa taka zitokanazo na huduma za afya.

138. Utupaji wa taka nyinginezo.

139. Uwezo wa jumla wa mamlaka za serikali za mitaa katika kupunguza taka.

**SEHEMU YA X**

**VIWANGO VYA UBORA WA MAZINGIRA**

140. Kuunda na kuidhinisha viwango vya ubora wa mazingira.

141. Kufikia viwango, n.k..

142. Kutekeleza viwango vya ubora wa mazingira.

143. Viwango vya ubora wa maji.

144. Viwango vya kumwaga vimiminika taka kwenye maji.

145. Viwango vya ubora wa hewa.

146. Viwango vya kudhibiti harufu yenye madhara.

147. Viwango vya kudhibiti uchafuzi utokanao na kelele na mitikisiko.

148. Viwango vya mitikisiko itokanayo na sauti.

149. Viwango vya kupunguza mnururisho.

150. Viwango vya ubora wa udongo.

**SEHEMU YA XI**

**AMRI ZA UREJESHWAJI, UTOAJI HAKI ZA NJIA NA UHIFADHI WA MAZINGIRA**

***(a) Amri za urejeshwaji***

151. Amri ya urejeshwaji wa mazingira.

152. Maudhui ya amri ya urejeshwaji wa mazingira.

153. Utoaji wa amri ya urejeshwaji wa mazingira.

154. Ushauri kabla ya kutolewa amri ya urejeshwaji wa mazingira.

155. Muda wa amri ya urejeshwaji wa mazingira.

***(b) Amri za utoaji  Haki za Njia***

156. Amri ya kutoa haki za njia ya mazingira na hifadhi.

157. Maombi ya haki za njia ya mazingira.

158. Utekelezaji wa haki za njia ya mazingira.

159. Usajili wa haki za njia ya mazingira.

160. Fidia kutokana na haki ya njia kwenye mazingira.

*(c) Amri za Uhifadhi*

161. Utoaji wa amri ya kuhifadhi mazingira.

**SEHEMU YA XII**

**UCHAMBUZI NA KUMBUKUMBU**

162. Uteuzi wa maabara za uchambuzi na uchukuaji sampuli.
163. Uteuzi wa wachambuzi na wachambuzi rejea
164. Hati ya uchambuzi na nguvu yake.
165. Utunzaji wa kumbukumbu ya masuala yanayoathiri mazingira.
166. Uwasilishaji kumbukumbu za mwaka.
167. Utoaji matokeo ya uchambuzi.
168. Majukumu ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuhusu mazingira.
169. Mbinu shirikishi za kubainisha kemikali chafuzi.
170. Wajibu wa kutoa taarifu kwa Baraza.
171. Kumbukumbu za mazingira kuhusu shughuli za uchimbaji madini.

**SEHEMU YA XIII**

**TAARIFA, ELIMU NA UTAFITI KUHUSU MAZINGIRA**

172. Uhuru wa kupata taarifa kuhusu mazingira.
173. Mamlaka ya Baraza kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa kuhusu mazingira.
174. Mfumo Mkuu wa Taarifa kuhusu Mazingira.
175. Taarifa ya Hali ya Mazingira.
176. Elimu na uhamasishaji kuhusu mazingira.
177. Utafiti wa mazingira.

**SEHEMU YA XIV**

**USHIRIKISHWAJI WA UMMA KATIKA MAAMUZI YANAYOHUSU MAZINGIRA**

178. Ushirikishwaji umma katika maamuzi yahusuyo mazingira.

## SEHEMU YA XV

## MIKATABA YA KIMATAIFA


179. Mikataba ya Kimataifa kuhusu Mazingira.

180. Programu za usimamizi wa mazingira mtambuko kati ya nchi jirani.

181. Kuanzishwa kwa ofisi za kitaifa na viungo.


## SEHEMU YA XVI

## UZINGATIAJI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA


182. Uteuzi wa wakaguzi wa mazingira.

183. Madaraka ya wakaguzi wa mazingira.

184. Makosa yanayohusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

185. Makosa yanayohusu kumbukumbu.

186. Makosa yanayohusu viwango vya mazingira.

187. Makosa yanayohusu uchafuzi wa mazingira.

188. Makosa yanayohusu bioanuwai.

189. Makosa yanayohusu amri za urejeshwaji, haki ya njia na hifadhi ya mazingira.

190. Makosa yanayohusu takataka.

191. Adhabu ya jumla.

192. Makosa ya madai.

193. Kuchukuliwa, kufutwa leseni, kazi za jumuiya na amri zingine.

194. Kuafikiana kwenye makosa.

195. Amri ya kizuizi ili kulinda mazingira.

196. Amri ya kizuizi kwenye shughuli zenye madhara makubwa kwa mazingira.

197. Amri ya dharura ya kulinda mazingira.

198. Amri ya kutimiza masharti ya mazingira.

199. Amri ya gharama.

200. Makosa yanayohusu wakaguzi wa mazingira.

201. Makosa yanayohusu watendaji wakuu wa asasi na mashirika.

202. Haki ya kushtaki ya mtu binafsi na asasi au shirika.

203. Utetezi.

**SEHEMU YA XVII**

**BARAZA LA RUFAA LA MAZINGIRA**

204. Kuanzishwa kwa Baraza la Rufaa la Mazingira.
205. Vyanzo vya fedha vya Baraza la Rufaa na wajumbe wake.
206. Mamlaka ya Baraza la Rufaa.
207. Mwenendo wa Baraza la Rufaa.
208. Maamuzi ya Baraza la Rufaa.
209. Kukata rufaa Mahakama Kuu.
210. Kinga ya kisheria kwa wajumbe wa Baraza la Rufaa.
211. Malipo kwa wajumbe wa Baraza la Rufaa.
212. Uteuzi wa Msajili.

**SEHEMU YA XVIII**

**MFUKO WA TAIFA WA DHAMANA YA HIFADHI YA MAZINGIRA**

213. Uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira.
214. Madhumuni ya Mfuko.
215. Muundo na utawala wa Mfuko.
216. Hesabu za mwaka na ukaguzi wa hesabu za Mfuko.

**SEHEMU YA XIX**

**MASHARTI KUHUSU FEDHA**

217. Vyanzo vya fedha kwa Baraza.
218. Akaunti ya benki na utengaji fedha.
219. Uwezo wa Baraza kukopa na kudhamini mikopo.
220. Vitega uchumi vya Baraza.
221. Bajeti ya mwaka na nyongeza yake.
222. Hesabu na ukaguzi wa fedha.
223. Taarifa ya Mwaka.

**SEHEMU YA XX**

**MASHARTI YA JUMLA NA MASUALA YA MPITO**

224. Sheria hii kuifunga Serikali.

225. Mambo ya mpito kuhusu mashauri ya madai.
226. Fidia za aina mbalimbali kwa muathirika.
227. Dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira.
228. Haki ya kufidiwa.
229. Utayari wa kukabiliana na dharura za mazingira.
230. Kanuni.
231. Kufutwa kwa sheria na kuendeleza baadhi ya masuala.
232. Mgongano na sheria nyinginezo.
233. Sheria kutafsiriwa kwa Kiswahili.

## MAJEDWALI

---

### JEDWALI LA KWANZA

WAJUMBE, MIKUTANO NA TARATIBU ZA KAMATI YA TAIFA YA USHAURI WA MAZINGIRA

---

### JEDWALI LA PILI

TARATIBU ZA KUENDESHA SHUGHULI ZA BODI

---

### JEDWALI LA TATU

AINA YA MIRADI INAYOHITAJI TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA

---

### JEDWALI LA NNE

WAJUMBE NA UENDESHAJI WA BODI YA WADHAMINI WA MFUKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA MWAKA 2004
(NA.20 YA 2004)

NAKUBALI

BENJAMIN W. MKAPA

Rais

8 Februari, 2005

**Sheria ya kuweka masharti ya muundo wa kisheria na kiasasi ya usimamizi endelevu wa mazingira; kuweka misingi ya usimamizi, tathmini na kuchukua hadhari kuhusu madhara kwa mazingira, kinga na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, usimamizi wa taka, ubora wa viwango vya mazingira, ushirikishwaji umma, utekelezaji sheria; kuweka misingi ya utekelezaji wa makubaliano ya kimataifa; kutekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira; kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Taifa ya mwaka 1983 na kuendeleza kuwepo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; kuundwa Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo.**

[………………………..]

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## SEHEMU YA I

## MASHARTI YA UTANGULIZI

**Jina** 1 Sheria hii itaitwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004.

**Tarehe ya Sheria kuanza kutumika** 2 (1) Sheria hii itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataiteua kwa kutoa tangazo katika *Gazeti la Serikali*.

(2) Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

**Fasili** 3 Katika Sheria hii, isipokuwa pale ambapo maelezo yataelekeza vinginevyo:-

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004;

"uchambuzi"maana yake ni majaribio au uchunguzi wa kitu chochote, kiini au mchakato kwa ajili ya kubaini hali au sifa au athari zake (ziwe za kimaumbile, kikemikali au kibiolojia) kwenye sehemu yoyote ya mazingira au uchunguzi wa utoaji au urekodi wa kelele au mitetemo ya sauti kubaini kiwango au dalili zingine za kelele au mitetemo ya sauti au athari kwenye sehemu ya mazingira;

"mchambuzi" maana yake ni mchambuzi aliyeteuliwa au kutajwa chini ya fungu la 163;

"matumizi yenye manufaa" maana yake ni matumizi ya mazingira, sehemu au dalili yake, yanayoweza kuleta afya kijamii, ustawi au usalama na yanayohitaji kulindwa dhidi ya athari za taka, umwagaji maji machafu, utoaji harufu, joto au mwanga na uwekaji wa taka unaoweza kuathiri mazingira;

"bioanuwai" maana yake ni tofauti kati ya viumbe hai kutoka vyanzo vyote ikiwa ni pamoja na mifumoikolojia ya nchi kavu, mifumoikolojia ya majini na ikolojia changamani ambayo ni sehemu ya mifumoikolojia hiyo; hii inahusisha tofauti kwenye spishi, kati ya spishi na ya mifumoikolojia;

"rasilimali kibiolojia" inahusisha rasilimali jeni, viumbe hai au sehemu ya viumbe hao, idadi ya viumbe, mimea na wanyama, au sehemu yoyote ya uhai au bioanuwai yenye thamani halisi au yenye uwezo wa kuwa na thamani kwa binadamu;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lililorejewa chini ya kifungu cha 19(1);

"matumizi salama ya bioteknolojia" maana yake ni kupuka hatari inayohusu ulinzi wa mazingira na afya ya binadamu, kufuatia matumizi ya tafiti na biashara za Viumbe Hai Vilivyobadilishwa Nasaba Kijeni;

"ardhi tengwa" maana yake ni ardhi ambapo imepitishwa haki ya njia ya mazingira;

"kemikali" maana yake ni dutu itumikayo katika kemia au inayopatikana

kwa kemia, iwe yenyewe au kwa kuchanganywa au kuandaliwa, kwa kutengenezwa, au kutokana na mazingira asilia, na kwa lengo la Sheria hii inahusisha kemikali za viwanda, madawa ya kuulia wadudu, mbolea na madawa;

"Baraza" maana yake ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lililorejewa chini ya fungu la 16;

"mchakato wa kufanya uamuzi" maana yake ni michakato au taratibu rasmi zilizowekwa na asasi za umma au binafsi kwa lengo la kufanya uamuzi wenye athari kimazingira, kijamii na kiuchumi;

"mwendelezaji" maana yake ni mtu anayeanzisha mradi unaolazimika kufanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira kwa mujibu wa Sheria hii;

"Mkurugenzi wa Mazingira" maana yake ni Mkurugenzi wa Mazingira aliyeteuliwa chini ya fungu la 14;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira;

"mfumoikolojia" maana yake ni elimumwendo changamani ya jamii za mimea, wanyama, vijiumbe na mazingira yao vikiwemo vitu visivyo hai;

"vimiminika taka" maana yake ni taka za gesi, maji au vimiminika vingine vitokavyo majumbani, kwenye kilimo, biashara au viwandani vilivyofanyiwa au visivyofanyiwa usafishaji na kumwagwa kwenye mazingira moja kwa moja au kwa kupitia kwingineko;

"elementi" katika muktadha wa mazingira maana yake ni sehemu yoyote muhimu ya mazingira ikiwa ni pamoja na maji, angahewa, udongo, mimea, tabianchi, sauti, harufu, ujumi, samaki na wanyamapori;

"mazingira" yanahusisha maumbile halisi yawazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabianchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe, hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana;

"ukaguzi wa mazingira" maana yake ni tathmini yenye lengo, utaratibu, kumbukumbu, inayofanyika vipindi maalumu kwa madhumini ya kufahamu ni kwa kiasi gani mpangilio wa kimazingira, usimamizi na maandalizi yanavyofanywa katika kuhifadhi na kulinda mazingira;

" haki ya njia ya mazingira" ni njia iliyoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya fungu la 156;

"elimu ya mazingira" ni pamoja na mchakato wa kutambua sifa na kufafanua dhana ili kuboresha taaluma na mitizamo muhimu kwa ajili ya kuelewa na kukubali uhusiano kati ya binadamu na utamaduni na hali hai inayomzunguka;

"tathmini ya athari kwa mazingira" maana yake ni uchunguzi wa hatua kwa hatua unaofanywa kubaini iwapo programu, shughuli au mradi utakuwa na madhara kwenye mazingira;

"Mkaguzi wa Mazingira" maana yake ni mkaguzi aliyeteuliwa au kutajwa chini ya au kwa mujibu wa fungu la 182;

"usimamizi wa mazingira" ni pamoja na kulinda, kuhifadhi na kutumia kwa njia endelevu sehemu ya mazingira;

“upelembaji mazingira” maana yake ni kubaini mara kwa mara au kwa vipindi, hali halisi na madhara bayana yatokanayo na shughuli au jambo linalohusu mazingira, liwe la muda mfupi au mrefu;

“uandaaji mipango ya mazingira” maana yake ni uwekaji mipango unaozingatia utunzaji na hifadhi ya mazingira, zikiwemo dharura zinazoweza kutokea katika mazingira;

“rasilimali za mazingira” ni pamoja na rasilimali za hewa, ardhi, mimea, wanyama, na maji pamoja na hali yake ya ujumi;

“amri ya kurekebisha mazingira” maana yake ni amri itoleyowa chini ya fungu la 151;

“uafiki mazingira” ni pamoja na jambo au shughuli ambayo haina madhara au uharibufu kwa mazingira;

“afya ya mazingira” maana yake inahusisha masuala ya afya ya binadamu na magonjwa yanayosababishwa na hali ya mazingira;

“hifadhi nje ya mahali asilia” maana yake ni hifadhi ya sehemu za bioanuwai nje ya mazingira ya asili;

“Mfuko” maana yake ni Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Mazingira ulioanzishwa chini ya kifungu cha 213(1);

“taka za gesi” maana yake ni utokaji gesi uliotajwa chini ya kifungu cha 132(1) na ni pamoja na utokaji uwezao kubainishwa;

“maunzi ya kijeni” maana yake ni kitu kitokanacho na mmea, mnyama, vijiumbe, au viumbe hai vingine vyenye uwezo wa kurithisha sifa za kijeni;

“Kiumbe Kilichobadilishwa Nasaba Kijeni” maana yake ni kitu chochote cha kibiolojia kiwezacho kujirudufu au kuhamisha taarifa za kijeni, na kinahusisha mimea, wanyama, bakteria na aina zote za vijiumbe, ukuzaji seli, virusi, plasma, na aina nyinginezo za vekta, zilizotengenezwa na kuzalishwa; kwa njia ya teknolojia ya seli au jeni; ambamo maunzi ya kijeni yamebadilishwa kwa njia ambayo kwa kawaida haitokei hivyo;

“rasilimali za kijeni” maana yake ni vitu vya kijeni vyenye sifa halisi au uwezo wa kuwa na sifa hizo;

“matumizi mazuri ya mazingira” maana yake ni matumizi kwa mujibu wa Sheria hii au sheria nyingine yoyote husika;

“dutu yenye madhara” maana yake ni kitu chochote ambacho ni kemikali, taka, gesi, dawa, mmea, mnyama au kijiumbe kiwezacho kuwa na madhara kwa afya, maisha ya binadamu au mazingira;

“taka yenye madhara” maana yake ni kitu chochote kigumu, majimaji, cha gesi au taka majimaji ambayo kwa sababu ya athari zake kikemikali, athari kwa mazingira na binadamu, maambukizo yake, kiwango chake cha sumu, ulipukaji na kulika/kubabuka kwake kinadhuru afya, maisha ya binadamu au mazingira;

“taka ya viwanda” maana yake ni taka itokanayo na viwanda vinavyozalisha au visivyozalisha, ambayo ni chanzo cha nishati, maji, mitambo ya kusafisha au mawasiliano pamoja na taka-ngumu zilizoelezwa chini ya Sehemu ya IX;

“hifadhi mahali asilia” maana yake ni hifadhi ya bioanuwai ndani ya

mfumoikolojia na makazi asili ya viumbe vya kibiolojia;
“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya mazingira;
“kelele” maana yake ni kila uchafuzi usababishwao na sauti ambayo kwa asili inakataliwa au ile iwezayo kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu, maisha au mazingira; pia ni pamoja na sauti iwezayo kubainishwa na Kamati ya Taifa ya Viwango vya Mazingira;
“tabaka la ozoni” maana yake ni tabaka la ukanda wa angahewa juu ya mpaka wa sayari kama ilivyofafanuliwa kwenye Mkataba wa Vienna wa Kulinda Tabaka la Ozoni wa mwaka 1985;
“ushirikishwaji” maana yake ni fursa na uwezo wa kuathiri matokeo ya mchakato wa kutoa uamuzi;
“Vichafuzi Dumufu vya Kikaboni” vina maana iliyotolewa kwake chini ya Sheria ya Kemikali za Viwanda na Walaji (Usimamizi na Udhibiti) ya mwaka 2003;
“kanuni ya mchafuzi hulipa” maana yake ni utaratibu ambapo gharama ya kulipia kusafisha sehemu yoyote ya mazingira yaliyoharibiwa kwa uchafuzi, kufidia waathirika wa uchafuzi, gharama za kupoteza manufaa ya matumizi kutokana na kitendo cha uchafuzi na gharama nyingine zihusianazo au zitokanazo na hayo, zitalipwa na mtu atakayetiwa hatiani kwa uchafuzi chini ya Sheria hii au sheria nyingine inayohusika;
“uchafuzi” maana yake ni mabadiliko ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja, ya rasilimali za kimaumbile, hali ya joto, kikemikali, kibiolojia, au sifa nururishi, ambazo kwazo ni sehemu ya mazingira kwa kumwaga, kuachia, au kuweka taka; hivyo kuleta madhara kwa matumizi yenye manufaa, kusababisha hali ambayo ni hatari kwa jamii kiafya, kiusalama au ustawi wa binadamu, au kwa wanyama, ndege, wanyamapori, samaki au viumbe wa majini, au kwa mimea au kusababisha kukiukwa kwa sharti lolote, kikomo, au kizuio chochote kwa mujibu wa leseni chini ya Sheria hii;
“makazi” ni pamoja na nyumba inapojumuisha kiwanja, majengo, ardhi, na mali ya kurithi, na kila aina ya milki pamoja na mashine, mtambo au gari litumikalo inayohusiana na kazi yoyote ifanywayo kwenye makazi hayo;
“Kemikali za Taarifa Awali” maana yake ni kemikali za hatari na viuavisumbufu ambavyo huhitaji udhibiti kwenye biashara ya kimataifa kama ilivyoelekezwa kwenye Mkataba wa Rotterdam na ni pamoja na kemikali na viuavisumbufu vingine vilivyoelezwa hivyo chini ya mikataba ya kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano imeridhia;
“mradi” ni pamoja na mradi wowote, programu au sera inayolenga miradi iwezayo kuathiri mazingira;
“mpendekezaji” maana yake ni mtu anayependekeza au kutekeleza mradi, programu au shughuli iliyobainishwa kwenye Jedwali la Tatu;
“umma” maana yake ni watu binafsi, jumuia za vyama vya kijamii , asasi za umma na za binafsi;
“mnururisho” ina maana iliyopewa chini ya Sheria ya Nishati Atomu ya mwaka 2003 na inahusisha uionishaji nururishi na unururishaji

mwingineo unaoweza kuwa na athari mbaya kwa afya ya binadamu, uhai wa mazingira;

"tathmini ya hatari" maana yake ni tathmini ya hatari ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, iwezayo kutokea kwa afya ya binadamu na mnyama, mazingira, bioanuwai uchumi jamii na nchi au sifa zake ziwezazo kuathiriwa kwa kuingiza, matumizi yaliyofichama kuachia kwa makusudi au kuweka kwenye soko kwa (VIHAVINAKI) Kiumbe Hai Kilichobadilishwa Nasaba Kijeni au mazao yake;

"kisehemu"kuhusiana na mazingira maana yake ni sehemu yoyote au zozote za mazingira zilizoelezwa kwa ujazo, nafasi, eneo, wingi wa vitu, ubora au muda au mchanganyo wa hayo;

"maji taka" maana yake ni mchanganyo wa kinyesi, mkojo, na uchafu na maji taka yatokanayo na uzalishaji na shughuli za majumbani, shughuli za asasi, biashara na viwanda;

"udongo" unajumuisha ardhi, mchanga, mwamba, mwambatope, madini, uoto, na mimea na viumbe waishio humo na vyote vitokanavyo kama vile vumbi;

"utupaji taka ngumu" maana yake ni hatua ya mwisho katika mfumo wa usimamizi wa taka ngumu;

"taka ngumu" maana yake ni vitu visivyo majimaji vitokanavyo na shughuli za majumbani, mitaani, biashara, viwandani na kilimo; pia ni pamoja na takataka au takataka za chakula, vitu visivyokuwa vya majimaji vitokanavyo na shughuli za ujenzi na ubomoaji, ufyekaji bustani na shughuli za madini, mizoga na mabaki ya magari mabovu;

"usimamizi wa taka-ngumu" maana yake ni huduma muhimu itolewayo kuhifadhi mazingira na afya ya jamii, kuendeleza usafi, urejeshwaji wa vitu, kuepuka na kupunguza wingi wa taka, kupunguza umwagaji uchafu na mabaki ya taka na kuzuia ueneaji wa magonjwa;

"kiwango" maana yake ni mipaka ya kumwaga au kuachia taka iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria hii au kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote iliyoandikwa;

"maendeleo endelevu" maana yake ni maendeleo yanayokidhi mahitaji ya kizazi cha sasa bila kuathiri uwezo wa vizazi vijavyo kutimiza mahitaji yao kwa kudumisha uwezo wa mihimili ya mifumoikolijia;

"matumizi endelevu" maana yake ni matumizi ya sasa ya mazingira au maliasili, ambayo hayaathiri uwezo wa kutumiwa na vizazi vijavyo au kupunguza uwezo wake wa mihimili ya mifumoikolojia;

"biashara" maana yake ni biashara yoyote, shughuli za biashara au kazi iliyoandaliwa kufanywa, iwe mwanzoni ilifanywa kwenye makazi yasiyohamishika au kwenye maeneo mbalimbali ambapo inaweza kusababisha kumwaga vitu na nishati, ikiwa ni pamoja na biashara, shughuli au kazi kwa madhumuni ya Sheria hii;

"vituo vya uhamisho" kuhusiana na taka ngumu, maana yake ni maeneo ya ardhi yaliyotengwa kwa ajili ya kukusanya taka-ngumu kutoka vyanzo mbalimbali kabla ya kutupwa;

"Baraza la Rufaa" maana yake ni Baraza la Rufaa la Mazingira

lililoanzishwa chini ya fungu la 204;

“taka” maana yake ni kitu chochote kiwe kioevu, kigumu, cha gesi au nururishi, ambacho kimemwagwa, kimeachiwa au kuwekwa kwenye mazingira kwa ujazo, muundo au kwa hali iwezayo kusababisha mabadiliko ya mazingira, ikiwa ni pamoja na taka iwezayo kuainishwa chini ya Sheria hii; na

“maji” ni pamoja na maji ya kunywa, mto, kijito, mkondo wa maji, bwawa, kisima, lambo, mfereji, mlangobahari, ziwa, kinamasi, mifereji wazi, au maji yaliyo chini ya ardhi.

## SEHEMU YA II
## MISINGI YA JUMLA

**Haki ya kuwa na mazingira safi, salama na ya kiafya**

4 (1) Kila mtu anayeishi Tanzania atakuwa na haki ya kuwa na mazingira safi, salama na ya kiafya.

(2) Haki ya kuwa na mazingira safi, salama na ya kiafya itahusisha haki kwa kila raia kutumia elementi za umma au sehemu mbalimbali za mazingira, kwa madhumuni ya burudani, elimu, afya, ibada, utamaduni na uchumi.

**Haki ya kufungua mahakamani madai kuhusu mazingira**

5 (1) Mtu yeyote, pale ambapo haki iliyoelezwa katika fungu la 4 imetishiwa kutokana na kitendo au kutotimiza wajibu ambako kunaweza kusababisha madhara kwa afya ya binadamu au mazingira, anaweza kufungua mashtaka dhidi ya mtu ambaye kitendo chake au kutotimiza wajibu kwake kunaweza kusababisha madhara kwa afya ya binadamu au mazingira.

(2) Mashtaka yaliyoelezwa kwenye kifungu cha (1) yanaweza-

(a) kuzuia, kukomesha, kusitisha au kutotekelezwa kwa shughuli yoyote, ambayo inaweza kusababisha madhara kwa afya ya binadamu au mazingira;

(b) kumlazimisha ofisa yeyote wa umma achukue hatua za kuzuia au kusimamisha shughuli yoyote au kutotekeleza wajibu, ambako kunaweza kusababisha madhara kwa afya ya binadamu au mazingira;

(c) kuamuru kuwa shughuli yoyote inayoendelea au kutotekeleza wajibu kunakoendelea kufanyiwe ukaguzi au upelembaji wa mazingira;

(d) kumtaka mtu ambaye shughuli yake au kutotekeleza wajibu kwake kunaweza kusababisha madhara kwa afya ya binadamu au mazingira, achukue hatua za kuhifadhi mazingira au maisha ya binadamu;

(e) kuwalazimisha watu wanaoharibu mazingira kurekebisha uharibifu huo kwa kiwango cha kuyarejesha mazingira katika hali ilivyokuwa kabla ya kuharibiwa;

(f) kuelekeza kumlipa fidia kwa mwathirika kutokana na madhara

au kutotimiza wajibu, pamoja na gharama zilizosababishwa na kukosa matumizi yenye manufaa kutokana na shughuli iliyosababisha madhara kwa afya ya binadamu au mazingira.

(3) Baraza la Rufaa, mahakama na mtu yeyote anayetekeleza mamlaka kwa mujibu wa Sheria hii, katika kutoa uamuzi, amri, utekelezaji wa wajibu au kutekeleza jukumu lolote, ataongozwa na misingi ya mazingira na maendeleo endelevu ifuatayo-

(a) msingi wa hadhari;

(b) msingi wa "mchafuzi hulipa";

(c) msingi wa hadhi ya mfumoikolojia;

(d) msingi wa ushirikishwaji umma katika sera za maendeleo, mipango na michakato ya usimamizi wa mazingira;

(e) msingi wa fursa ya kupata haki;

(f) msingi wa usawa kati ya kizazi na kizazi na pia ndani ya kizazi;

(g) msingi wa ushirikiano wa kimataifa katika usimamizi wa rasilimali za mazingira zinazochangiwa na nchi mbili au zaidi; na

(h) msingi wa wajibu wa lengo moja lakini uliotofautishwa.

**Wajibu wa kulinda mazingira**

6 Mtu yeyote anayeishi Tanzania atakuwa mdau na atawajibika kutunza na kuendeleza mazingira na kutoa taarifa kwa mamlaka husika kuhusu shughuli au jambo lolote ambalo kwa kiasi kikubwa linaweza kuathiri mazingira.

**Misingi ya usimamizi wa mazingira**

7 (1) Lengo la Sheria hii ni kuraghibisha na kuboresha uendelezaji, ulinzi, uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

(2) Katika kuendeleza lengo lililotajwa katika kifungu cha (1), Sheria hii inaweka mfumo wa kisheria ambao ni muhimu kwa ajili ya kuratibu shughuli mwafaka na zinazogongana ili kufungamanisha shughuli hizo kwenye mfumo wa jumla wa usimamizi endelevu wa mazingira kwa kutoa msaada muhimu wa kitaalamu kwa Wizara za kisekta.

(3) Ili kufikia lengo la Sheria hii, kila mtu atakayetekeleza mamlaka yake chini ya Sheria hii atazingatia misingi kwamba:

(a) mazingira ni urithi wa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo;

(b) athari mbaya zizuiwe au kupunguzwa kwa mipango fungamanifu, uratibu na jitihada za pamoja zinazozingatia mazingira kwa ujumla ;

(c) msingi wa hadhari unaozingatia kuwa kuna uwezekano wa kutokea

hatari kubwa ya athari zisizorekebishika, ukosefu wa uhakika wa kisayansi haupaswi kuzuia au kuzorotesha hatua za hadhari za kulinda mazingira;

(d) msingi wa "mchafuzi hulipa," unaomtaka mtu yeyote anayesababisha athari katika mazingira kulipa gharama kamili ya kuepuka, kupunguza, na au kurekebisha athari hizo;

(e) msingi wa ushirikishwaji wa umma, unaotaka uhusishwaji wa watu katika maandalizi ya sera, mipango na michakato ya usimamizi wa mazingira;

(f) upatikanaji wa taarifa za mazingira za kuwezesha raia kufanya uamuzi binafsi kutokana na taarifa zinazohimiza utendaji bora wa tasnia na serikali;

(g) upatikanaji wa haki inayotoa kwa watu binafsi, umma na vikundi vya wadau, fursa ya kulinda haki zao, kushiriki na kupinga maamuzi yasiyozingatia maslahi yao;

(h) uzalishaji wa taka upunguzwe kadiri itakavyowezekana na kwa kuzingatia umuhimu wake, taka zitumike upya, zirejelezwe, au zitupwe bila kusababisha athari kwenye mazingira; pale itakaposhindikana basi athari zake kwa mazingira ziwe ndogo sana;

(i) mazingira na maliasili ni muhimu kwa maisha ya binadamu, matumizi yake yawe endelevu ili kupunguza umaskini, na kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi;

(j) maliasili zisizo jadidifu zitumiwe kwa uangalifu ikizingatiwa matokeo kwa kizazi kilichopo na vizazi vijavyo; na

(k) maliasili jadidifu na mifumoikolojia itumike kwa namna ambayo ni endelevu na isiyoathiri utoshelevu na ukamilifu.

(4) Kwa kuzingatia misingi iliyotajwa katika kifungu cha (1), Waziri atakuwa msimamizi mkuu katika kuhimiza uratibu wa uhusiano kati ya Serikali, mamlaka ya serikali za mitaa na asasi nyingine zinazoshughulikia usimamizi wa mazingira kama suala mtambuko, na katika hali hiyo atadumisha utaratibu shirikishi, ushauriano na ushirikiano na mtu yeyote mwenye jukumu chini ya Sheria hii.

**Jukumu la kutekeleza misingi ya usimamizi wa mazingira**

8 Mtu yeyote anayefanya kazi ya umma ambaye katika kutekeleza kazi hiyo, anatakiwa kuchukua hatua yoyote, kutoa uamuzi, kuandaa, kurejea, au kutekeleza sera, mpango, mkakati, sheria, mwongozo au taratibu zozote zinazoweza kuathiri usimamizi, uhifadhi au uendelezaji mazingira au usimamizi endelevu wa maliasili na rasilimali za kiutamaduni,

atazingatia misingi ya usimamizi wa mazingira.

**Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira**

9 Watu wote wanaotekeleza madaraka chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge inayohusiana na usimamizi wa mazingira watalazimika kuhakikisha wanatekeleza na kuzingatia Sera ya Taifa ya Mazingira.

**Siku ya Mazingira**

10 (1) Waziri atateua siku moja maalumu itakayojulikana kuwa Siku ya Mazingira ambapo matukio na shughuli zitaandaliwa kueleza malengo ya siku hiyo, malengo ya Sheria na kuhimiza kujitolea kutekeleza shughuli zinazohusiana na hifadhi, ulinzi na usimamizi wa mazingira.

(2) Serikali, Baraza na asasi husika zote zitajitahidi kuonesha matukio yatakayojenga ari na kutimiza lengo la Siku ya Mazingira.

## SEHEMU YA III
## UTAWALA NA MUUNDO WA ASASI

*(a) Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira*

**Kuanzishwa kwa Kamati na Wajumbe wake**

11 (1) Itaanzishwa Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira itakayomshauri Waziri.

(2) Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira itaundwa na wajumbe wenye uzoefu katika maeneo mbalimbali ya usimamizi wa mazingira kwenye sekta za umma, binafsi na vyama vya kiraia.

(3) Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira itakuwa na wajumbe waliotajwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria hii.

**Kazi za Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira**

12 Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira itamshauri Waziri au Wizara ya sekta yoyote kuhusu suala lolote litakaloelekezwa kwake, hasa -
(a) kuchunguza suala lolote litakaloelekezwa kwake na Waziri au wizara ya sekta yoyote linayohusu kulinda na kusimamia mazingira, pia, kadiri itakavyokuwa, itapendekeza kwa Waziri au Wizara ya sekta, hatua yoyote muhimu itakayofanikisha malengo ya Sheria hii;

(b) kumshauri Waziri kuhusu suala lolote linalohusiana na kurudishia na kudhibiti idadi ya mifugo;

(c) kumshauri Waziri kuhusu masuala yanayohusu kunywesha, kuchunga, kulisha na kuhamisha mifugo;

(d) kupendekeza kwa Waziri pale utokeapo uharibifu wa mazingira;

(e) kupitia upya na kushauri kuhusu viwango, miongozo na kanuni zozote za mazingira zitakazowekwa kwa mujibu wa Sheria hii;

(f) kupokea na kujadili taarifa kutoka wizara za kisekta kuhusu kulinda na kuhifadhi mazingira kwa mujibu wa Sheria hii na sheria nyinginezo zilizotungwa na Bunge; na

(g) kumshauri Waziri kuhusu masuala mengine ya mazingira kadiri itakavyolazimu.

***(b) Waziri Mwenye Dhamana ya Mazingira***

**Mamlaka ya Waziri** 13 (1) Waziri atakuwa msimamizi mkuu wa masuala ya mazingira na kwa mantiki hiyo atatoa miongozo muhimu ya sera ili kukuza, kulinda na kusimamia kiendelevu mazingira nchini Tanzania.

(2) Waziri anaweza kutoa miongozo ya jumla kwa Wizara za Kisekta, Idara za Serikali, Baraza, Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira, Jiji, Manispaa, Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya Wilaya, wakala au asasi nyingine yoyote ya umma au binafsi, miongozo ambayo ni muhimu kwa ajili ya kutekeleza au kufanikisha yaliyoelezwa kwenye Sheria hii.

(3) Waziri anaweza kuteua na itakapolazimu, kuagiza asasi yoyote iliyoelezwa kwenye kifungu cha (2) na kufanya shughuli yoyote au kutofanya kitendo chochote katika muda maalumu ambacho kwa matokeo yake mazingira yanaweza kuhatarishwa au kuathiriwa vibaya sana.

(4) Pale ambapo Waziri ametoa agizo kwa mujibu wa kifungu cha (3) kwa chombo chochote, chombo hicho kitalizingatia au kulitekeleza.

***(c) Mkurugenzi wa Mazingira***

**Mkurugenzi wa Mazingira** 14 Kutakuwa na Mkurugenzi wa Mazingira na maofisa wengine kadiri itakavyoonekana muhimu kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya ofisi ya Mkurugenzi wa Mazingira.

**Kazi za Mkurugenzi wa Mazingira** 15 Katika kusimamia masuala ya mazingira, Mkurugenzi wa Mazingira atafanya yafuatayo–

(a) kuratibu shughuli mbalimbali za kusimamia mazingira zinazofanywa na vyombo vinginevyo na kukuza ufungamanishaji wa masuala ya mazingira katika maandalizi ya sera, mipango, programu, mikakati, miradi ya maendeleo na kufanya tathmini ya kimkakati ya mazingira kwa lengo la kuhakikisha usimamizi madhubuti na matumizi ya kirazini ya rasilimali za mazingira kwa misingi endelevu kwa ajili ya

kuboresha maisha ya binadamu nchini Tanzania;

(b) kuishauri Serikali kuhusu hatua za kisheria nyinginezo za usimamizi wa mazingira au utekelezaji wa mikataba ya kimataifa inayohusu mazingira;

(c) kuishauri Serikali kuhusu mikataba ya kimataifa ya mazingira ambayo Tanzania inapaswa kujiunga au kujitoa;

(d) kufuatilia na kutathmini shughuli zinazofanywa na vyombo husika ili kuhakikisha kuwa mazingira hayaharibiwi na shughuli hizo, malengo ya usimamizi wa mazingira yanazingatiwa na hadhari ya awali ya kutosha inatolewa kuhusu dharura inayoweza kutokea katika mazingira;

(e) kuandaa na kutoa taarifa kuhusu hali ya mazingira nchini Tanzania;

(f) kuratibu masuala yanayohusu maelezo na utekelezaji wa masuala ya usimamizi wa mazingira katika sera za sekta nyinginezo; na

(g) kuratibu hoja zinazohusu maelezo na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira.

***(d) Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira***

**Baraza**

16 (1) Kutakuwa na Baraza litakaloitwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, kwa kifupi, "NEMC".

(2) Baraza–

(a) litakuwa chombo cha kisheria cha kudumu chenye urithi na lakiri;

(b) kwa hali yake kama chombo cha kisheria litaweza kushtaki na kushtakiwa; na

(c) kwa madhumuni ya Sheria hii, Baraza litaweza kumiliki, kununua na vinginevyo, kujipatia, kutoa au kuuza mali inayohamishika au isiyohamishika.

**Lengo la kuanzishwa kwa Baraza**

17 (1) Lengo na madhumuni ya kuanzishwa kwa Baraza ni kusimamia udhibiti, utekelezaji, uzingatiaji, upitiaji upya na upelembaji wa tathmini ya athari kwa mazingira na, kwa ajili hiyo, litawezesha ushirikishwaji wa umma katika uamuzi kuhusu mazingira, kutekeleza usimamizi wa jumla na uratibu wa masuala yote ya mazingira yaliyoelekezwa kwa Baraza kwa mujibu wa Sheria hii au Sheria nyinginezo zilizotungwa na Bunge.

(2) Baraza litatayarisha na kuwasilisha taarifa kwa Waziri kila baada ya miaka miwili kuhusu jinsi lilivyotekeleza Sheria hii na lilivyoitekeleza na kutimiza malengo na madhumuni yake.

**Kazi za Baraza** 18 (1) Katika kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii, Baraza linaweza kufanya yale yote yanayoonekana yana faida au yanafaa na yanahusiana na utekelezaji wa kazi zake au yanayoambatana na utendaji wake na linaweza kutekeleza shughuli yoyote kati ya hizo peke yake au kwa kushirikiana na mtu au kikundi cha watu.

(2) Bila kuathiri kifungu cha (1), Baraza kwa kushirikiana na Wizara za sekta husika:

(a) litafanya ukaguzi wa mazingira unaohusiana na fungu la 101;

(b) litafanya uchunguzi utakaosaidia usimamizi na uhifadhi wa mazingira unaofaa;

(c) litafanya na kuratibu utafiti na uchunguzi kwenye mazingira ili kukusanya na kusambaza taarifa kuhusu matokeo ya utafiti na uchunguzi huo;

(d) litapitia taarifa ya tathmini ya athari za mazingira na kupendekeza kuhusu utoaji wa idhini ya taarifa za athari kwa mazingira;

(e) litabainisha miradi na programu au aina ya miradi na programu, zinazotakiwa kufanyiwa uhakiki wa mazingira au upelembaji wa mazingira chini ya Sheria hii;

(f) litasimamia udhibiti na utekelezaji wa viwango vya ubora wa mazingira kitaifa;

(g) litaanzisha na kubuni taratibu na kinga za kuzuia ajali zinazoweza kusababisha uharibifu wa mazingira na pia kubuni hatua za marekebisho pindi zitokeapo ajali;

(h) litaanzisha programu zinazokusudia kuendeleza elimu ya mazingira na elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa usimamizi mwafaka wa mazingira pamoja na kutambua mchango wa umma na kutia moyo bidii zinazofanywa na vyombo vingine kwa lengo hilo;

(i) litachapisha na kusambaza vitabu vya miongozo, kanuni za kisheria au miongozo kuhusu usimamizi wa mazingira na kuzuia au kupunguza uharibifu wa mazingira;

(j) pale iwezekanapo, litatoa ushauri wa kitaalamu kwa vyombo vinavyojihusisha na usimamizi wa maliasili na mazingira ili kuviwezeshesha kutekeleza wajibu wake; na

(k) litatekeleza kazi nyinginezo kama zitakavyotolewa na Waziri au kama itavyoelekezwa na Waziri au itavyojitokeza chini ya

Sheria hii.

(3) Mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Baraza chini ya fungu hili anaweza kukata rufaa kwa Waziri.

**Bodi ya Baraza**

19 (1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza.

(2) Baraza litasimamiwa na Bodi itakayokuwa na wajumbe wafuatao-

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi wa Mazingira;

(c) Wajumbe saba, walioteuliwa na Waziri kati yao angalau wawili wakiwa wanawake.

(3) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Katibu wa Bodi.

(4) Mtu hatateuliwa chini ya kifungu cha (2) (a) na (c) isipokuwa tu mwenye shahada kutoka chuo kikuu kinachotambuliwa, katika nyanja za taaluma za sheria ya mazingira, sayansi ya afya ya mazingira, usimamizi wa maliasili au sayansi ya jamii husika, au badala yake mtu aliyedhihirisha kuwa na uzoefu na ufahamu kwenye eneo la mazingira.

(5) Wajumbe walioelezwa chini ya ibara (a) na (c) za kifungu cha (2) watateuliwa nyakati tofauti kiasi kwamba kumalizika kwa muda wao wa uteuzi kutatofautiana.

**Uendeshaji wa shughuli na masuala ya Baraza**

20 (1) Bodi itakutana angalau mara tatu kwa mwaka.

(2) Taratibu za kuendesha shughuli za Bodi na kukatisha au kumalizika kwa ujumbe wa Bodi zitakuwa kama ilivyoelezwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria hii.

**Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu**

21 (1) Kutakuwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu.

(2) Mkurugenzi Mkuu atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu ambao, pamoja na kuwa na shahada kutoka chuo kikuu kinachotambulika katika taaluma za sheria ya mazingira, sayansi ya afya ya mazingira, uhandisi wa mazingira, usimamizi wa maliasili, au taaluma nyingine husika, awe na uzoefu angalau wa miaka kumi kwenye eneo husika.

(3) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Ofisa mtendaji mkuu wa Baraza na, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, atawajibika na usimamizi wa shughuli za kila siku za Baraza.

(4) Mkurugenzi Mkuu atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano

na anaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine.

(5) Mkurugenzi Mkuu atawajibika kwa Bodi katika utawala na usimamizi madhubuti wa majukumu na shughuli za Baraza na atatekeleza majukumu mengine kwa kadiri atakavyoelekezwa na Bodi.

(6) Mkurugenzi Mkuu, watumishi na waajiriwa wa Baraza watalipwa mishahara na posho kama itakavyoamriwa na Serikali.

**Watumishi na waajiriwa wa Baraza**

22 Baraza linaweza kuajiri Maofisa wengine au watumishi kadiri litakavyoona ni muhimu kwa utekelezaji unaofaa wa majukumu ya Baraza chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge na kwa masharti ya kazi kadiri itakavyoamriwa na Bodi

**Mamlaka ya jumla ya Baraza**

23 Baraza litakuwa na madaraka kamili ya kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake chini ya Sheria hii na hasa, bila kuathiri madaraka yaliyotajwa kwa ujumla, Baraza litakuwa na mamlaka ya-

(a) kudhibiti na kusimamia mali za Baraza ili kuwezesha kufikia malengo ya Baraza;

(b) kubaini viwango vya upatikanaji wa rasilimali na matumizi ya kawaida, na akiba ya Baraza;

(c) kupokea au kutoa misaada, zawadi, michango au mali iliyowekwa wakfu;

(d) kushirikiana na asasi na jumuia ndani na nje ya nchi kama itakavyoona inafaa ili kudumisha malengo ya Baraza;

(e) kufungua akaunti moja au zaidi za benki kwa ajili ya fedha za Baraza; na

(f) kuwekeza fedha zozote za Baraza ambazo hazihitajiki kwa kipindi hicho kwa madhumuni yaliyoelezwa kwenye fungu la 220.

**Mamlaka ya Baraza kwa mawakala wengineo**

24 (1) Kwa kuzingatia kifungu cha (2), Baraza linaweza, baada ya kutoa ilani ya nia ya kufanya hivyo, kuagiza wakala yeyote kutekeleza, katika muda na namna itakavyoelezwa, wajibu wowote aliopewa wakala chini ya Sheria hii au sheria yoyote iliyoandikwa, na iwapo wakala hatatekeleza agizo hilo, Baraza linaweza kutekeleza au kuhakikisha utekelezaji wa wajibu husika unafanyika, na gharama itakayotokana na kufanya hivyo litakuwa ni deni liwezalo kudaiwa na Baraza kutoka kwa wakala huyo.

(2) Baraza litaomba na kupata kibali kimaandishi kutoka kwa Waziri kabla ya kutekeleza mamlaka yake chini ya fungu hili.

**Mamlaka ya Baraza katika kuhakikisha utekelezaji wa Sheria hii**

25 Baraza litakuwa, na linaweza kutumia madaraka yake kuwezesha kutekelezwa maelekezo yoyote litoayo, pia kwa lengo hilo linaweza kuchukua au kuhakikisha hatua zinachukuliwa, ikiwa ni pamoja na kufungua kesi mahakamani au kwenye Baraza la Rufaa.

**Kukasimu madaraka kwa vyombo vingine**

26 Kwa kuzingatia Sheria hii, Baraza linaweza kukasimu kwa Wizara ya kisekta, chombo cha usimamizi wa mazingira, mwajiriwa au wakala wa Baraza, madaraka yoyote au majukumu ya Baraza chini ya Sheria hii.

**Lakiri ya Baraza**

27 (1) Kutakuwa na lakiri ya Baraza kama itakavyoamriwa na Bodi.

(2) Lakiri ya Baraza haitawekwa kwenye hati yoyote isipokuwa tu mbele ya Mwenyekiti au Katibu au ofisa mwingine wa Baraza, na angalau mjumbe mmoja wa Bodi.

**Kinga kwa Bodi, wajumbe, n.k. kutowajibika binafsi**

28 Suala au jambo lolote lililofanywa na Bodi, mjumbe wa Bodi, mwajiriwa au wakala wa Baraza, iwapo lilifanywa kwa nia njema katika kutekeleza majukumu, mamlaka au wajibu wa Baraza; Bodi, mjumbe, mtumishi au wakala, hawatawajibika nalo binafsi kisheria kuhusiana na kesi, au dai la aina yoyote.

**Mgongano wa maslahi**

29 Ili kuepuka mgongano wa maslahi, upendeleo na kwa madhumuni ya utendaji mzuri, hakuna mwajiriwa, mtumishi wa Baraza, au wakala wa Baraza au mtu yeyote mwenye makubaliano kimkataba na Baraza kufanya mapitio ya tathmini ya athari kwa mazingira, atakayefanya utafiti wa athari kwa mazingira kutokana na kuitikia matakwa ya maelekezo yoyote ya Sheria hii.

***(e) Wizara za kisekta***

**Kuanzishwa kwa sehemu ya mazingira katika kila sekta.**

30 Kutaanzishwa katika kila Wizara sehemu ya mazingira , itakayokuwa na kazi na wajibu utakaoelekezwa kwake chini ya Sheria hii, ikiwa ni pamoja na-

(a) jukumu la kuhakikisha Wizara ya kisekta inatii matakwa ya Sheria hii;

(b) jukumu la kuhakikisha masuala yote ya mazingira ndani ya sheria nyingine zilizopo chini ya wizara ya kisekta husika na inatolewa taarifa ya utekelezaji wake kwa Mkurugenzi wa Mazingira; na

(c) kuwa kiungo kwa Mkurugenzi wa Mazingira na Baraza kuhusu mazingira na yale yanayohitaji ushirikiano au mgawanyo wa majukumu unaofaa au kutakiwa chini ya Sheria hii.

**Kazi za sehemu ya mazingira katika kila**

31 (1) Kila sehemu ya mazingira katika sekta itatakiwa-

(a) kwa kushirikiana na vyombo vingine, kushauri na kutekeleza sera za

**sekta**

Serikali kuhusu kulinda na kusimamia hifadhi ya mazingira;

(b) kuratibu shughuli zinazohusu mazingira ndani ya Wizara;

(c) kuhakikisha masuala ya mazingira yanajumuishwa ndani ya mipango ya maendeleo na utekelezaji wa miradi ya Wizara au idara kwa njia ambayo inalinda mazingira;

(d) kushirikiana na asasi na wakala wengine, kutathimini sera na sheria zilizopo na zinazopendekezwa na kupendekeza hatua za kuhakikisha sera na sheria hizo zinazingatia kikamilifu athari kwenye mazingira;

(e) kuandaa na kuratibu utekelezaji wa mipango tekelezi ya mazingira ngazi za kitaifa na eneoni kama itakiwavyo chini ya Sheria hii;

(f) kuendeleza uhamasishaji umma kuhusu masuala ya mazingira kupitia programu za elimu na usambazaji taarifa;

(g) kutoa taarifa kwa Baraza kuhusu suala lolote la utekelezaji kwa madhumuni ya Sheria hii;

(h) kufanya kazi nyingine muhimu kulingana na madhumuni ya Sheria hii;

(i) kufanya uchambuzi wa athari kwa mazingira zitokanazo na sheria, kanuni, sera, mipango, mikakati na programu za sekta kwa kutumia tathmini ya athari kwa mazingira kimkakati;

(j) kuhakikisha viwango vya kisekta vinakidhi katika kulinda mazingira;

(k) kusimamia matayarisho na utekelezaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira inayohitajika kwa uwekezaji ndani ya sekta hiyo;

(l) kuhakikisha kuwa utekelezaji wa kanuni, miongozo na taratibu zilizotolewa na Waziri unafanyika; na

(m) kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya serikali za mitaa, kutoa ushauri wa mazingira na msaada wa kiufundi kwa watumishi ngazi ya wilaya wanaofanya kazi kwenye sekta husika.

(2) Kila Wizara ya kisekta itatekeleza majukumu na wajibu wake kuhusu mazingira kama ilivyoainishwa kwenye sheria nyingine yoyote ili mradi kwamba sheria hiyo haigongani na yanayoelezwa kwenye Sheria hii.

**Kuwasilishwa kwa taarifa za Wizara za kisekta**

32 (1) Wizara ya kisekta iliyopewa jukumu la usimamizi wa mazingira chini ya sheria yoyote na kupitia kwa Mratibu wa Mazingira wa Sekta, itawasilisha kwa Mkurugenzi wa Mazingira-

(a) taarifa, mara mbili kwa mwaka, kuhusu hali ya sehemu ya mazingira na hatua zilizochukuliwa na Wizara ya kisekta kutunza au kuendeleza mazingira;

(b) mapitio ya sheria ya mazingira iliyopo chini ya Wizara na kiwango cha utekelezaji wake;

(c) kupitia kitengo cha mazingira cha Wizara, kutoa taarifa nyingine zinazoweza kutakiwa na Mkurugenzi wa Mazingira.

(2) Endapo wizara ya kisekta itahisi au kubaini ukiukwaji wa sheria yoyote ya mazingira nje ya uwezo wake wa kuwajibika, kupitia sehemu ya mazingira, bila kuchelewa itamtaarifu Mkurugenzi Mkuu na Wizara ya sekta husika.

**Uteuzi wa mratibu wa mazingira kisekta**

33 (1) Kila Wizara ya kisekta itaajiri au kuteua mtu atakayejulikana kama Mratibu wa Mazingira wa Sekta.

(2) Mratibu wa Mazingira wa Sekta atafanya kazi zifuatazo:

(a) kuratibu shughuli zote na utendaji wa kazi zinazohusu mazingira;

(b) kuzuia na kudhibiti shughuli yoyote iwezayo kusababisha au kuleta uharibifu wa mazingira;

(c) kutoa taarifa ya utendaji na utekelezaji wa masharti ya sheria za mazingira zilizopo chini ya mamlaka ya sekta;

(d) kuwa kiungo kati ya Wizara ya kisekta na Mkurugenzi wa Mazingira na Baraza.

(3) Mratibu wa Mazingira wa Sekta ataajiriwa au kuteuliwa kutokana na maofisa ndani ya kila Wizara ya kisekta na atakuwa mtu mwenye maarifa ya kutosha katika usimamizi wa mazingira.

***(f) Sekretarieti ya Mkoa***

**Uratibu wa usimamizi wa mazingira kimkoa**

34 Sekretarieti ya Mkoa itawajibika na uratibu wa ushauri wowote kuhusu usimamamizi wa mazingira kwenye maeneo husika ya mkoa wake na kuwa kiungo kwa Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu katika kutekeleza na kusimamia Sheria hii.

**Uteuzi wa mtaalamu wa usimamizi wa mazingira wa mkoa**

35 (1) Waziri mwenye dhamana ya tawala za mikoa ataajiri au kuteua mtu atakayejulikana kama Mtaalamu wa Usimamizi wa Mazingira wa Mkoa atakayekuwa na wajibu wa kushauri serikali za mitaa kuhusu masuala ya utekelezaji wa Sheria hii.

(2) Mtaalamu wa Usimamizi wa Mazingira wa Mkoa atakuwa ni kiungo kati ya mkoa na Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu.

***(g) Mamlaka za Serikali za Mitaa***

**Majukumu ya Ofisa Usimamizi wa Serikali za Mitaa**

36 (1)Kila Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Wilaya na Mji itateua au kuajiri Ofisa Usimamizi wa Mazingira ambaye atakuwa Ofisa wa umma na atakuwa-

(a) kwenye eneo la mamlaka ya Jiji, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Jiji;

(b) kwenye eneo la mamlaka ya Manispaa, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Manispaa;

(c) kwenye eneo la mamlaka ya Wilaya, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Wilaya; na

(d) kwenye eneo la mamlaka ya Mji, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Mji.

(2) Mtu aliyeteuliwa au kuajiriwa na Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Wilaya au Mji kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira atakuwa mwenye shahada au stashahada kutoka asasi ya elimu ya juu inayotambulika na mwenye uwezo katika usimamizi wa mazingira

(3) Ofisa Usimamizi wa Mazingira atakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) kuhakikisha utekelezaji wa Sheria hii kwenye eneo lake la kazi;
(b) kushauri Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya eneo lake la kazi kuhusu masuala yote ya mazingira;
(c) kukuza weledi kuhusu ulinzi wa mazingira na uhifadhi maliasili kwenye eneo lake;
(d) kukusanya na kusimamia taarifa kuhusu mazingira na matumizi ya maliasili kwenye eneo hilo;
(e) kuandaa taarifa za mihula kuhusu hali ya mazingira ndani ya eneo husika;
(f) kufuatilia maandalizi, mapitio na vibali vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa ajili ya uwekezaji wa ndani;
(g) kufanya mapitio ya sheria ndogo zinazohusu usimamizi wa mazingira na shughuli maalumu za kisekta zinazohusiana na mazingira;
(h) kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu kuhusu utekelezaji wa Sheria; na
(i) kutekeleza majukumu mengine kwa kadiri mamlaka ya serikali za mitaa itakavyokuwa ikiyatoa.

**Kamati za Kudumu za Mamlaka za**

37 (1) Kamati ya Kudumu ya Mipango Miji na Mazingira iliyoanzishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 42 la Sheria ya Serikali za Mitaa

**Serikali za Mitaa.**

**Sheria Na. 7 na 8 za mwaka 1982**

(Mamlaka za Miji) ya mwaka 1982, pamoja na Kamati ya Kudumu ya Masuala ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira iliyoazishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 74 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982, kila moja itakuwa Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya Jiji, Manispaa au Wilaya kuhusiana na Jiji, Manispaa, na Wilaya kwa kila moja ya Kamati ya Kudumu iliyoanzishwa.

(2) Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya Jiji, Manispaa na Wilaya itatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa chini ya vifungu vya (1) na (2) vya fungu la 55 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) ya mwaka 1982 na kama itakavyokuwa, vifungu vya (1) na (2) vya fungu la 118 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982 pamoja na kanuni zilizotengenezwa chini ya sheria hizo.

(3) Bila kuathiri kifungu cha (2), Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya Jiji, Manispaa na Wilaya pia-

(a) itatekeleza kazi nyingine za ziada kama zilivyobainishwa na Sheria hii au kama, kwa nyakati mbalimbali, itakavyoagizwa na Waziri kwa Jiji, Manispaa au Wilaya kupitia taarifa iliyotangazwa kwenye *Gazeti la Serikali*; na

(b) kutekeleza maagizo yoyote yaliyotolewa kwao na Waziri yanayohusu kuendeleza na kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira.

**Kamati za Kudumu za Miji, Kata, Vijiji na Vitongoji**

38 (1) Kila Kamati ya Kudumu ya Masuala ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ya mji iliyoanzishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 96 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982, kamati maalumu iliyoundwa kufuatana na fungu la 107 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982 pamoja na Kamati ya Maendeleo ya Kata iliyoanzishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 31 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982,yanayohusu eneo ilimoanzishwa Kamati hiyo-

(a) itawajibika kusimamia mazingira kikamilifu yanayohusu eneo ilimoanzishwa;

(b) itatekeleza kazi nyingine za ziada kama zilivyobainishwa na Sheria hii au kama itakavyoagizwa na Waziri au Baraza, kwa kila mmoja au mmojawapo;

(c) itatekeleza maagizo yote yatakayotolewa kwake na Waziri yanayohusu kuendeleza na kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira; na

(d) itatekeleza majukumu au kazi zingine zozote zinazohusiana na usimamizi unaofaa kwa mazingira kama ilivyoelezwa chini ya

Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982.

(2) Kamati ya Maendeleo ya Kijiji ya kila kijiji itawajibika kusimamia kikamilifu mazingira kwenye eneo ilimoanzishwa na kwa utaratibu huo inaweza kufanya majukumu mengine yaliyotolewa chini ya ibara (a), (b), (c) na (d) za kifungu cha (1).

**Uteuzi wa Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji**

39 Halmashauri ya Wilaya itamteua Ofisa wa umma kwa ajili ya kila eneo la utawala la mji, kata, kijiji, Mtaa na Kitongoji ambaye-

(a) kwenye eneo la mamlaka ya mji ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Mji;

(b) kwenye eneo la mamlaka ya Kitongoji ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Kitongoji;

(c) kwenye eneo la mamlaka ya Kata ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Kata;

(d) kwenye eneo la mamlaka ya Mtaa ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Mtaa; na

(e) kwenye eneo la mamlaka ya Kijiji ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Kijiji.

**Kazi za Ofisa Msimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji.**

40 Kazi za Ofisa Usimamizi Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji itakuwa ni kuratibu kazi zote na shughuli zinazolenga kuhifadhi mazingira kwenye eneo la mji, kata, mtaa, kijiji na kitongoji, au kadiri itakavyokuwa ndani ya Wilaya ya eneo husika.

**Madaraka ya jumla ya Kamati za Usimamizi wa Mazingira za Jiji, Manispaa, Wilaya, Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji**

41 Kila Kamati ya Usimamizi wa Mazingira inayohusu eneo ilimoanzishwa, itakuwa na madaraka ya-

(a) kuanzisha uchunguzi na upelelezi kuhusu tuhuma yoyote inayohusu mazingira na utekelezaji au ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii;

(b) kumtaka mtu yeyote kutoa maelezo au taarifa kuhusu suala lolote linalohusu mazingira;

(c) kutatua migogoro kati ya watu binafsi, makampuni, wakala, asasi zisizokuwa za kiserikali, idara au asasi za Serikali, inayohusu majukumu, kazi, uwezo, wajibu au shughuli zao chini ya Sheria hii;

(d) kukagua na kuchunguza makazi, mtaa, gari, ndege au sehemu nyingine yoyote au kitu kinachoaminika au kuna sababu za msingi kuamini kuwa kichafuzi au vitu vingine vinavyoaminika kuwa vichafuzi vimewekwa au vinasafirishwa;

(e) kumtaka mtu yeyote aondoe kwa gharama yake, kitu au dutu yoyote kutoka mahali popote panapoaminika kuwa kitu au dutu hiyo

inaweza kuhifadhiwa kwa usalama au kuharibiwa bila kuleta madhara kwa afya; na

(f) kufungua kesi za madai au jinai dhidi ya mtu yeyote, kampuni, wakala, idara au asasi inayoshindwa au kukataa kufuata agizo lolote lililotolewa na Kamati hizo.

## SEHEMU YA IV
## UANDAAJI MIPANGO YA MAZINGIRA

**Mipango Tekelezi ya Mazingira ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa**

42 (1) Kila mamlaka ya serikali za mitaa, kwenye eneo lake itaandaa Mpango Tekelezi wa Mazingira kwa mujibu wa Mpango Tekelezi wa Mazingira wa Taifa.

(2) Kila Mpango Tekelezi wa Mazingira ulioandaliwa na serikali za mitaa-

(a) utazingatia Mpango Tekelezi wa Mazingira wa Taifa;

(b) utabainisha matatizo sugu ya mazingira katika eneo hilo na kupendekeza hatua za kuyazuia;

(c) utaandaliwa kwa mujibu wa masharti ya Sehemu ya XIV ya Sheria hii; na

(d) utakuwa na masuala yanayoweza kubainishwa chini ya Sheria hii.

**Mipango ya mazingira kisekta**

43 (1) Waziri atatunga kanuni zitakazobainisha maandalizi ya mipango ya mazingira ya kipindi hadi kipindi kwenye ngazi ya kisekta.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "Wizara ya kisekta" itafasiliwa kuwa ni Wizara au Idara au Wakala wa Serikali ambaye kwa muda huo ana dhamana ya sehemu fulani ya mazingira au chombo chochote ambacho shughuli yake inaweza kuathiri mazingira.

(3) Kila baada ya miaka mitano, kila Wizara ya kisekta itaandaa na kuwasilisha kwa Waziri, Mpango Tekelezi wa Mazingira wa Sekta.

(4) Kila Mpango Tekelezi wa Mazingira wa Sekta-

(a) utazingatia Mpango Tekelezi wa Mazingira wa Taifa;

(b) utabainisha matatizo sugu ya mazingira katika eneo hilo na kupendekeza hatua za kuyazuia;

(c) utaandaliwa kwa mujibu wa masharti ya Sehemu ya XIV ya Sheria hii; na

(d) utakuwa na masuala yanayoweza kubainishwa chini ya Sheria hii.

**Uandaaji wa mipango ya mazingira kitaifa**

44 (1) Kila baada ya miaka mitano Mkurugenzi wa Mazingira, kwa kushauriana na Baraza na Wizara ya kisekta, ataandaa na kuwasilisha kwa Waziri Mpango Tekelezi wa Mazingira wa Taifa.

(2) Uandaaji wa Mpango Tekelezi wa Mazingira wa Taifa-

(a) utakuwa msingi wa kufungamanisha masuala yahusuyo mazingira katika uundaji na utekelezaji wa mipango na programu;

(b) utatoa mwongozo wa jumla wa usimamizi na ulinzi wa mazingira na maliasili;

(c) utabainisha matatizo ya msingi ya mazingira yanayoikabili kila sekta ya mazingira;

(d) utapendekeza njia za kukuza ufahamu kitaifa kuhusu umuhimu wa matumizi endelevu ya mazingira na maliasili kwa maendeleo ya taifa;

(e) utazingatia Mipango Tekelezi iliyoandaliwa kwa mamlaka ya serikali za mitaa, Wizara za kisekta na ngazi nyinginezo zilizowekwa na Waziri;

(f) utakuwa na taarifa ya uchambuzi wa kina wa matumizi mbalimbali na thamani ya maliasili itakayojumuisha na kuzingatia masuala ya usawa kati ya kizazi na kizazi;

(g) utapendekeza vivutio vya kisheria na fedha vinavyofaa ambavyo vinaweza kutumika kuhamasisha jumuia ya wafanyabiashara kuhusisha mahitaji ya kuhifadhi mazingira katika mipango na michakato ya uendeshaji;

(h) utabainisha na kutathmini mielekeo ya ukuaji wa makazi mijini na vijijini, athari zake kwa mazingira, na mikakati ya kuondokana na athari zake mbaya;

(i) utapendekeza miongozo ya ufungamanishaji wa viwango vya ulinzi wa mazingira katika mipango ya maendeleo na usimamizi;

(j) utaweka vipaumbele vya maeneo ya utafiti wa mazingira na kueleza kwa muhtasari njia za kutumia matokeo ya utafiti;

(k) utabainisha na kupendekeza njia za kisera na kisheria za kuzuia, kudhibiti au kupunguza athari mbaya mahsusi na pia za jumla kwa mazingira; na

(l) utashughulikia suala lingine lolote litakaloelekezwa na Waziri.

**Kanuni za kuandaa, kukubali na kutekeleza Mipango Tekelezi**

45 Waziri anaweza kutunga kanuni zitakazoagiza taratibu na namna ya kuandaa, kukubali na kutekeleza Mpango Tekelezi wa Mazingira.

**Ushirikishwaji wa umma katika kuandaa Mpango**

46 Wakati wa maandalizi na usambazaji wa Mpango Tekelezi wa Mazingira wa Taifa kwa umma, Waziri, kwa mujibu wa Sehemu ya XIV, atawezesha ushirikishwaji wa umma kwa jumla.

**Tekelezi wa Taifa wa Mazingira**

## SEHEMU YA V
## USIMAMIZI WA MAZINGIRA

*(a) Maeneo ya Hifadhi ya Mazingira*

**Tangazo la Maeneo ya Mazingira Lindwa**

47 (1) Waziri anaweza, kwa pendekezo la Kamati ya Taifa ya Ushauri ya Mazingira, kutangaza eneo lolote la ardhi linaloweza kuharibika upesi kiikolojia au eneo nyeti, kuwa Eneo la Mazingira Lindwa.

(2) Mamlaka aliyopewa Waziri kwa mujibu wa fungu hili hayatahusu maeneo ambayo tayari yametangazwa au yatatangazwa kuwa maeneo lindwa chini ya Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge.

(3) Katika kuamua iwapo eneo litangazwe kuwa Eneo la Mazingira Lindwa au la, Waziri atazingatia mambo yafuatayo:

(a) mawasilisho ya mtu yeyote au asasi zisizo za kiserikali zenye masilahi ya kutosha ya umma au binafsi kwenye eneo;
(b) mandhari asilia na uzuri wa eneo;
(c) mimea na wanyama katika eneo;
(d) mandhari ya kipekee au maalum kijiografia, kifiziolojia, kiikolojia au kihistoria na kiutamaduni ya eneo;
(e) mandhari yoyote ya kipekee ya kisayansi, kiutamaduni au kibioanuwai yaliyomo katika eneo;
(f) maslahi ya jumuia za wenyeji ndani ya eneo na maeneo ya jirani; na
(g) umuhimu wa Serikali kutekeleza wajibu wake wa kimataifa kwa mujibu wa makubaliano yoyote ambayo Tanzania imeridhia.

(4) Usimamizi wa Eneo la Mazingira Lindwa utakuwa chini ya mamlaka ya Baraza.

(5) Waziri atahakikisha kutangazwa kwa Eneo la Mazingira Lindwa katika *Gazeti la Serikali* na kuwa chini ya usimamizi wa Baraza.

**Mpango wa ulinzi wa mazingira na usimamizi wa mifumoikolojia kwa ajili ya maeneo ya mazingira lindwa**

48 (1) Pale ambapo eneo litatangazwa kuwa Eneo Mazingira Lindwa, Baraza, kwa kushauriana na sekta husika, litaandaa mpango wa ulinzi wa mazingira kwa ajili ya eneo hilo.

(2) Mpango wa ulinzi wa mazingira-

(a) utaweka malengo ya kulinda na kusimamia eneo;
(b) utaweka sera za kulinda na kusimamia eneo;

(c) utaandaa mikakati ya kulinda na kusimamia eneo;
(d) utawezesha uendelezaji wa huduma za jamii na fursa za burudani inapobidi;
(e) utawezesha kufanyika utafiti wa kisayansi; na
(f) utajumuisha mahitaji yote muhimu ya mipango ya usimamizi wa mazingira.

(3) Bila kujali masharti ya vifungu vya (1) na (2), Baraza linaweza kuandaa mpango wa usimamizi wa mfumoikolojia wa Eneo Mazingira Lindwa.

### *(b) Mipango ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maeneo Lindwa ya Taifa*

**Mipango ya usimamizi wa mazingira kwa ajili ya maeneo Lindwa ya Taifa**

49 (1) Kila eneo lindwa la taifa litaongozwa na kusimamiwa kwa mujibu wa sheria inayolilinda.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu cha (1), kila mamlaka ya usimamizi wa eneo lindwa la taifa itaandaa na kutekeleza mpango wa usimamizi wa mazingira ambao-
(a) unatambua maeneo yenye bioanuwai;
(b) unatambua jamii zinazohusika, watumiaji wengine na asasi nyingine husika;
(c) unaeleza kazi za ugani na elimu kwa jamii na watumiaji wengine kuhusu uanzishwaji wa maeneo lindwa;
(d) unaonyesha gharama na manufaa ya ulinzi wa eneo kwa utaratibu wa haki kwa watu waliotambulishwa katika kifungu cha (2)(b);
(e) unaeleza mipaka ya eneo lindwa la taifa;
(f) unafafanua hatua za usimamizi zitakazochukuliwa ndani ya eneo lindwa la Taifa;
(g) unaeleza kanuni zinazotumika kwenye eneo lindwa la Taifa;
(h) unabainisha namna ya kufuatilia utekelezaji wa mpango;
(i) unaeleza suala lingine lolote lihusulo usimamizi bora wa mazingira kwenye eneo lindwa la taifa;
(j) unaidhinishwa na mamlaka husika yenye dhamana chini ya sheria ya eneo lindwa husika; na;
(k) umetangazwa, na pale inapofaa, utangazwe kwenye *Gazeti la Serikali* na Waziri mwenye dhamana ya mifumo ya maeneo lindwa ya taifa.

(3) Hatua ya usimamizi itakayoweza kuchukuliwa chini ya kifungu cha (2)(f) inaweza kujumuisha-
(a) kugawa katika kanda;
(b) masharti ya fursa ya utumiaji;
(c) masharti ya matumizi;
(d) kugawana manufaa;
(e) ada ya kuingia na vibali; na

(f) hatua zingine zozote zitakazodhaniwa zinafaa kwa matumizi mazuri na bora ya eneo.

### *(c) Hifadhi na Ulinzi*

**Usimamizi wa matumizi ya ardhi**

50 Usimamizi na matumizi ya ardhi utakuwa kwa mujibu wa sheria za ardhi zilizopo isipokuwa tu pale penye mgongano wowote kwenye suala linalohusu mazingira katika usimamizi wa ardhi, masharti ya Sheria hii yatatumika.

**Maeneo ya mazingira nyeti**

51 (1) Pale Waziri atakapoona inabidi, anaweza kutangaza kwa amri itakayotangazwa kwenye *Gazeti la Serikali*, eneo lolote kuwa mazingira nyeti kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Usimamizi wa eneo la mazingira nyeti kwa mujibu wa fungu hili utafanywa kwa kuzingatia taratibu zitakazotolewa na Waziri.

(3) Mtu yeyote atakayeshindwa, kupuuza au kukataa kuzingatia taratibu zilizobainishwa katika kusimamia maeneo ya mazingira nyeti , atakuwa anatenda kosa.

**Utambuzi wa maeneo ya mazingira nyeti**

52 Bila kuathiri fungu la 51, kwa madhumuni ya Sheria hii maeneo ya ardhi yafuatayo yatakuwa maeneo ya mazingira nyeti –

(a) vinamasi;

(b) eneo lolote lililotangazwa na mamlaka ya serikali za mitaa kuwa ni eneo la mazingira nyeti;

(c) eneo lililodhihirishwa na Baraza kuwa lipo hatarini kuathiriwa na mmomonyoko wa udongo;

(d) ardhi iliyotengwa na Baraza kuwa ardhi ambapo yametokea au yanaelekea kutokea maporomoko ya ardhi;

(e) maeneo yote ambayo Waziri amezuia ufugaji, makazi, kilimo na shughuli nyinginezo zilizoainishwa;

(f) eneo kwenye miteremko yenye mwinamo unaozidi pembe yoyote ambayo Waziri atabainisha, baada ya kuzingatia ushauri mwafaka wa kisayansi;

(g) ardhi kame na nusu kame;

(h) ardhi ambayo imebainishwa na Baraza kuwa ardhi isiyopaswa kuendelezwa kutokana na hali yake ya kuharibika kwa urahisi au umuhimu wake kwa mazingira; na

(i) ardhi iliyotangazwa kwa mujibu wa sheria yoyote nyingineyo iliyotungwa na Bunge kuwa ni eneo la mazingira nyeti au ni ardhi yenye madhara.

**Masharti ya hifadhi ya mazingira kwenye ardhi ya Vijiji**

53 Licha ya masharti na mashuruti yaliyobainishwa na fungu la 29 la Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999, kuhusu ardhi ya Vijiji au utaratibu kuhusu matumizi ya ardhi kwa pamoja kati ya wafugaji na wakulima kwa mujibu wa fungu la 58 la Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999, Waziri anaweza kubainisha masharti mengine ya ziada yanayohusu kulinda mazingira, masharti ambayo yatazingatiwa na watakaopewa hakimiliki za kimila.

**Kutangazwa mito, kingo za mito, maziwa au miambao ya maziwa na fukwe lindwa.**

54 (1) Bila kujali sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge kwa wakati huu inayosimamia mito, kingo za mito, maziwa au miambao ya maziwa na fukwe, Waziri kwa kushauriana na Wizara zingine husika, kwa notisi iliyotangazwa kwenye *Gazeti la Serikali*, anaweza-

(a) kutangaza mto, ukingo wa mto, ziwa, mwambao wa ziwa au ufukwe, kuwa eneo lindwa kwa madhumuni ya Sheria hii; na

(b) kuweka masharti yoyote ambayo ataona ni muhimu kwa ajili ya kulinda mto, ukingo wa mto, ziwa, au ufukwe husika, ili kuepuka uharibifu wa mazingira.

(2) Waziri anapotumia madaraka yake kwa mujibu wa kifungu cha (1), atazingatia-

(a) ukubwa kijiografia wa mto, ukingo wa mto, ziwa, au ufukwe;

(b) maslahi ya jamii ya wakazi karibu na mto, ukingo wa mto, ziwa, au ufukwe;na ushauri wowote unaoweza kutolewa na Wizara za kisekta.

**Ulinzi na usimamizi wa mito, miambao ya mito, maziwa au miambao ya maziwa na fukwe.**

55 (1) Bila kuathiri masharti yoyote ya sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge, Baraza na mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika na masuala ya mazingira, zitatoa miongozo na kubainisha hatua za kilinda, kingo za mito, mito, maziwa au miambao ya maziwa na fukwe.

(2) Pale ambapo miongozo na hatua zitakapokuwa zimebainishwa kufuatia kifungu cha (1), litakuwa ni kosa kufanya shughuli yoyote kati ya hizi zifuatazo bila kwanza kupata ruhusa au kibali kilichotolewa na Waziri-

(a) kutumia, kusimika, kujenga, kuweka, kubadili, kuongeza, kuondoa, au kubomoa jengo au umbile kwenye au chini ya bahari au fukwe asili za ziwa, ukingo wa mto au bwawa;

(b) kufukua, kuchoronga, kutoboa au kuharibu fukwe za bahari au

ziwa asili, kingo za mto au kisima cha maji au bwawa;

(c) kupandikiza mmea au sehemu yoyote ya mmea, kupandikiza sampuli ya mmea wa kigeni au wa asili uliokufa au ulio hai katika mto unaoingia baharini, kingo za mto au mwambao wa ziwa;

(d) kutupa kitu kwenye mto, kingo za mto, ziwa au, ufukwe wa ziwa, ufukwe au ardhi oevu au ndani au chini yake, kiwezacho kuwa na athari mbaya kwa mazingira kwenye mto, kingo za mto, ziwa, fukwe za ziwa au ardhi oevu;

(e) kuchepusha au kuzuia mto, ukingo wa mto, ziwa au, mwambao wa ziwa, ufukwe au ardhi oevu kutoka mkondo wake wa asili;

(f) kukausha mto au ziwa.

(3) Mtu yeyote anayekiuka masharti ya fungu hili anatenda kosa.

(4) Waziri anaweza kukasimu madaraka yake chini ya fungu hili kwa Mkurugenzi wa Mazingira, au Ofisa wa mamlaka ya serikali za mitaa au Ofisa kwenye Wizara ya kisekta.

**Tangazo la ardhi oevu lindwa.**

56 (1) Waziri, baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya ardhi, atatangaza eneo la ardhi yoyote kuwa ardhi oevu lindwa chini ya Sheria hii.

(2) Kwa madhumuni ya usimamizi wa ardhi oevu iliyotangazwa chini ya kifungu cha (1), Wizara za kisekta zenye mamlaka kwenye eneo linalohusika na ardhi oevu, zitawajibika kusimamia ardhi oevu iliyopo chini ya mamlaka hizo.

(3) Waratibu wa mazingira kisekta watatoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mazingira kuhusu usimamizi na hali ya ardhi oevu iliyoko chini ya mamlaka yao.

(4) Masharti yaliyobainishwa katika kifungu 55(2) vivyo hivyo yakifanyiwa marekebisho muhimu yatatumika kwa ardhi oevu.

(5) Waziri, kwa kushauriana na Wizara nyingine za kisekta anaweza kutengeneza kanuni na miongozo ya usimamizi endelevu wa ardhi oevu lindwa chini ya Sheria hii.

**Kuzuia shughuli za binadamu katika baadhi ya maeneo.**

57 (1) Kwa kuzingatia kifungu cha (2), ndani ya mita sitini hakutafanyika shughuli yoyote ya binadamu ya kudumu au ambayo kwa asili yake inaweza kuhatarisha au kuathiri vibaya ulinzi wa mazingira na, au utunzaji wa bahari au kingo za mto, bwawa, au miambao ya asili ya ziwa.

(2) Waziri anaweza kuweka miongozo ya kuendesha shughuli za binadamu ndani ya maeneo yaliyoelezwa kwa mujibu wa kifungu cha

(1).

**Ulinzi wa milima, vilima na mandhari.**

58 (1) Baraza, kwa kushauriana na mamlaka ya serikali za mitaa, ndani ya miaka mitano ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, litabainisha maeneo ya vilima na milima ambayo mazingira yake yako katika hatari ya kuharibika.

(2) Eneo lenye vilima au milima litachukuliwa kuwa mazingira yake yako katika hatari ya kuharibika iwapo-

(a) lina uwezekano wa kuathiriwa na mmomonyoko wa udongo;
(b) kumetokea au kuna mwelekeo wa kutokea maporomoko ya ardhi katika eneo hilo;
(c) mimea imeondolewa au inaelekea kuondolewa kutoka kwenye eneo hilo kwa kasi kubwa kuliko inavyorudishiwa; au
(d) kuna shughuli nyingine yoyote ya matumizi ya ardhi kwenye eneo hilo iwezayo kusababisha uharibifu wa mazingira.

(3) Waziri, kwa Amri itakayochapishwa katika *Gazeti la Serikali,* atatangaza orodha ya maeneo ya mandhari ya nchi, milima na vilima yanavyochukuliwa kuwa yako katika hatari ya mazingira yake kuharibiwa.

(4) Orodha ya maeneo yote yaliyotengwa katika kifungu cha (3) itatunzwa na Baraza na maeneo hayo yatachukuliwa kuwa ni maeneo lindwa, na Baraza litabainisha mikakati ya kuyasimamia.

**Kuendeleza usimamizi wa mazingira ya pwani**

59 Waziri, baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya mamlaka ya serikali za mitaa na asasi nyingine husika, atatengeneza kanuni za kuendeleza usimamizi fungamanishi wa mazingira katika ukanda wa pwani.

**Masharti ya mazingira katika sheria za maji**

60 (1) Mwombaji yeyote wa kibali cha kutumia maji kinachotolewa chini ya sheria husika zinazotawala usimamizi wa raslimali maji, kutoa na kutumia maji, atatakiwa kutoa tamko kuhusu uwezekano wa athari kwa mazingira kutokana na matumizi ya maji yaliyoombwa.

(2) Kwa madhumuni ya kuweka kumbukumbu za masuala yanayoathiri mazingira kwa sababu ya kutoa na kutumia maji, Bodi za Maji ya Bonde zitawasilisha taarifa za mwaka kwa Mratibu wa Mazingira wa Sekta zikionyesha kiwango cha uzingatiaji wa masharti yafuatayo kwa mwenye kibali cha kutumia maji-

(a) wajibu wa urejeshwaji wa maji kwenye chanzo cha maji yalikochukuliwa baada ya kuyatumia;
(b) kuhakikisha kuwa maji yaliyorejeshwa kwenye chanzo chochote kilichoelezwa hayakuchafuliwa;

(c) kuchukua hadhari kwa kiwango kitakachomridhisha Ofisa wa Maji kuzuia mkusanyiko kwenye mto wowote, kijito au njia ya maji yenye mchangatope, mchanga, kokoto, mawe, takataka za vumbi la mbao, njia ya maji taka, taka za mkonge au kitu kingine chochote kinachoweza kuleta madhara kutokana na matumizi ya maji hayo kwa binadamu na sehemu nyinginezo za mazingira.

(3) Bodi za Maji ya Bonde katika kuweka vipaumbele vya matumizi mbalimbali ya maji zitahakikisha kuwa maji ya kutosha yanapatikana kwa ajili ya mazingira.

**Waziri anaweza kushauri kuhusu umwagaji wa maji taka.**

61 Bila kuathiri madaraka ya mamlaka ya serikali za mitaa kuhusu umwagaji wa maji taka, Waziri anaweza kushauri, na inapofaa, kutoa maelekezo yoyote kwa mtu yeyote, ofisa au mamlaka kuhusu umwagaji huo.

**Ushauriano kuhusu umwagaji vichafuzi.**

62 Waziri atashauriana na kumshauri Waziri mwenye dhamana ya maji kuhusu utengenezaji wa kanuni zinazotawala utoaji wa vibali vya kumwaga maji taka kutoka viwandani.

**Usimamizi wa raslimali za misitu.**

**Sheria Na. 14 ya mwaka 2002**

63 (1) Misitu yote itasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 na masuala yahusuyo mazingira yatazingatia masharti ya Sheria hii.

(2) Pale ambapo suala lolote lihusianalo na usimamizi wa mazingira unaofanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Misitu ya mwaka 2002, linapogongana na masharti ya Sheria hii, Sheria hii itatumika.

(3) Waziri, katika kutunga kanuni za kusimamia mazingira ya rasilimali za misitu, atashauriana na Waziri mwenye dhamana ya misitu.

**Uendelezaji hifadhi ya nishati**

64 Waziri, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya misitu au kadiri itakavyokuwa, nishati, ataendeleza matumizi ya vyanzo vya nishati jadidifu kwa-

(a) kuendeleza utafiti wa vyanzo vya nishati jadidifu vinavyofaa;

(b) kubuni motisha za kuendeleza vyanzo vya nishati jadidifu;

(c) kuendeleza sera na hatua za kuhifadhi vyanzo vya nishati jadidifu;

(d) kuchukua hatua za kushawishi upandaji miti na vitalu vya miti kwa watumiaji binafsi, asasi na vikundi vya jumuia.

**Uendelezaji wa hifadhi ya rasilimali za uvuvi na wanyamapori**

65 (1) Rasilimali zote za samaki zitasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 na Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ya mwaka 1994.

**n.k.**

**Sheria Na. 22 ya mwaka 2003; Sheria Na. 29 ya mwaka 1994**

(2) Rasilimali za wanyamapori zitasimamiwa kwa mujibu wa masharti ya sheria inayohusika na masuala ya wanyamapori.

(3) Shughuli zote za utalii zitaongozwa na kusimamiwa kwa mujibu wa sheria zinazohusika na utalii.

(4) Pale ambapo suala lolote linalohusu usimamizi wa mazingira linalofanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003, Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ya mwaka 1994, sheria zozote zinazohusika na masuala ya wanyamapori na utalii, litakapogongana na Sheria hii, Sheria hii itatumika.

**Hifadhi ya bioanuwai.**

66 (1) Waziri atajitahidi kufanikisha hifadhi ya bioanuwai, matumizi endelevu ya vijenzi vyake na mgawanyo kwa utaratibu wa haki manufaa yatokanayo na matumizi ya rasilimali za kijeni.

(2) Mamlaka ya Waziri chini ya fungu hili yatahusisha kwa ujumla kuratibu fursa mwafaka ya kupata rasilimali za kijeni inayofaa na uhamisho wa teknolojia zinazohusika, kwa kuzingatia haki zote kwenye rasilimali hizo, elimu ya asili, maarifa ya ufundi na ugharamiaji unaofaa.

(3) Waziri, kwa kuzingatia hali mahususi yoyote na uwezo, na baada ya kushauriana na Wizara ya sekta husika, anaweza kutunga kanuni zinazoagiza:-

(a) kutengeneza mikakati, programu na mipango ya kitaifa ya hifadhi na matumizi endelevu ya bioanuwai;

(b) marekebisho ya mikakati, mipango au na taratibu zilizopo kwa madhumuni ya kuhifadhi bioanuwai;

(c) ufungamanishaji, kwa kadiri iwezekanavyo na ifaavyo, hifadhi na matumizi endelevu ya bioanuwai kwenye mipango, taratibu na sera za kisekta na sekta mtambuko husika;

(d) utambuaji wa vijenzi vya bioanuwai muhimu kwa hifadhi na matumizi endelevu, kwa kuzingatia viwango vyovyote vya kimataifa vinavyotumika Tanzania;

(e) upelembaji kwa kuchukua sampuli na mbinu zingine, vijenzi vya bioanuwai, kwa kuzingatia zaidi zile zinazohitaji hatua za haraka za hifadhi na zile zinazoleta kwa kiasi kikubwa matumizi endelevu;

(f) kubaini michakato na aina za shughuli zenye au zinazoweza kuwa na athari mbaya kwenye kuhifadhi kwa utaratibu wa haki na matumizi endelevu ya bioanuwai, na kufuatilia madhara yake kwa kuchukua sampuli na mbinu zingine; na

(g) matunzo na mpangilio:

(i) kwa utaratibu wowote; au

(ii) takwimu zilizotokana na shughuli za utambuzi na upelembaji kutokana na fungu hili.

**Hifadhi ya bioanuwai mahali asilia**

67 (1) Waziri, kwa kushauriana na Wizara ya sekta husika, anaweza kutengeneza kanuni zinazoelekeza hifadhi ya bioanuwai mahali asilia.

(2) Kanuni zilizotengenezwa chini ya fungu hili zinaweza kubainisha:

(a) taratibu za kuanzisha mifumo ya maeneo lindwa au maeneo ambapo hatua maalumu zinatakiwa kuchukuliwa kuhifadhi bioanuwai;
(b) miongozo ya kuchagua, kuanzisha na kusimamia maeneo lindwa au maeneo ambapo hatua maalumu zinatakiwa kuchukuliwa kuhifadhi bioanuwai;
(c) namna ya kuratibu au kusimamia rasilimali za kibiolojia muhimu kwa hifadhi ya bioanuwai iwe zilizomo ndani au nje ya maeneo lindwa, kwa kusudi la hifadhi na matumizi endelevu;
(d) kuendeleza ulinzi wa mifumoikolojia, makazi ya asili ya viumbe hai na kutunza wanyama au mimea ya spishi ziwezekanazo kuwemo kwenye eneo asilia;
(e) ukuzaji wa mazingira yakubalikayo kwa maendeleo endelevu kwenye maeneo yanayopakana na maeneo lindwa kwa lengo la kuboresha zaidi ulinzi wa maeneo haya;
(f) ukarabati na urejeshaji mifumoikolojia iliyoharibiwa na kuendeleza urejeshwaji wa spishi zilizoko hatarini, pamoja na mengineyo, kwa kuendeleza na kutekeleza mipango na mikakati mingine ya usimamizi;
(g) kubaini na kusimamia hatari zinazohusiana na viumbe ambavyo nasaba zake zimefanyiwa mabadiliko kijeni kutokana na bioteknolojia ya kisasa, na viwezavyo kuwa na athari mbaya kwa mazingira kiasi cha kuathiri hifadhi na matumizi endelevu ya bioanuwai, pia kwa kuzingatia hatari kwa afya ya binadamu vilevile matakwa ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kimaadili;
(h) kuzuia uingizaji, udhibiti au uondoaji spishi za kigeni ziwezazo kuhatarisha mifumoikolojia, makazi ya viumbe hai au spishi asilia;
(i) kutoa masharti yanayoweza kuhitajika kufungamanisha matumizi yaliyopo na hifadhi ya bioanuwai na matumizi endelevu ya vijenzi vyake;
(j) miongozo ya njia za kuheshimu, kutunza na kudumisha elimu, ubunifu, na utendaji wa asili wa wenyeji;
(k) kuchukua hatua zinazokubalika kiuchumi na kijamii zitumikazo kama motisha kwa ajili ya uhifadhi na matumizi endelevu ya vijenzi vya bioanuwai;
(l) kuendeleza na kuhimiza ushirikiano kwa utaratibu wa haki katika manufaa yanayotokana na matumizi kama ya elimu, ubunifu na

utendaji; na

(m) taratibu za kuanzisha mfumo au mifumo ya maeneo lindwa au maeneo ambamo hatua maalumu zinatakiwa kuchukuliwa kuhifadhi bioanuwai.

**Hifadhi ya bioanuwai mahali pasipo asilia.** 68 Waziri, kwa kushauriana na Wizara husika, anaweza kutunga kanuni zinazohusu hifadhi mahali pasipo asilia zikielekeza hatua zifuatazo:

(a) kuchukua hatua za kuhifadhi vijenzi vya bioanuwai vyenye asili ya Tanzania;

(b) kuanzisha na kutunza huduma za hifadhi mahali pasipo asilia na utafiti unaohusu mimea, wanyama na vijiumbe, hasa kwenye nchi asili ya rasilimali za kijeni;

(c) kuchukua hatua za urejeshwaji na urekebishwaji wa spishi zilizomo hatarini na kwa kuzianzisha tena kwenye makazi yake ya asili katika hali inayofaa;

(d) kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa rasilimali za kibiolojia kutoka makazi ya asilia kwa malengo ya kuhifadhi mahali pasipo asilia ili kuepuka kuleta tishio kwa mifumoikolojia na idadi ya spishi zilizohifadhiwa mahali asilia;

(e) kuchukua hatua zinazokubalika kiuchumi na kijamii ziwezazo kutumika kama motisha ya uhifadhi na matumizi endelevu ya vijenzi vya bioanuwai; na

(f) kushiriki katika kutoa misaada ya kifedha na mingineyo kwa ajili ya hifadhi mahali pasipo asilia.

**Kanuni za kuendeleza, kushughulikia na kutumia viumbe vilivyobadilishwa nasaba kijeni na mazao yake.** 69 (1) Bila kuathiri sheria yoyote inayohusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa, mtu yeyote mwenye kuendeleza, kushughulikia, kutumia, kuingiza ndani au kutoa nje ya nchi viumbe hai vilivyobadilishwa nasaba kijeni na, au mazao yake, atakuwa na wajibu wa jumla wa kuhakikisha viumbe hai hivyo haviathiri, au kusababisha uharibifu au upotevu wa mazingira na afya ya binadamu ikiwa ni pamoja na matakwa ya kiuchumi jamii, kiutamaduni na kimaadili.

(2) Madhara, uharibifu au upotevu unaohusisha madhara binafsi, uharibifu wa mali, upotevu wa fedha, na uharibifu wa mazingira au bioanuwai.

(3) Kwenye fungu hili "viumbe" maana yake ni kitu chochote hai, hatua dhaifu au bwete ya maisha ya kitu chenye sifa ya kuishi, pamoja na mimea, bakteria, kuvu, mikoplasma, wanyama wenye uti wa mgongo na wasio na uti wa mgongo, vilevile vitu kama, virusi au kitu chochote hai chenye uhusiano nacho.

**Usimamizi wa** 70 (1) Waziri kwa kushauriana na Mawaziri wa sekta husika, anaweza kutoa

**ardhi ya malisho.**

miongozo na kuelekeza hatua za usimamizi na matumizi endelevu ya ardhi ya malisho ya mifugo.

(2) Katika kutoa miongozo na kuelekeza hatua zilizoelezwa kwenye kifungu cha (1), Waziri atazingatia-

(a) uhimili wa ardhi;

(b) hifadhi ya udongo;

(c) hatari ya kuwa jangwa inayoikabili ardhi ya malisho ya mifugo;

(d) suala lingine lolote ambalo Waziri, kwa kushauriana na Mawaziri wa sekta husika, anaweza kuona linafaa.

**Miongozo ya mipango ya matumizi ya ardhi.**

71 Waziri, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya ardhi, anaweza kutoa maagizo ya jumla au mahususi kuhusu mipango ya mazingira na matumizi ya ardhi ambayo yatahusishwa au kuzingatiwa na-

(a) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi;

(b) Kamati za Mipango Miji zilizoanzishwa chini ya sheria inayohusika na mipango miji;

(c) mamlaka za maji taka;

(d) mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika na kazi zozote za mipango vijijini au mijini;

(e) mamlaka za serikali za mitaa husika katika kuandaa kanuni zozote za matumizi ya ardhi zinazotenga maeneo kwa ajili ya makazi, biashara, viwanda, malisho na kilimo; na

(f) asasi nyingine yoyote inayotekeleza wajibu unaohusu matumizi ya ardhi.

**Wajibu kuhusu matumizi endelevu ya ardhi.**

72 Watumiaji na wamiliki wa ardhi watawajibika kuitunza, kuiendeleza na kuiboresha, na kuitumia katika hali endelevu ya mazingira kama itakavyoelekezwa na Waziri.

**Kulinda urithi asilia na wa kiutamaduni.**

73 (1) Suala au shughuli yoyote inayohusu kutunza au kuhifadhi urithi wa kiutamaduni itazingatia matakwa muhimu ya kutunza mazingira kama ilivyoelezwa chini ya Sheria hii.

(2) Pale suala lolote lihusulo usimamizi wa mazingira lifanywapo kwa mujibu wa sheria yoyote iliyopo, linapogongana na Sheria hii, Sheria hii itatumika.

**Hifadhi ya angahewa.**

74 (1) Waziri, kwa kushauriana na Wizara ya sekta husika, ataweza-

(a) kufanya au kuagiza watu wengine kufanya uchunguzi wa kitaifa

na kutambua maendeleo katika maarifa ya kisayansi yanayohusu vitu, kazi na vitendo vinavyoondoa tabaka la ozoni ya stratosfia na vijenzi vya stratosfia, kiasi cha kuathiri afya ya umma na mazingira;

(b) kutoa miongozo, na kuanzisha programu zinazohusu-

(i) kuondoa dutu zinazoharibu tabaka la ozoni; au

(ii) vitendo na shughuli za usimamizi zinazoweza kusababisha uharibifu wa tabaka la ozoni na stratosfia; au

(iii) kupunguza hatari kwa afya ya binadamu zitokanazo na uharibifu wa tabaka la ozoni na stratosfia.

(2) Waziri atatunga kanuni za kudhibiti uingizaji ndani na utoaji nje ya nchi na matumizi ya dutu zinazoharibu ozoni au vifaa husianifu.

**Hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.**

75 Waziri, kwa kushauriana na Wizara za sekta husika:

(a) atachukua hatua za kukabili mabadiliko ya tabianchi, hususani athari za mabadiliko ya tabianchi na hatua za marekebisho;

(b) kila baada ya kipindi fulani, atatoa miongozo kwa Wizara na asasi zingine ili kukabili mabadiliko ya tabianchi na athari zake;

(c) atazitaka Wizara na idara za Serikali zinazojitegemea kuweka mikakati na mipango ya utekelezaji ili kushughulikia mabadiliko ya tabianchi na kushauri shule na asasi za elimu ya juu kuhusisha kwenye mitaala yao masuala yanayohusu mabadiliko ya tabianchi;

(d) atafanya mapitio na kuidhinisha hatua zozote za kukabili mabadiliko ya tabianchi zinazochukuliwa na asasi, shirika, sekta au watu binafsi, ziwe ni kutoka nje au ndani ya nchi, pamoja na hatua zinazohusiana na matumizi ya ardhi, maji, misitu na mifumoikolojia mingine yoyote ndani ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kupunguza gesi zinazosababisha ongezeko la joto duniani; na

(e) ataelekeza nafasi na msimamo wa kitaifa katika ngazi ya kimataifa zinazohusu namna ya kushughulikia tatizo la mabadiliko ya tabianchi kulingana na Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi.

**Usimamizi wa mazingira ya kazi na maunzi na michakato hatari.**

76 (1) Waziri, kwa kushauriana na Wizara husika, anaweza kuagiza hatua za kuboresha mazingira ya kazi.

(2) Waziri anaweza kisheria kubainisha mchakato wowote wa vitu kuwa ni mchakato hatari ambao kufanyika kwake au utoaji wake wa maunzi hatari kwenye mazingira, unalazimika kudhibitiwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(3) Kanuni zilizotungwa na Waziri kufuatia kifungu cha (2) zinaweza-

(a) kubainisha mazingira tofauti ambayo utoaji wa dutu kwenye mazingira hayo ni lazima udhibitiwe;

(b) kueleza kuwa ufafanuzi wa dutu ni ubainishaji tu kwa tabia ya wastani ya kimazingira pale inapowekwa kwenye tabia hiyo ya wastani kwa viwango katika vipindi na kwa mikolezo au katika hali nyingine za namna hiyo zinazoweza kubaishwa kwenye kanuni; na

(c) kuweka masharti ya kibali na masuala yatokanayo na kibali cha kuidhinisha mchakato na utoaji wa dutu kwenye mazingira.

**Mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kuhusu vichafuzi dumufu vya kikaboni.**

77 (1) Kwa lengo la kuondoa utoaji wa vichafuzi dumufu vya kikaboni:

(a) kila Wizara ya kisekta itachukua hatua muhimu kisheria na kiutawala kupunguza au kuondoa vichafuzi dumufu vya kikaboni viliyozalishwa kwa makusudi wakati wa uzalishwaji, matumizi, uingizwaji na utolewaji nchini kwa mujibu wa masharti ya Mkataba wa Stockholm;

(b) Mkurugenzi wa Mazingira, kwa kushauriana na Wizara za sekta husika, anaweza kuweka orodha ya kemikali ambazo Serikali inaweza kuziombea kibali cha msamaha maalum chini ya Mkataba huo; na

(c) kila Wizara ya kisekta itachukua hatua za kupunguza jumla ya kiasi kinachoachiwa kutokana na shughuli za binadamu za vichafuzi dumufu vya kikaboni visivyoachiwa kwa makusudi.

(2) Waziri kwa kuchapisha kanuni kwenye *Gazeti la Serikali*, atabainisha vichafuzi dumufu vya kikaboni ambavyo havitatumika.

(3) Mkurugenzi wa Mazingira ataandaa na kusimamia mpango wa kitaifa wa utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm kama ilivyoelezwa kwenye Mkataba.

(4) Wizara zote za sekta husika na mamlaka za serikali za mitaa zitaingiza sehemu husika za Mpango wa Taifa wa Utekelezaji kwenye sera, sheria, mipango na programu zake, na kuwasilisha taarifa za mwaka kwa Waziri kuhusu hatua iliyofikiwa katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Utekelezaji.

(5) Bila kuathiri sheria yoyote iliyopo na inayotumika, Waziri atakuwa na mamlaka ya kutunga kanuni zinazoeleza masuala yafuatayo yanayohusu vichafuzi dumufu vya kikaboni -

(a) kutimiza wajibu wa kimataifa kuhusu vichafuzi dumufu vya kikaboni na viuavisumbufu;

(b) kutekeleza Mkataba wa Stockholm kuhusu Vichafuzi Dumufu vya Kikaboni wa mwaka 2001;

(c) kukuza utambuzi wa njia mbadala ambazo ni endelevu katika kubadilisha vichafuzi dumufu vya kikaboni;

(d) kuweka orodha ya vichafuzi dumufu vya kikaboni;

(e) kutupa vichafuzi dumufu vya kikaboni vilivyopo;

(f) kuhusisha tasinia hususani kuchangia gharama za kutupa na kuchukua jukumu la kutupa vichafuzi dumufu vya kikaboni;

(g) kukuza utendaji ufaao katika usimamizi wa viuavisumbufu na kemikali;

(h) kuandaa mfumo imara wa data kwa ajili ya ufahamu bora wa matatizo yahusianayo na na vichafuzi dumufu vya kikaboni;

(i) kuratibu uingizaji ndani na utoaji nje ya nchi wa vichafuzi dumufu vya kikaboni;

(j) kuelekeza ufungaji mzuri kuwa ni sharti la msingi ili kuepuka uvujaji na uchafuzi wa mazingira wakati wa usafirishaji na utunzaji;

(k) usafirishaji salama wa taka za sumu au kemikali hatari, kemikali ambazo muda wake wa matumizi umekwisha au kemikali za aina hiyo, ikiwa ni njia ya kulinda mazingira na afya ya binadamu;

(l) kutimiza makubaliano ya kimataifa kuhusu usafirishaji ulioratibiwa vizuri wa maunzi ya hatari;

(m) kubuni njia bora zaidi za kuimarisha uwezo na fursa za kitaifa, usimamizi wa kemikali ikiwa ni pamoja na uhawilishaji wa teknolojia, utoaji misaada ya kifedha na kiufundi na ukuzaji ushirikiano na serikali zingine;

(n) kuratibu uingizaji na matumizi ya kemikali ambazo matumizi yake yamezuiliwa, au kibali chake kimekataliwa au kimefutwa chini ya sheria yoyote iliyopo iliyotungwa na Bunge kwa ili kulinda afya ya binadamu au mazingira;

(o) kutaja viuavisumbufu vyenye madhara makubwa, kuwa kemikali zilizozuiliwa Tanzania;

(p)masuala ya usalama wa mazingira yahusuyo mabomba ya gesi miminika, na usafirishaji wa maunzi yaliyotajwa kuwa ni hatari;

(q) fidia, usafishaji, na mwitiko wa dharura kwa dutu hatari zilizoachiwa kwenye mazingira na usafishaji wa maeneo yasiyotumika ambamo taka hatari zimetupwa;

(r) mipango ya dharura ya kitaifa, jiji, manispaa, mji na kijiji pindi ikitokea dutu hatari zimeachiwa kwenye mazingira;

(s) mahitaji ya upangaji mipango ya dharura, ilani, utoaji taarifa na

mafunzo; na

(t) mipango ya dharura zitokeapo ajali kubwa viwandani, udhibiti wa moto hatari, milipuko na utoaji sumu hatari.

**Taratibu za awali za kibali kwa ajili ya baadhi ya kemikali hatari na viua visumbufu.**

78 (1) Waziri,kuhusiana na usimamizi wa kemikali zinazolazimu Taarifa ya Awali ya Kibali (TAAKI), anaweza kuteua asasi itakayokuwa na jukumu la:

(a) kupendekeza nyongeza ya kemikali za TAAKI zenye maslahi kwa Tanzania;

(b) kuchukua hatua mwafakai kisheria na kiutawala kuzuia au kupunguza athari mbaya za kemikali za TAAKI kwa afya ya binadamu, maisha na mazingira;

(c) kufanya utafiti wa kemikali za TAAKI mbadala;

(d) kujumuisha taratibu za uingizaji ndani na utoaji nje ya nchi kemikali za TAAKI;

(e) kukuza utambuzi kuhusu kemikali zinazolazimu TAAKI na madhara yake kwa afya ya binadamu, maisha na mazingira;

(f) kufanya tathmini ya hatari ya kemikali za TAAKI na kujenga uwezo wa usimamizi wa hatari hizo;

(g) kufanya shughuli zingine zozote kwa mujibu wa masharti ya Mkataba wa Rotterdam katika maeneo yake ya mamlaka kijiografia;

(h) kuwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mkataba wa Rotterdam wa mwaka 1998, katika maeneo yake ya mamlaka kijiografia.

(2) Waziri, kwa kushauriana na Wizara zenye dhamana ya kilimo na afya, atatunga kanuni na miongozo kuhusu kuingiza ndani na kutoa nje ya nchi, kusafirisha na kutupa mabaki ya kemikali za TAAKI zisizohitajika na takataka zake.

**Ukuzaji wa uzalishaji bora na matumizi endelevu ya bidhaa na huduma.**

79 (1) Waziri, kwa kushirikiana na wakala wengine, atakuza teknolojia na mbinu za uzalishaji bora na matumizi endelevu ya bidhaa na huduma.

(2) Waziri anaweza kutoa miongozo inayohusu:

(a) kijitabu kuhusu teknolojia na mbinu za uzalishaji bora na matumizi endelevu ili kuongoza shughuli zinazohusiana na viwanda, utalii, biashara, madini, kilimo na huduma;

(b) kufuatilia athari za uzalishaji bora;

(c) kujumuisha uzalishaji bora kwenye taratibu za fedha na asasi za fedha ili kufanikisha njia endelevu za kugharamia uzalishaji bora;

(d) kujumuisha uzalishaji bora na kuweka taratibu za matumizi endelevu kwenye sera husika kwenye ngazi za Serikali na

kampuni.

*(d) Nyenzo za Kiuchumi*

**Motisha na nyenzo za kiuchumi kwa ajili ya kulinda mazingira.**

80 (1) Kwa madhumuni ya kupunguza uharibifu wa mazingira, Mkurugenzi wa Mazingira kwa nyakati mbalimbali ataandaa mapendekezo ya nyenzo za kiuchumi na vivutio vya kifedha na kuviwasilisha kwa Waziri.

(2) Waziri, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya fedha, anaweza kutunga kanuni na taratibu za nyenzo za kiuchumi kwa kuagiza-

(a) namna bora ya kuhakikisha kuwa watu binafsi au vikundi wanapofanya uamuzi kuhusu uzalishaji, matumizi na uwekezaji, wazingatia matokeo yake kwa mazingira;

(b) hatua za kuchukua ili kujumuisha gharama za mazingira bila kutegemea taratibu za uwekaji wa bei;

(c) hatua zenye misingi ya bei, tozo ya utumiaji na ruzuku ili kujumuisha gharama na manufaa yatokanayo na mazingira;

(d) ruzuku, makato na punguzo la kodi litakalolipwa kwa ajili ya kuendeleza utunzaji mazingira;

(e) misaada maalumu ya fedha kwa ajili ya programu na miradi maalumu, ikiwemo miradi ya mazingira;

(f) kuhamasisha urejeshwaji chupa, plastiki na vyuma kwa ajili ya urejelezaji na utupaji taka unaokubalika; na

(g) hatua nyingine yoyote inayoweza kuamriwa na Waziri ili itekelezwe na nyenzo za kiuchumi.

(3) Waziri, kwa kibali cha Waziri mwenye dhamana ya fedha, anaweza pia kuagiza vivutio na hatua za kifedha zifuatazo kwa ajili ya kutunza mazingira-

(a) tozo la maji machafu kutoka viwandani, kwa misingi ya ujazo na kiasi cha umwagaji kwenye hewa, maji, au mfumo wa maji taka;
(b) ada ya tozo la utumiaji kwa kutumia rasilimali asilia hiyo na kwa watu wengine wanaopatiwa huduma kama vile ya kukusanyiwa takataka;
(c) tozo la uzalishaji, kama vile tozo la bidhaa za makasha ya plastiki na chupa, tozo linalokwaza utupaji au kuhamasisha urejelezaji taka; na
(d) kodi ya mauzo na ushuru vinavyotoa nafuu ya bei kwa bidhaa zinazoafiki mazingira, dhidi ya bidhaa zinazochafua mazingira.

(4) “Nyenzo ya Kiuchumi” kama ilivyotumika kwenye Sheria hii maana

yake ni nyenzo ya usimamizi wa mazingira na maliasili iliyokusudiwa kushawishi mwenendo wa mawakala wa kiuchumi ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za viumbe hai na mazingira yake, na inajumuisha nyenzo za kifedha, mfumo wa tozo, haki za mali, uanzishaji wa masoko, mikataba ya utekelezaji na mifumo ya kurejeshwa amana, mifumo ya madeni, utoaji nyenzo za taarifa na fedha.

## SEHEMU YA VI
## TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA NA TATHMINI NYINGINEZO

**Wajibu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.**

81 (1) Mtu yeyote, awe mpendekejazi au mwenye mradi au shughuli ya aina yoyote iliyobainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria hii, ambapo Tathmini ya Athari kwa Mazingira inatakiwa kufanywa kwa sheria inayosimamia mradi au shughuli hiyo au kama haipo sheria hiyo, kwa kanuni zilizotengenezwa na Waziri, atafanya au kuhakikisha tathmini ya athari kwa mazingira ya shughuli au mradi huo inafanyika kwa gharama yake mwenyewe.

(2) Tathmini ya Athari kwa Mazingira itafanyika kabla ya kugharamia au kuanza kwa mradi au shughuli husika.

(3) Kibali au leseni ya kufanya mradi au shughuli yoyote kwa mujibu wa sheria yoyote iliyoandikwa haitampa mpendekezaji au mwenye mradi haki ya kufanya au kusababisha kufanyika mradi au shughuli bila hati ya tathmnini ya athari kwa mazingira iliyotolewa chini ya Sheria hii.

(4) Mtu yeyote atakayekiuka kifungu cha (3), atatenda kosa.

**Kanuni na Miongozo ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.**

82 (1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha (2), Waziri atatengeneza kanuni na miongozo ya namna ya kufanya tathmini ya athari kwa mazingira chini ya Sheria hii na sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge.

(2) Pale sheria nyingine inapoelekeza Tathmini ya Athari kwa Mazingira ifanyike kuhusu mradi au shughuli yoyote na namna ambavyo Tathmini ya Athari kwa Mazingira inapaswa kufanywa, haitakuwa lazima kutumia viwango vilivyowekwa kwa kanuni zilizowekwa chini ya Sheria hii isipokuwa tu pale ambapo kiwango kilichowekwa na sheria hiyo hakikidhi viwango vya chini ambavyo ni muhimu kwa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira ya aina hiyo.

**Wataalamu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira**

83 (1) Bila ya kujali masharti ya kifungu cha (2) cha fungu la 82, Tathmini ya Athari kwa Mazingira itafanywa na wataalamu au vikundi vya wataalamu ambao majina na sifa zao zitakuwa zimesajiliwa na Baraza.

(2) Waziri ataainisha kwenye kanuni, sifa za mtu anayeweza kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

(3) Baraza litatunza daftari lenye orodha ya wataalamu na vikundi vya wataalamu walioidhinishwa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

(4) Daftari la orodha ya wataalamu na vikundi vya wataalamu litawekwa kwenye masjala ya wazi na litaweza kupekuliwa na umma baada ya kulipa ada iliyowekwa.

(5) Mpendekezaji au mwenye mradi atachagua wataalamu kati ya watu wenye sifa zilizoainishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha (2), kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

**Kutolewa Hati si kinga dhidi ya mashtaka ya kisheria**

84 (1) Kutolewa kwa Hati ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa mradi wowote, hakutakuwa kinga dhidi ya mashtaka yoyote kisheria yatakayofanywa dhidi ya mpendekezaji wa mradi au shughuli kuhusu namna ambavyo mradi au shughuli inatekelezwa, kusimamiwa au kuendeshwa.

(2) Hati ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira inaweza kuhamishwa kutoka mmiliki mmoja kwenda kwa mwingine endapo tu miliki ya mradi itabadilika na si vinginevyo, na kwa sharti kwamba taarifa ya kusudio la kufanya uhamisho huo iwe imetolewa kwa Waziri kwa maandishi ndani ya siku thelathini kabla ya uhamisho.

**Kubaini mawanda ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira**

85 (1) Pale ambapo inatakiwa kutolewa Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira, Baraza litaamua mawanda ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira, kwa kukubaliana na mpendekezaji yanayohusu-

(a) hoja zilizoagizwa ambazo zinapaswa kushughulikiwa katika Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira;

(b) watu na asasi zinazopaswa kutoa maoni wakati wa maandalizi ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira;

(c) mbinu na njia za kukusanya, kulinganisha na kuchambua data zinazotakiwa; na

(d) suala lingine lolote linalochangia kubaninisha mawanda ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

(2) Taarifa za Tathmini ya Athari kwa Mazingira zitawekwa na kutunzwa na Baraza kwenye masjala ya wazi na zinaweza kupekuliwa baada ya kulipa ada iliyowekwa.

**Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.**

86 (1) Baraza, baada ya kupitia muhtasari wa mradi, litamtaka mpendekezaji wa mradi au shughuli afanye Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kuandaa Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

(2) Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira iliyotayarishwa chini ya kifungu cha (1) itawasilishwa kwa Baraza kwa mapitio.

(3) Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira itatayarishwa kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa na Waziri.

**Mapitio ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.**

87 (1) Baraza litafanya mapitio ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira katika muda wa siku sitini baada ya kuwasilishwa.

(2) Baraza, kwa madhumuni ya kufanya mapitio chini ya kifungu cha (1), linaweza kuunda kamati mtambuko ya kiufundi ili kupata ushauri kuhusu mapitio ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

(3) Mpendekezaji atatii agizo la kuleta taarifa ya ziada ambayo ni muhimu katika kuliwezesha Baraza kukamilisha mapitio na atafanya hivyo ndani ya muda ulioelekezwa katika agizo.

(4) Taarifa zinazotakiwa na Baraza kwa malengo ya kufanya mapitio ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira zinaweza kujumuisha, pamoja na mambo mengine, ramani na michoro ya usanifu, nyaraka za mradi, taarifa au vitu mbalimbali, maelezo ya kitaalamu, ushauri wa kisekta na masuala mengineyo yanayoweza kufikiriwa kuwa muhimu.

**Kutembelea eneo kwa nia ya kufanya uhakiki unaohusu mapitio ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.**

88 (1) Baraza, wakati wa mchakato wa mapitio, linaweza kutembelea kwa madhumuni ya ukaguzi au uhakiki wa eneo au jambo lolote linalohusishwa na mradi au shughuli iliyopendekezwa kwa gharama ya mwenye mradi.

(2) Mchakato wa mapitio ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira utazingatia vigezo vifuatavyo:

(a) uwiano kati ya manufaa ya muda mfupi na mrefu ya mradi kijamii na kiuchumi, na madhara kwa binadamu na mazingira;

(b) aina ya mradi au shughuli na namna inavyoweza kufikia viwango vya mazingira;

(c) njia mbadala zinazoweza kupunguza athari au hatua nyingine za kurekebisha mazingira yaliyoharibika;

(d) maoni yaliyopokelewa wakati wa mikutano ya hadhara na michakato mingine ya kushauriana chini ya Sehemu hii; na

(e) vigezo vingine vyovyote kama vilivyoelezwa kwenye Kanuni.

**Ushirikishwaji wa umma katika Tathmini ya Athari kwa Mazingira**

89 (1) Bila kuathiri Sehemu ya XIV, Baraza litaridhia na kutumia miongozo inayohusu ushirikishwaji umma, hasa ile inayoweza kusaidia katika mradi unaofanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

(2) Bila kuathiri kifungu cha (1), baada ya kupokea Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira, Baraza-

(a) litaisambaza ili kupata maoni ya kimaandishi kutoka asasi na wakala mbalimbali wa serikali;

(b) litautaarifu umma, kwa njia zinazofaa,kuhusu mahali na muda wa kufanya mapitio ya Taarifa ya Athari kwa Mazingira na kuwasilisha maoni kimaandishi kwa namna ilivyoelekezwa; na

(c) litatafuta maoni ya mdomo au ya maandishi kwa njia yoyote inayofaa, kutoka kwa watu watakaoathiriwa na mradi.

**Mkutano wa kutoa taarifa kwa umma na kupata maoni ya umma**

90 (1) Bila kujali masharti ya fungu la 87 la Sheria hii na masharti mengine ya Sheria hii, mapitio ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira yatafanywa, pamoja na mambo mengine, kupitia mikutano ya hadhara.

(2) Baraza, ndani ya siku sitini baada ya kupokea Taaarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira, litaamua ama kuitisha au kutoitisha mkutano wa hadhara kwa lengo la kupata maoni ya umma kuhusu mradi au shughuli iliyopendekezwa.

(3) Pale Baraza litakapoamua au kuombwa kuitisha mkutano wa hadhara, litaonyesha na kuwezesha kupatikana, kwa ajili ya ukaguzi na kunukuu, taarifa zozote husika, nyaraka na mawasilisho yaliyofanywa kwa maandishi wakati na baada ya kipindi cha mapitio hadi kipindi cha kupata maoni ya umma kitakapokwisha.

**Mapendekezo ya Baraza kuhusu Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira**

91 Baada ya kukamilisha mapitio ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira, Baraza litawasilisha mapendekezo kwa Waziri.

**Waziri kukubali au kukataa Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira**

92 (1) Waziri, ndani ya siku sitini, baada ya kupokea mapendekezo ya Baraza anaweza-

(a) kukubali Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kutoa Hati ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; au

(b) kukataa Taaarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; au

(c) kukubali Taaarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa masharti anayoweza kuamua kuyaweka, na kutoa Hati ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

(2) Endapo Waziri atakataa Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira-

(a) atamtaarifu mpendekezaji kwa maandishi sababu za kukataa; au

(b) atapendekeza kwa mamlaka inayotoa leseni kwamba shughuli hiyo isiruhusiwe.

**Kufuta leseni iwapo Tathmini ya Athari kwa Mazingira itakataliwa**

93 Waziri atakataa na kupendekeza kwa mamlaka inayotoa leseni kwamba mradi usiruhusiwe au, pale leseni inapokuwa imetolewa, kuifuta iwapo-

(a) mradi au shughuli inaweza kusababisha athari mbaya na bayana kwa mazingira;

(b) hakuna mbadala wa kupunguza au kurekebisha uwezekano wa uharibifu bayana kwa mazingira;

(c) mpendekezaji ameshindwa kuzingatia hatua za kupunguza athari zilizoelezwa kwenye Taaarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira au masharti yaliyotolewa na Waziri; au

(d) kuna sababu za lazima za kijamii, kiuchumi, kiafya, kiutamaduni, au kidini ambazo zinaweza au zinaelekea kusababisha athari zisizorekebishika kwa jamii.

| | | |
|---|---|---|
| **Kukasimu madaraka ya kuidhinisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira** | 94 | Waziri anaweza, kwa hati iliyotangazwa katika *Gazeti la Serikali,* kukasimu madaraka yake ya kuidhinisha Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwenda kwa Mkurugenzi wa Mazingira, mamlaka za serikali za mitaa au Wizara za kisekta. |
| **Rufaa dhidi ya uamuzi wa Waziri kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira** | 95 | Mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Waziri wa kukubali au kukataa Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira anaweza kukata rufaa kwenye Baraza la Rufaa la Mazingira. |
| **Utunzaji wa kumbukumbu za maamuzi kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira** | 96 | (1) Mkurugenzi Mkuu atatunza kumbukumbu ya maamuzi yanayohusu vibali na kukataliwa Taarifa ya Athari kwa Mazingira.<br><br>(2) Kumbukumbu iliyoelezwa chini ya kifungu cha (1) itawekwa kwenye masjala ya wazi na itapatikana kwa umma baada ya kulipa ada iliyobainishwa. |
| **Kutakiwa kufanyika upya Tathmini ya Athari kwa Mazingira** | 97 | Baraza linaweza, wakati wowote baada ya kutolewa kwa hati ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira, kumtaka mwenye hati hiyo kufanya upya tathmini ya athari kwa mazingira kwa gharama yake mwenyewe kisha kuwasilisha maelezo yake kwenye Baraza ndani ya muda ambao Baraza litaelekeza iwapo;<br>(a) kumetokea mabadiliko au marekebisho makubwa wakati wa utekelezaji wa mradi au shughuli tofauti na ilivyokuwa awali;<br><br>(b) mradi au shughuli husika inatishia kuwapo kwa uharibifu wa mazingira ambao haukuweza kugundulika awali wakati wa uchambuzi au mapitio; au<br><br>(c) wakati wowote iwapo itagundulika kwamba taarifa au data iliyotolewa na mtekelezaji wa mchakato wa awali wa tathmini ya Athari kwa Mazingira hazikuwa sahihi, zilikuwa za uongo au zilikusudia kulipotosha Baraza. |
| **Kosa la kukiuka Tathmini ya Athari kwa Mazingira** | 98 | Mtu yeyote ambaye atashindwa au kupuuza kuzingatia maagizo ya Baraza yatakayotolewa chini ya fungu la 97, atakuwa anatenda kosa. |
| **Upelembaji wa hali ya mazingira** | 99 | (i) Baraza, kwa kushirikiana na Wizara au wakala wa Serikali litafuatilia:-<br>a) vigezo na viashiria vyote vya mazingira kwa lengo la kufanya tathmini ya mabadiliko yoyote yanayoweza kutokea kwenye mazingira pamoja na |

athari zake; na

b) Utekelezaji wa mradi au shughuli yoyote kwa lengo la kubaini athari zake za muda mfupi na mrefu kwa mazingira.

(2) Baada ya kutoa notisi mkaguzi wa mazingira au ofisa yeyote aliyeidhinishwa, anaweza kuingia sehemu yoyote kwa madhumuni ya kukagua athari kwa mazingira zinazotokana na shughuli zinazofanyika kwenye eneo husika.

**Upelembaji wa uzingatiaji wa maelekezo ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.**

100 (1) Pale ambapo matokeo ya upelembaji yataonyesha kutokuzingatiwa kwa maelekezo ya Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira, mwenye Hati ya Tathimini ya Athari kwa Mazingira anaweza kutakiwa:-

(a) kuchukua kila hadhari katika kuzuia athari inayotokana na kutokuzingatia maelekezo yaliyo katika Taarifa na kutoa taarifa kwa Baraza kuhusu hatua alizochukua; au

(b) kulipa faini iliyowekwa na Baraza kwa taratibu za kiusimamizi kwa kukiuka utekelezaji wa maelekezo yaliyo katika Taarifa.

(2) Baraza linaweza kupendekeza kwa Waziri kufutwa kwa hati ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira iliyotolewa iwapo matokeo ya upelembaji wa ziada yataonyesha ukiukwaji wa mara kwa mara wa uzingatiaji wa masharti yaliyotajwa katika Hati ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na pia Baraza linaweza kuchukua hatua za kisheria mahakamani dhidi ya uharibifu au madhara yoyote ambayo yanaweza kuwa yamesababishwa na kuendelea kutozingatiwa kwa masharti yaliyo kwenye Hati

**Uhakiki wa Mazingira.**

101 (1) Baraza litakuwa na wajibu wa kuhakiki mazingira kwenye mradi au shughuli yoyote yenye mwelekeo wa kusababisha athari kubwa kwa mazingira.

(2) Mkaguzi wa mazingira au ofisa mwingine yeyote aliyeidhinishwa, baada ya kutoa notisi anaweza kuingia kwenye ardhi au jengo lolote kwa madhumuni ya kutambua jinsi gani shughuli zinazofanyika kwenye ardhi au jengo hilo zinawiana na taarifa zilizo katika Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

(3) Bila kujali masharti ya vifungu vya (1) na (2), mpendekezaji au mwenye mradi au shughuli ambayo imetolewa Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira atatakiwa kuweka kumbukumbu sahihi na kupeleka kwa Baraza taarifa za mwaka zikieleza ni jinsi gani mradi katika utekelezaji wake unazingatia maelekezo yaliyomo kwenye Taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

(4) Mpendekezaji au mwenye mradi wa mradi au shughuli atachukua hatua zinazofaa kupunguza athari zozote ambazo awali hazikutarajiwa katika Taarifa yaTathmini ya Athari kwa Mazingira, na ataandaa taarifa yenye maelezo ya kina kuhusu hatua hizo ambayo ataiwasilisha kwenye Baraza kila mwaka au kadiri Baraza

litakavyoelekeza.

**Urejeshaji wa mazingira ya eneo la mradi au shughuli baada ya mradi au shughuli kufungwa**

102 (1)Baada ya muda wa mradi au shughuli zilizotajwa kwenye Jedwali la Tatu lililopo kwenye Sheria hii kuisha, mpendekezaji au mwenye mradi, kwa gharama zake atasawazisha na kurejesha mazingira katika hali yake ya awali, ikiwa ni pamoja na uondoshaji wa vifaa na, ukarabati wa eneo na urejeshaji wa mfumo wa ikolojia katika hali yake ya awali kabla ya kufunga mradi au shughuli.

(2) Mkurugenzi wa Mazingira hatarejesha amana ya utendaji kuhusu mazingira iliyowekwa chini ya fungu la 227 la Sheria hii mpaka pale mwenye amana hiyo atakapotimiza masharti yaliyotajwa chini ya kifungu cha (1).

**Tathmini nyinginezo.**

103 Bila kujali masharti ya awali katika sehemu hii, Waziri anaweza kumtaka mtu yeyote ambaye shughuli zake zinaonekana kuwa na uwezekano mkubwa wa kuleta athari kwa mazingira kutoa maelezo juu ya athari iliyopo kwa jamii, afya, bioteknolojia, au athari nyingine kwa mazingira ambazo anaweza kuziona.

## SEHEMU YA VII

## TATHMINI YA MAZINGIRA KIMKAKATI

**Tathmini ya Mazingira kimkakati kuhusu Miswada, kanuni, sera, mikakati, programu na mipango**

104 (1) Wakati wa kuandaa Muswada wa Sheria yoyote ambayo inaashiria kugusa suala la:-

(a) usimamizi, hifadhi na uboreshaji wa mazingira, au

(b) usimamiaji endelevu wa maliasili, italazimu kuandaa na kuwasilisha kwa Waziri maelezo ya kina kuhusu Tathmini ya Mazingira Kimkakati ya athari kwa Mazingira zinazoweza kusababishwa na utekelezaji wa sheria hiyo.

(2) Bila ya kuathiri kifungu cha (1) wakati wa kuandaa Kanuni, Sera za Umma, programu na mipango ya maendeleo itatakiwa kuandaliwa kwa taarifa ya tathmini ya mazingira kimkakati juu ya athari kwa mazingira ambazo zinaweza kusababishwa na Kanuni, Sera za Umma, Programu au Mipango ya maendeleo.

(3) Kila Taarifa ya Tathmini ya Mazingira kimkakati inayotolewa chini ya fungu hili litajumuisha;

(a) maelezo kamili ya Sera, Muswada, Sheria, Mkakati, Programu, mpango na malengo yanayokusudiwa kufikiwa;

(b) uchambuzi, maelezo na tathmini ya matokeo mazuri au mabaya ambayo utekelezaji wa Sera, Miswada, mikakati, programu, mpango au Sheria hizo unaweza kusababisha kwenye mazingira na kwenye

usimamizi wa maliasili.

(c) utambuzi, maelezo na tathmini ya athari za matokeo tarajiwa ya njia mbadala za kuyafikia malengo ya sera, Muswada, sheria, mkakati, programu na mpango;

(d) utambuzi, maelezo na tathmini ya uzito wa hatua madhubuti ambazo zitaweza kuchukuliwa kuepuka, kupunguza au kurekebisha athari yoyote mbaya inayoweza kutokea kutokana na utekelezaji wa sera, Muswada, sheria, mkakati, programu au mpango; na

(e) Taarifa nyingine yoyote ambayo Waziri anaweza kubainisha kwa kanuni.

(4) Pale ambapo mtu mwenye dhamana ya Muswada, Kanuni, Sera ya Umma, Mkakati, Programu au mpango hatahitaji Tathimini ya Mazingira ya Kimkakati chini ya fungu hili, atawasilisha rasimu ya Waraka husika kwa Waziri ambaye naye ataamua kwa haraka kadiri itakavyowezekana kama tathmini inahitajika ama la, na atatoa uamuzi wake pamoja na sababu.

(5) Baada ya kupokea taarifa ya tathmini ya mazingira kimkakati, Waziri atamuagiza Mkurugenzi wa Mazingira kuiangalia upya sera, Muswada, sheria, mkakati programu au Mpango na kuwasilisha maoni yake kwa Waziri ambaye naye atatoa maoni yake kwa mtu anayehusika;

(6) Mtu aliyepewa maoni na Waziri atatakiwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa, na pia atatakiwa kuwasilisha kwake taarifa mpya yenye kuonyesha;

(a) mapitio yaliyofanyika kwenye Waraka husika ili kuendeleza usimamizi wa Mazingira na usimamizi endelevu wa maliasili, au kuepuka, kupunguza au kurekebisha athari ambazo zingetokea kutokana na utekelezaji wa Sheria, Sera, Programu au mpango wa awali;

(b) hatua zingine zozote zinazotakiwa kuchukuliwa ili kuepuka kupunguza au kurekebisha athari mbaya kwa mazingira na ni lini hatua hizo zilichukuliwa au zitachukuliwa, na iwapo hatua zozote zilizopendekezwa kwenye taarifa ya tathmini zimechukuliwa au hazitachukuliwa, sababu za kutokufanya hivyo; na

(c) Waraka uliorekebishwa wa sera, Muswada, sheria, mkakati programu na mpango.

(7) Iwapo Waziri ana maoni kwamba masuala ya mazingira yaliyotolewa

wakati wa mchakato wa Tathmini ya Mazingira kimkakati hayajashughulikiwa ipasavyo katika Muswada, kanuni, sera, mkakati, programu au mpango uliorekebishwa na kwamba hatua zaidi kwa kuzingatia gharama zinahitaji kuchukuliwa ili kuepuka au kupunguza makali ya athari hizo, ataweka pingamizi ndani ya siku thelathini baada ya kupokea nyaraka zilizotajwa chini ya kifungu cha (5) kwa mtu husika kwa nia ya kufikia muafaka juu ya mabadiliko yanayotakiwa kufanywa kwenye sera, Muswada, sheria, mkakati, programu au mpango uliorekebishwa ili kuyapa nguvu madhumuni na misingi ya Sheria hii.

(8) Pale ambapo Waziri ameagiza na Mkurugenzi wa Mazingira na mtu anayehusika wakashindwa kufikia muafaka juu ya mabadiliko yanayotakiwa yafanyike kwenye sera, Muswada, sheria, mkakati, program au Mpango uliorekebishwa kuhusu hatua ambazo zinapaswa kuchukuliwa, Mkurugenzi au mtu husika watatoa notisi ya kuweka pingamizi kwa Waziri.

(9) Waziri, baada ya kupokea notisi ya pingamizi, anaweza kuamuru kwamba ule waraka uliotajwa chini ya kifungu cha (6) upitiwe upya au ujadiliwe kwenye mkutano wa hadhara kabla hajautolea uamuzi wa mwisho.

**Tathmini ya mazingira kimkakati kwa ajili ya shughuli za madini, petroli, umeme wa nishati ya maji na mipango ya miradi mikubwa ya maji**

105 (1) Iwapo rasilimali ya madini au mafuta itagundulika kabla ya mpango wowote au kabla ya kuwa na mpango wa kujenga kituo cha nishati ya umeme wa maji au kabla mpango wa mradi kamambe wa maji haujafanyika, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya madini, nishati au maji atafanya tathmini ya mazingira kimkakati.

(2) Tathmini ya Mazingira Kimkakati iliyotajwa chini ya kifungu cha (1) itatathmini eneo lililotengwa kwa ajili ya shughuli husika pamoja na mambo yafuatayo:-

(a) hali halisi ya mazingira na ya maliasili;

(b) utambuzi wa maeneo nyeti kiikolojia na yanayolindwa ;

(c) utambuzi na maelezo kuhusu jamii zinazolizunguka eneo husika ;

(d) hali halisi ya kiuchumi jamii iliyopo;

(e) shughuli za kiuchumi na miundombinu iliyopo;

(f) maendeleo yanayopendekezwa ikiwa ni pamoja na malengo mbali mbali ya muda mrefu na maendeleo ya ujumla ya aina tofauti za machimbo ya madini au maeneo ya mafuta na gesi au vituo vya umeme wa nishati ya maji;

(g) miundombinu na rasilimali inayohitajika kuhudumia maendeleo haya.

(h) Uwezekano wa athari kwa mazingira na jamii kutokana na maendeleo ya uchimbaji madini au mafuta au nishati ya umeme wa

maji au mradi wowote mkubwa wa maji, na;

(i) Mapendekezo juu ya uongoji wa ardhi na vikwazo dhidi ya maendeleo kwenye maeneo tofauti.

(3) Waziri atamuagiza Mkurugenzi wa Mazingira kupitia tathmini ya mazingira kimkakati na kuandaa taarifa kuhusu utoshelevu au upungufu wa taarifa na maeneo yanayohitaji kuboreshwa na kisha atatoa mapendekezo kwa Waziri kwa kadiri inavyostahili.

(4) Mkurugenzi wa Mazingira atawasilisha kwa Waziri taarifa ya mapitio kwa madhumuni ya kupata idhini.

(5) Baada ya kupokea mapendekezo, Waziri ataidhinisha taarifa na kutoa mapendekezo kwa Wizara yenye dhamana ya masuala ya madini, nishati au maji kuhusu mbinu bora ya kuhifadhi mazingira ndani ya muktadha wa mradi unaotarajia kushughulikiwa.

(6) Wizara yenye dhamana ya masuala ya madini, nishati au maji itapaswa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na Waziri.

## SEHEMU YA VIII
## UZUIAJI NA UDHIBITI WA UCHAFUZI

**Uzuiaji wa uchafuzi kwa ujumla**

106 (1) Litakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuchafua au kuruhusu mtu mwingine yeyote kuchafua mazingira kwa kukiuka viwango vyovyote vilivyobainishwa chini ya Sheria hii au sheria nyingine zinazodhibiti uchafuzi wa sehemu yoyote ya mazingira.

(2) Katika kuamua kuhusu kutoa au kutokutoa leseni, kibali au idhini ya kumwaga uchafu, na kuhusu masharti ya leseni, kibali au idhini, Baraza au mtu mwingine yeyote aliyekasimiwa madaraka ya kutoa uamuzi atahakikisha kuwa njia iliyobainishwa kuwa ni bora itatumika.

(3) Kwa madhumuni ya fungu hili “njia iliyobainishwa kuwa ni bora” kwa kumwaga uchafu au kupiga kelele maana yake ni mbinu bora ya kuzuia au kupunguza athari mbaya kwa afya ya binadamu, viumbe hai na mazingira.

(4) Si ruhusa kwa mtu yeyote kutoa aina yoyote ya uchafu ambao utasababisha uchafuzi wa hewa, kinyume na viwango vilivyobainishwa au vitakavyobainishwa chini ya sheria hii.

(5) Si ruhusa kwa mtu yeyote kupiga kelele au kusababisha kupiga kelele kuzidi kiwango kilichoainishwa au kitakachobainishwa kuhusiana na upigaji kelele.

(6) Litakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kumwaga uchafu au kupiga kelele bila kuzingatia njia iliyobainishwa kuwa ni bora katika kanuni zinazoweza kutungwa na Waziri.

**Mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni za kuzuia na kudhibiti vichafuzi**

107 Waziri, kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana ya serikali za Mitaa anaweza kutengeneza kanuni zaidi za:-

(a) kuzuia na kudhibiti shughuli yoyote iliyoelezwa bayana yenye kusababisha athari mbaya kwa mazingira;

(b) kumtaka kila mtu kufuatilia utoaji wa uchafu na kuweka kumbukumbu za matokeo ya upelembaji huo;

(c) kuunda mifumo fungamanishi ya uzuiaji na uthibiti wa uchafu;

(d) kuweka mahitaji ya lazima na utaratibu wa kisheria kwa ajili ya watu wanaotoa leseni na vibali chini ya sheria hii au kanuni;

(e) kuweka masharti, viwango na miongozo ya kuzuia na kudhibiti utoaji wa taka kwenye mazingira na kwa ajili ya shughuli na uendeshaji wa vitu vinavyoweza kusababisha utoaji wa taka kwenye mazingira;

(f) kuwataka watu wanaotuma maombi ya leseni yanayohusu utoaji taka kulipia gharama za uendeshaji kuhusu maombi hayo ikiwa ni pamoja na gharama za misaada ya kitaalamu wakati wa kushughulikia maombi hayo;

(g) kubainisha umwagaji taka utoaji taka, utupaji taka, vyombo, vyanzo vya vichafuzi jongevu na tuli na mizigo hatari;

(h) kubainisha dutu yoyote mpya ya hatari, dutu zenye sumu au zenye uwezekano wa kuwa na sumu, dutu zenye madhara kwa mazingira na aina nyingine ya dutu zinazodhibitiwa;

(i) kuzuia, kukataza na kudhibiti kwa njia nyingine za leseni, miongozo, uingizaji wa bidhaa, usafirishaji wa bidhaa nchi za nje, utengenezaji, usafirishaji, ubebaji, uuzaji, umiliki, utumiaji, uhifadhi au utupaji wa aina yoyote ya dutu, zao au bidhaa yenye dutu inayodhibitiwa;

(j) kujumuisha kwenye kanuni za ndani ya nchi mwenendo wa sasa wa sheria na desturi za kimataifa za mazingira;

(k) kuhitaji upelembaji wa vichafuzi vya mazingira kwenye maeneo yanayozunguka taka zilizovuja;

(l) kuweka viwango vinavyohusu utengenezaji, usambazaji, uuzaji au kutangaza uuzaji wa mazao au bidhaa ambazo utengenezaji, utumiaji au utupaji wake ungeweza au unaweza kusababisha utoaji wa uchafu kwenye mazingira;

(m) kuhusu magari;

(i) kuhitaji, kudhibiti na kuzuia ufungaji, ukarabati na utumiaji wa vifaa na zana;

(ii) kuanzisha viwango vya kisheria vya utoaji taka na programu za majaribio;

(iii) kukataza utumiaji wa gari lolote ambalo litashindwa kuzingatia viwango vya utoaji wa moshi; na

(iv) kuzuia au kudhibiti matumizi ya magari kwenye maeneo fulani ya barabara yaliyochaguliwa au kwenye sehemu fulani za maeneo ya miji.

(n) kutaka, kudhibiti na kuzuia utumiaji wa matangazo, alama na vitambulisho kwenye bidhaa, makasha na makontena;

(o) kukataza au kudhibiti kwenye maeneo fulani, kwa siku fulani za mwaka au vyote kwa pamoja utekelezaji na jinsi ya kutekeleza shughuli ambazo zinaweza kusababisha utoaji wa uchafu; na

(p) kumtaka mtu yeyote kutoa taarifa inayohusu udhibiti au uzuiaji wa utoaji wa uchafu au upigaji wa kelele.

**Uzuiaji na udhibiti fungamanishi wa uchafuzi**

108 Ili kufikia lengo la uzuiaji na udhibiti fungamanishi wa uchafuzi, Baraza linaweza kubainisha miongozo inayofaa kuhusu mbinu bora zaidi za kuzuia au kupunguza athari kwa mazingira, likitilia maanani masuala kama vile:

(a) aina ya uchafu unaomwagwa au unaotolewa pamoja na unyeti wa mazingira yatakayopokea uchafu kwa madhara makubwa yanayoweza kutokea;
(b) gharama kifedha na matokeo kwa mazingira vitakavyoletwa na chaguo moja ukilinganisha na lingine; na
(c) hali ya sasa kiteknolojia na uwezekano kwamba chaguo linaweza kutumika kwa mafanikio.

**Kuzuia uchafuzi wa Maji**

109 (1) Mtu yeyote ambaye atakuwa anajua ataweka au kuruhusu kuwekwa kuanguka au kubebwa hadi ndani ya kijito chochote ikiwa aidha ni kit kimoja ama kwa kujumuisha na vitendo vingine vinavyolingana na h ambapo atakuwa ameingilia mtiririko wa maji ya mto huo au kuchafua yake, au kuweka taka ngumu za kiwanda chochote au mchakato utengenezaji viwanda au atatupa takataka au uchafu wowote au uozo wa chochote kigumu ndani ya kijito hicho, atakuwa ametenda kosa;

(2) Mtu yeyote ambaye atasababisha kuanguka au kutiririka au kuchukuliwa ndani ya mto wowote kichafuzi kimimika, harufu mbaya au uchafuzi unaotoka kwenye kiwanda chochote au mchakato wa usindikaji atakuwa ametenda kosa.

**Kuzuia umwagaji wa dutu hatari, kemikali mafuta, n.k.**

110 (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumwaga dutu hatari, kemikali, mafuta au mchanganyiko wenye mafuta kwenye eneo lolote la maji au sehemu yoyote ya mazingira isipokuwa kwa mujibu wa miongozo iliyowekwa chini ya Sheria hii, au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge.

(2) Mtu yeyote atakayetupa dutu ya hatari, mafuta au mchanganyiko wa mafuta kwenye maji au sehemu yoyote ya mazingira, atakuwa ametenda kosa.
(3) Mbali na adhabu ya jumla inayotolewa kwa mujibu wa chini ya

mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa chini ya fungu hili anaweza kuamrishwa na Mahakama:

(a) kulipa gharama za kuondosha takataka pamoja na gharama zozote ambazo Serikali au Wakala wa Serikali wamegharamia katika urejeshwaji wa hali ya mazingira yaliyoharibika kutokana na umwagaji; na

(b) kulipa gharama za walioathiriwa, umwagaji, ukarabati, urejeshaji katika hali ya awali au fidia kama itakavyoamriwa na mahakama.

(4) Itakuwa wajibu wa kila shirika na mtu binafsi anayezalisha, anayesafirisha, anayefanya biashara, anayetuimia, au anayehifadhi au kuondoa kemikali, mafuta vitu vyenye sumu, dutu zinazoshika moto ili kuzingatia kanuni zilizobainishwa na Waziri kuhusu usalama wa watu na viumbe hai na pia kuepuka kusababisha uharibifu wa mazingira.

(5) Bila kuathiri sheria nyingine yoyote iliyopo, Waziri kwa kushauriana na mamlaka husika anaweza kuweka katika kanuni orodha ya dutu zenye sumu zinazoshika moto na zinazolipuka ambazo zinazuiwa chini ya Sheria hii.

(6) Kwa madhumuni ya kudhibiti uzalishaji, utunzaji, au usafirishaji wa dutu za sumu, zinazoshika moto au kulipuka ambazo chini ya kifungu cha (5) zimezuiwa, Waziri anaweza kuwataka wamiliki au waendeshaji wa uzalishaji au wasafirishaji kupunguza athari za shughuli zao kwa mazingira kwa-

(a) kutoa notisi kuhusu umwagikaji;
(b) kuanza mara moja shughuli za kusafisha eneo kwa kutumia mbinu bora zilizopo za usafishaji;
(c) kutekeleza maagizo kama Baraza litakavyoelekeza.

(7) Baraza linaweza kukamata chombo cha uzalishaji, huduma ya kuhifadhi au usafirishajiau gari au chombo cha usafiri wa majini hadi pale mmiliki au muendeshaji atakapochukua hatua za kuzuia athari.

(8) Baraza litaomba amri ya Mahakama ili kuondosha huduma ya kuhifadhi au usafirishaji au gari au chombo cha usafiri wa majini na iwapo mmiliki au mwendeshaji huyo atashindwa kuchukua hatua za kuzuia athari ndani ya muda ulioamuliwa.

(9) Bila kuathiri sheria yoyote nyingine, Baraza litahakikisha kwamba:-

(a) mahali, mchoro, utengenezaji na uendeshaji wa mitambo inayotumia nishati ya atomiki;
(b) viwanda, uzalishaji, usafirishaji, utumiaji na utunzaji vinururishaji;
(c) utupaji wa taka zenye vitu nururishaji; na

asasi, watu binafsi wanaotumia mitambo, zana, nyenzo, mnururisho

wa sumaku umeme wenye madhara au mnururisho wa ioni, wanazingatia masharti ya sheria yoyote au kanuni zinazoweza kubainishwa kwa makusudi ya kulinda mazingira, upekuzi wa mara kwa mara na kwa ajili ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kuhusiana na vyombo na ripoti itakayowasilishwa kwenye Baraza kwa nyakati mbalimbali.

**Wajibu wa kuwa na taarifa za mabadiliko ya kiteknolojia**

111 (1) Itakuwa ni wajibu wa Baraza, kwa kushirikiana na chombo kingine chochote, kufuatilia kwa karibu maendeleo katika teknolojia na mbinu za kuzuia au kupunguza uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na utoaji wa dutu kutoka kwenye michakato iliyobainishwa.

(2) Mtu yeyote ambaye anafanya shughuli inayoathiri mazingira atatakiwa kufuata agizo linaloweza kutolewa na Baraza kuhusu kufanya marekebisho yanayotakiwa kufuatia maendeleo yoyote katika teknolojia na mbinu hizo za kuzuia au kupunguza uchafuzi wa mazingira.

**Wajibu wa kutoa taarifa ili kuzuia uchafuzi**

112 (1) Kwa madhumuni ya kurahisisha uzuiaji na udhibiti wa uchafuzi, Waziri anaweza kubainisha taratibu za kisheria zinazoshurutisha utoaji wa taarifa kwa Baraza au kwa mtu aliyeteuliwa kwa ajili hiyo kutoka kwa:

(a) mtu yeyote anayemiliki au kuendesha mradi wa umwagiliaji maji, mfumo wa maji taka, mtambo wa uzalishaji wa kiwandani, mtambo wa kusafisha taka zinazotoka viwandani, mahali pa kutupia taka ngumu, biashara na chombo cha kutunzia bidhaa za petroli, karakana au shughuli nyingine yoyote yenye kumwaga au iliyo na uwezekano mkubwa wa kumwaga vimiminika taka au vichafuzi vingine kwenye mazingira; au

(b) asasi au chombo kingine chochote kinachotakiwa na sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge, kuchukua hatua za kuzuia uchafuzi ndani ya maeneo ambayo inayadhibiti kiutawala au asasi nyingine yoyote au chombo chochote kitakachoweza kupewa jukumu hilo kwa nyakati mbalimbali.

**Sheria Na. 21 ya 2003**

(2) Masharti ya kifungu cha (1) hayatapunguza madaraka ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya meli kuhusu kutunga kanuni, kwa ajili ya kuzuia uchafuzi kwenye vyombo vya usafirishaji majini kwa mujibu wa masharti ya Sehemu ya XIX, ya Sheria ya Meli za Kibiashara ya Mwaka 2003.

(3) Mtu yeyote mwenye kukiuka matakwa ya kutoa taarifa kwa Baraza au kwa mtu yeyote aliyeteuliwa atakuwa ametenda kosa.

**Notisi ya kuzuia aina ya mchakato au shughuli zilizoagizwa.**

113 (1) Pale ambapo Baraza litakuwa na maoni kwamba uendeshaji wa shughuli au mchakato uliobainishwa au kuendelea kwa mchakato au shughuli yoyote kwa mtindo fulani unaohusisha kutokea kwa hatari kubwa ya uchafuzi wa mazingira, Baraza linaweza kumpelekea notisi ya kumzuia mtu anayeshughulika na mchakato au shughuli hiyo.

(2) Notisi ya kuzuia inayotolewa chini ya kifungu cha (1)-

(a) itaeleza hatari iliyopo kwa mazingira kutokana na shughuli au mchakato huo;

(b) itaeleza hatua zinazoweza kuchukuliwa pamoja na muda utakaotumika katika kuondosha hatari hiyo kwenye shughuli au mchakato huo;

(c) itaagiza kwamba, idhini ya kuendelea na mchakato au shughuli isimame hadi hapo sehemu ya matakwa au matakwa yote katika notisi yatakapokuwa yameondolewa.

(d) pale ambapo notisi inahusu sehemu tu ya mchakato au shughuli, itatoa masharti yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa kushughulikia mchakato au shughuli ambayo imeidhinishwa kutekelezwa.

## SEHEMU YA IX
## USIMAMIZI WA TAKA

### *(a) **Usimamizi wa Taka ngumu***

**Wajibu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kusimamia na kupunguza taka ngumu**

114 (1) Ili kuhakikisha kwamba taka ngumu zinapunguzwa kufikia kiwango cha chini katika maeneo yaliyo chini ya mamlaka yake, Serikali za Mitaa zitaagiza:-

(a) kwa aina tofauti za taka, takataka, mabaki au uchafu, zichambuliwe na kutenganishwa kwenye chanzo chake;

(b) kuweka viwango vya kuongoza aina, saizi, umbo, rangi na vipimo vingine kwa ajili ya jaa za taka zinavyotumika; na

(c) kuweka utaratibu kwa kushirikisha viwanda na sekta binafsi na Asasi Zisizo za Kiserikali katika kupanga, kukuza weledi miongoni mwa wazalishaji, wachuuzi, wasafirishaji, watengenezaji viwandani na watu wengine kwa nia ya kupata jaa zinazofaa kwa taka na utenganishaji wa taka kwenye chanzo.

(2) Mamlaka ya serikali za mitaa kwenye maeneo yake zitafanya mambo yafuatayo:-

(a) zitahakikisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira inayofaa inafanyika kwa ajili ya shughuli zote kuu mpya zinazolenga kwenye usimamizi unaostahili wa taka ngumu;

(b) zitasimamia taka ngumu zinazozalishwa kwa mujibu wa mipango endelevu iliyotolewa na serikali za mitaa husika; na

(c) zitahakikisha uchambuzi wa taka unaostahili unafanyika pale kwenye chanzo na unazingatia viwango au vipimo vilivyoagizwa na serikali husika ya mitaa.

(3) Kwa madhumuni ya kutoa uamuzi kuhusu ubora wa mbinu yoyote mahsusi ya ukusanyaji, ushughulikiaji wa upunguzaji wa madhara au utupaji wa taka ngumu, mamlaka ya serikali za mitaa itatafiti kwenye maeneo yake kwa lengo la kupata uelewa wa kiwango cha uzalishaji wa taka ngumu na muundo wake.

**Utupaji wa taka ngumu kutoka kwenye masoko, maeneo ya biashara na asasi**

115 (1) Kila mamlaka ya serikali za mitaa itapaswa kufanya utafiti kipindi hadi kipindi ili kujua aina ya taka ngumu zinazozalishwa kutoka kwenye masoko, maeneo ya biashara na asasi na itaamua njia zinazofaa kutumika wakati wa uchambuaji, utunzaji au utupaji wa taka.

(2) Katika kubaini njia inayofaa ya uhifadhi au utupaji wa taka ngumu zinazozalishwa toka kwenye vyanzo mbalimbali vya masoko, vituo au maeneo ya biashara na kwenye asasi zilizo chini ya mamlaka yake, mamlaka ya serikali za mitaa itahakikisha kwamba taka ngumu zinaainishwa na zinahifadhiwa inavyostahili kutegemea na aina yake, yaani zinazooza, plastiki, kioo au chuma.

(3) Waziri anaweza kuagiza ubainishaji wa makundi ya taka ngumu kitaifa ambayo mamlaka ya serikali za mitaa inaweza kuyakubali katika maeneo yake.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, “asasi” inajumuisha shule, ofisi, hospitali, polisi, kambi ya jeshi, majengo ya kidini, makambi, nyumba za watawa na ushirika au chombo chochote ambacho Waziri anaweza kukitangaza kuwa ni asasi kwa madhumuni ya usimamizi wa taka ngumu.

**Uhifadhi wa taka ngumu kutoka viwandani**

116 (1) Mamlaka ya serikali za mitaa zitahakikisha kwamba viwanda vilivyomo kwenye maeneo yake vimetenga eneo na vifaa vya kutosha kwa ajili ya usimamizi wa taka ngumu zinazozalishwa kutoka kwenye viwanda hivyo kabla ya taka kukusanywa ili kutupwa kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo.

(2) Mamlaka ya serikali za mitaa itahakikisha kwamba mashimo ya taka au maeneo yaliyotengwa mahsusi na viwanda kwa ajili ya kukusanyia taka ngumu yanawekwa katika hali ya usafi na yanalindwa dhidi ya nzi, wanyama na viumbe wanaokula mizoga.

(3) Waziri, baada ya kushauriana na Mawaziri wenye dhamana ya viwanda, ardhi, afya na mamlaka ya serikali za mitaa, atatoa amri kuhusu taka ngumu ambazo zitazingatiwa na viwanda mbalimbali.

**Ukusanyaji wa taka ngumu**

117 Mamlaka ya serikali za mitaa katika maeneo ya mijini na vijijini zitabainisha mambo yafuatayo-

**kwenye maeneo ya** mijini **na vijijini**

(a) njia bora zinazowezekana kwa ukusanyaji wa taka ngumu za aina mbalimbali kutoka vyanzo vya uzalishaji wa taka hizo, na itapanga njia za kupata fidia ya gharama za ukusanyaji wa taka ngumu, peke yake au kwa kushirikiana na sekta ya biashara na sekta binafsi; na

(b) zana zinazofaa, wakati na njia za kupita katika ukusanyaji wa taka ngumu.

**Vituo vya taka vya muda.**

118 (1) Mamlaka ya serikali za mitaa itatenga vituo vya kuweka taka kwa muda kama vituo vya kukusanyia taka ngumu kwenye majiji au manispaa, au miji au maeneo mengine ambapo kiasi kikubwa cha taka ngumu huzalishwa.

(2) Kabla ya mamlaka ya serikali za mitaa haijatenga eneo kuwa kituo cha kuweka taka ngumu kwa muda kwa madhumuni ya kukusanya taka ngumu, Mamlaka hiyo;

(a) itafanya tathmini ya athari kwa jamii, afya na mazingira;

(b) itahakikisha kuwa eneo hilo linatosha kwa ukubwa na liko mbali na makazi ya watu;

(c) itahakikisha uondoaji wa mara kwa mara wa taka ngumu ili kuepuka kero zinazoweza kujitokeza; na

(d) itahakikisha kwamba eneo hilo limewekewa uzio na linalindwa ili kuzuia watu wasiohusika kuingia.

**Hatua ya mwisho ya utupaji wa taka ngumu**

119 Mamlaka ya serikali za mitaa wakati wa kuchagua njia bora ya utupaji wa taka ngumu kwenye maeneo itazingatia mambo yafuatayo-

(a) hali ya tabianchi;
(b) uwezo kiuchumi;
(c) maslahi ya jumuia;
(d) manufaa ya kimazingira, kiafya na kijamii; na
(e) upatikanaji wa maeneo ya kujaziliza taka.

***(b) Usimamizi wa takataka***

**Ufafanuzi kuhusu usimamizi wa takataka**

120 Kwa madhumuni ya vifungu vya 121 na 122 isipokuwa pale ambapo muktadha unahitaji vinginevyo;

"ardhi ya umma" maana yake ni ardhi iliyokabidhiwa kwa Rais kama mdhamini wake, na inajumuisha ardhi ya kawaida au ardhi inayokaliwa binafsi.

"uwekaji"kuhusu takataka unajumuisha-

(a) kutupa kuweka, kurusha au kuangusha takataka;

(b) kuruhusu takataka kutupwa, kurushwa au kuangushwa au kudondoka kutoka kwenye chombo cha kusafirishia takataka;

"takataka" inajumuisha mabaki ya chakula, mabaki ya wanyama, vioo, chuma, plastiki, maganda, kifusi cha mvunjiko, uchafu, uvundo, mkojo, mabaki ya mvunjiko, kokoto, mawe, udongo, maji taka au kitu chochote kinachofanana na hali hiyo;

"ardhi binafsi" maana yake ni mahali popote ambapo si eneo la umma;
"eneo la umma"-

(a) linajumuisha mambo yafuatayo:-

(i) kila barabara, mtaa, mtaa binafsi, kichochoro, njia ya kuingilia mifereji/mitaro ya maji ya mvua, barabara ya pembeni mwa barabara kuu, mahakama , nyumba ya biashara mbalimbali, gati na uwanja wa ndege ambapo kwa kawaida watu huweza kuingia kwa malipo au hata bila malipo na inajumuisha mbuga au hifadhi yoyote ya taifa;

(ii) mbuga, bustani au mahali popote pa burudani ambapo umma huweza kuingia, iwe kwa malipo au hata bila malipo yoyote;

(iii) pwani au ufukwe wowote au ukingo wa mto au kijito chochote, au ukingo wa ziwa lolote ambako kwa kawaida umma huweza kuingia iwe kwa malipo au bila malipo;

(iv) sehemu yoyote ya maji, ambayo kwa kawaida umma huweza kuingia kwa madhumuni mengine ya kuburudika iwe kwa kulipia au bila malipo yoyote;

(v) kila gati, kidaraja cha kupanda kuingia au kushuka melini, au ambacho umma hutumia, au kikuta dhidi ya kuingia, ambacho umma huweza kuingia;

(vi) uwanja wowote wa ndege;

(vii) ardhi yoyote ya matumizi ya umma iliyodhaminishwa kwa Rais au inayodhibitiwa naye ambapo ardhi hiyo haimilikiwi chini ya utaratibu wowote wa pango, leseni au mamlaka nyingineyo ya mtu yeyote binafsi;

(viii) mahali pengine popote panapomilikiwa na umma au binafsi palipo wazi ambapo watu huweza kuingia, iwe kwa malipo au bila malipo yoyote; lakini

(b) haijumuishi eneo lolote lililotengwa au lililoidhinishwa kwa madhumuni ya kutupia taka kwa mujibu wa Sheria hii au sheria nyingine yoyote au jalala lililojengwa katika eneo la umma.

**Udhibiti wa takataka kwenye maeneo ya umma**

121 (1) Kila mtu anayemiliki au kusimamia eneo la umma lenye uwezekano wa kuwa na takataka, wakati wote, atapaswa kuweka na kutunza ndani ya eneo hilo idadi ya majalala inayoweza kuhimili takataka zinazotupwa kwa muda katika eneo hilo kadiri itakavyohitajika ili kulifanya eneo hilo kubaki bila takataka.

(2) Pale ambapo takataka zinazalishwa au kudhaniwa kuzalishwa hasa kwenye jengo au eneo lolote, zinazoonesha uwezekano wa kuchukuliwa au kupeperushwa kwa namna yoyote kutoka kwenye jengo au eneo hilo kuingia kwenye eneo lolote, Mkaguzi wa Mazingira anaweza kumtaka mkazi kuchukua hatua zinazostahili kuzuia takataka hizo kuchukuliwa au kupeperushwa kuingia kwenye eneo la umma.

(3) Pale inapoonekana kuwa takataka nyingi zaidi zinadhaniwa au zinajitokeza kutoka kwenye majengo au eneo mahsusi, Mkaguzi wa Mazingira anaweza kuwataka wakazi wa jengo au eneo hilo kutoa na kutunza idadi ile ya majaa ya takataka yanayoweza kuhimili takataka kwenye eneo la umma jirani na, au karibu na majengo au maeneo ya kutupa takataka kwa muda ili kuhakikisha eneo hilo linabaki bila takataka.

(4) Pale ambapo mkazi yeyote atashindwa kuzingatia ndani ya wakati muafaka agizo lililotolewa na Mkaguzi wa Mazingira chini ya kifungu cha (2) au (3), ofisa huyo anaweza kuchukua hatua zozote zinazofaa ili kurekebisha kosa hilo, na mkazi huyo atafidia gharama hizo kama deni la huduma iliyotolewa.

(5) Mtu yeyote ambaye fungu hili linamhusu atapaswa pia kuweka utaratibu unaofaa wa kumwaga takataka zilizomo kwenye majaa ambayo yapo kwenye maeneo ya umma yaliyo chini ya udhibiti na usimamizi wake, na ataziondoa na kuzitupa takataka hizo haraka iwezekanavyo na kwa ufanisi.

**Wamiliki wa ardhi binafsi kuondoa takataka**

122 Mkaguzi wa Mazingira anaweza kumpelekea notisi ya maandishi mmiliki au mkazi wa ardhi yoyote binafsi au ardhi yoyote iliyodhaminishwa au iliyo chini ya udhibiti wa mtu yeyote kumtaka mmiliki au mkazi huyo kutekeleza kwa kiasi cha kumridhisha Mkaguzi wa Mazingira mambo yafuatayo:-

(a) kuondoa au kuondosha kutoka kwenye ardhi;

(b) kusafisha; au

(c) kukinga, kufunika au vinginevyo kuzificha takataka hizo zisionekane kwa wakati huo kadiri itakavyokuwa inaelekezwa katika notisi.

***(c) Usimamizi wa Taka Vimiminika.***

**Utupaji wa taka vimiminika katika eneo zilipozalishwa**

123 (1) Mamlaka za serikali za mitaa zanaweza kubainisha na kuweka miongozo kuhusu jinsi ya kushughulikia taka vimiminika toka majumbani na maeneo ya biashara na hatimaye kuondoa kabisa taka maji katika maeneo hayo na nje ya maeneo hayo.

(2) Bila kuathiri kifungu cha (1), Waziri anaweza kutoa miongozo mahsusi ambayo itazingatiwa na mamlaka ya serikali za mitaa au mamlaka za maji taka katika utupaji wa taka vimiminika za kawaida au mahsusi.

**Usafirishaji wa**

124 Mamlaka za serikali za mitaa, kwa kuzingatia maeneo yaliyo chini ya mamlaka

**taka vimiminika**

zao, zitatoa na kuweka miongozo na viwango vya jinsi ya kukusanya maji taka na taka tope kutoka shimo la maji taka na kuisafirisha kwa magari maalumu kwa ajili ya kutupwa.

**Jinsi ya kusafisha taka vimiminika**

125 Mamlaka ya serikali za mitaa itahakikisha kwamba maji taka yanasafishwa ipasavyo kabla ya kumwagwa katika maeneo ya kukusanyia maji taka au ardhi iliyo wazi, na hayaongezi hatari ya maradhi au kuvuruga ikolojia na kusababisha uharibifu wa mazingira.

**Utupaji wa taka vimiminika**

126 Mamlaka za serikali za mitaa itatenga malambo kwa ajili ya kumwaga maji taka na kuhakikisha upatikanaji zana za kusafishia maji taka na vituo vya kupitishia maji taka hayo.

**Udhibiti na upelembaji wa mfumo wa maji taka**

127 Baada ya kukamilisha ujenzi wa mfumo wa maji taka, mamlaka ya serikali za mitaa itahakikisha majaribio ya awali, na mengineyo ya kipindi hadi kipindi yanafanyika ili kuhakikisha kwamba taka vimiminika inayokusudiwa kutupwa imefikia viwango vitakavyokuwa vimeagizwa na Waziri kabla ya hatua ya mwisho ya kutupwa.

**Taka vimiminika za viwandani**

128 Waziri atatunga kanuni zinazobainisha njia bora za kusafisha taka vimiminika kutoka viwandani zenye madhara na zisizo na madhara.

**Usimamizi wa maji ya mvua**

129 (1) Kila mamlaka ya serikali ya mitaa kwenye eneo lake itajenga au kuandaa mifereji ya maji ya mvua.

(2) Mifereji ya maji ya mvua daima itapaswa kuwa safi kwa madhumuni yaliyoifanya ijengwe.

(3) Waziri anaweza kutoa amri kuhusu-

(a) kiwango cha mwinuko wa mifereji ya maji ya mvua ili kuzuia maji yasituame;

(b) usafishaji wa mifereji ya maji ya mvua kipindi hadi kipindi ili kuondosha mrundikano wa tope;

(c) mifereji ya maji ya mvua iliyofunikwa mifuniko kwa ajili ya ukaguzi na chemba kwa ajili ya ukaguzi na uondoaji wa mrundikano wa mchanga au tope.

***(d) Usimamizi wa Gesi Taka***

**Gesi taka kutoka majumba ya makazi**

130 Mamlaka ya serikali za mitaa itahakikisha kwamba majumba yote ya makazi:-

(a) yana nafasi wazi za kutosheleza kuingiza na kutoa hewa;

(b) yanatoa njia zinazotosheleza kutolea moshi kutoka jikoni na maeneo mengine ndani ya nyumba kama itakavyopasa; na

(c) hayaruhusu kupikia ndani ya nyumba za makazi au kutumia samadi kama nishati ya kupikia katika maeneo yaliyotengwa na hayapitishi hewa.

**Udhibiti wa gesi taka za viwandani**

131 (1) Mamlaka za serikali za mitaa zitahakikisha kuwa viwanda vinavyozalisha gesi taka vinajengwa mbali kutoka maeneo ya makazi ya watu kwa kuzingatia mwelekeo wa upepo na mapendekezo ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

(2) Kila mamlaka ya serikali za mitaa itaweka na kubainisha sheria ndogo taratibu na adhabu zinazosimamia:

(a) utaratibu wa mara kwa mara wa ukaguzi wa mitambo ili kuhakikisha inafanya kazi kwa ufanisi na haisababishi utoaji wa gesi; na

(b) vipimo vya dohani na vifaa vya udhibiti wa gesi vinavyopaswa kufungwa kwenye karakana na viwanda.

**Gesi taka na taka chembechembe kutoka kwenye magari.**

132 (1) Mamlaka ya serikali za mitaa itabainisha taratibu za kisheria zenye kubainisha utoaji gesi kutoka kwenye ekzosi zitakazotumika katika maeneo yake.

(2) Pale ambapo viwango vya kitaifa vimewekwa, mamlaka ya serikali za mitaa itapaswa kutumia viwango vilivyowekwa kitaifa vya utoaji wa gesi kutoka kwenye ekzosi.

***(e) Usimamizi wa Taka zenye Madhara***

**Uingizaji na utoaji nchini wa taka zenye madhara**

133 (1) Itakuwa ni kosa kuingiza au kusafirisha nje ya Tanzania taka zenye madhara bila kuwa na kibali kilichotolewa na Waziri.

(2) Pale ambapo taka zenye madhara zitasafirishwa nje ya Tanzania, mtu anayetaka kusafirisha taka hizo itamlazimu kupata kibali kimaandishi kitakachotolewa na mamlaka inayotambulika kwenye nchi itakayopokea taka hiyo.

(3) Mtu yeyote hataruhusiwa kusafirisha taka zenye madhara ndani ya nchi au kupitia Tanzania.

(4) Waziri anaweza kutunga kanuni zinazobainisha mambo yafuatayo:-

(a) njia bora zaidi zinazowezekana kusimamia aina mbalimbali za taka zenye madhara pamoja na adhabu zinazotolewa dhidi ya ukiukwaji wowote;

(b) uwajibikaji na dhamana kwa mtu aliyehusika katika uzalishaji, usafirishaji, utoaji nje ya nchi na utupaji wa taka zenye madhara;

(c) taratibu za utoaji wa taarifa juu ya usafirishaji na utupaji wa taka zenye madhara;

(d) mahitaji yoyote ya utoaji taarifa juu ya utekelezaji wa mikataba ya kimataifa kuhusu taka zenye madhara na yale matukio yanayoweza kusababisha madhara kwa afya ya binadamu, viumbe hai na mazingira;

(e) vyombo vilivyosajiliwa vinavyotumika katika utupaji wa taka zenye madhara;

(f) uwajibikaji na dhamana kwa mtu au kundi la watu waliosababisha uchafuzi wa mfumo wa ikolojia ya mazingira, au wamiliki wa maeneo kama hayo;

(g) vigezo vyenye kubainisha maeneo yaliyochafuliwa na taka zenye madhara; na

(h) kusafisha maeneo yaliyochafuliwa na taka zenye madhara.

(5) Waziri anaweza kuelekeza vigezo kuhusu kuweka matabaka ya taka zenye madhara kwa nia ya kufahamu hali ya-

(a) madhara yake;

(b) ubabuzi wake kikemikali;

(c) uwezekano wake wa kusababisha saratani;

(d) uwakaji wake;

(e) udumufu kwake;

(f) usumu wake;

(g) ulipukaji wake; na

(h) mionzi umionzi wake.

**Wajibu wa mamlaka ya serikali za mitaa kuhusiana na taka zenye madhara**

134 (1) Kila mamlaka ya serikali ya mitaa kwenye maeneo yake itahakikisha kwamba:

(a) viwango vilivyowekwa vya usimamizi wa taka zenye madhara vipo na vinatumika wakati wote.

(b) maeneo yanayozalisha taka zenye madhara yana nafasi ya kutosha kutolea hewa na yanazingatia viwango vilivyowekwa.

(c) taka vimiminika zinasafishwa au kubadilishwa kwa kuzingatia viwango vilivyobainishwa kabla ya utupwaji wa mwisho; na

(d) taka vimiminika zenye madhara zinasafishwa kulingana na viwango vya mazingira vilivyobainishwa kiwandani au mahali taka zinapozalishwa kabla ya kumwagwa kwenye mifereji ya maji taka, madimbwi ya manispaa ya kuhifadhia maji taka au mahali pa wazi au majini.

(2) Kila viwango na miongozo iliyowekwa na serikali ya mitaa kwa madhumuni ya Sheria hii, vitazingatia viwango vilivyowekwa chini ya Sheria hii.

**Usafirishaji wa taka zenye madhara**

135 (1) Waziri atahakikisha kwamba usafirishaji wowote wa taka zenye madhara kutoka au kupitia Tanzania utafanyika kwa namna ambayo inazuia au kupunguza kuwepo kwa athari kwa afya ya binadamu na kwa mazingira, na kwamba utazingatia taratibu za usafirishaji kama itakavyokuwa umebainishwa katika kanuni.

(2) Mzalishaji yeyote wa taka zenye madhara atapashwa kuchukua hatua

kupunguza uzalishaji wa taka hizo.

(3) Mwenye kuzalisha taka zenye madhara atawajibika kuzitupa na pia atabeba dhamana kwa madhara ya taka hizo kwa afya ya watu, viumbe hai na kwa mazingira.

**Tathmini ya Athari kwa Mazingira kuhusu taka zenye madhara**

136 (1) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha (2), utupaji wa taka yoyote yenye madhara utafanywa kwa utaratibu unaojali uhifadhi wa mazingira safi.

(2) Tathmini ya Athari kwa Mazingira italazimu kufanyika kabla ya taka zenye madhara hazijatupwa udongoni, ardhini, hewani au kwenye vyanzo vya maji.

**Hatua ya mwisho ya utupaji wa taka na huduma za afya**

137 (1) Waziri, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya afya, atahakikisha kwamba taka zitokanazo na huduma za afya zinachambuliwa na kutunzwa katika kontena maalumu zilizobainishwa na kusafirishwa kwenye magari maalumu yaliyoundwa na kusajiriwa kwa madhumuni hayo.

(2) Waziri, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya afya, ataagiza njia bora zaidi ziwezekanazo kwa ajili ya utupaji wa mwisho wa taka za aina mbalimbali zinazozalishwa kutokana na huduma za afya.

(3) Katika kifungu hiki, “taka zitokanazo na huduma za afya;” zinajumuisha, lakini hazitahusisha tu taka zenye kuambukiza magonjwa, taka za kipatholojia, vitu vyenye ncha kali, dawa, genetoksiki, taka zenye mionzi, taka za mgando wa damu na dawa za binadamu.

**Utupaji wa taka nyinginezo**

138 Waziri, kwa kushauriana na wizara nyingine  na mamlaka nyinginezo, ataagiza njia zaidi zinazowezekana za ushughulikiaji na utupaji wa:-

(a) taka za mifugo zitokazo machinjioni;

(b) dawa za mifugo;

(c) taka zitokanazo na shughuli za kilimo;

(d) taka za madawa ya kilimo;

(e) taka za kemikali; na

(f) aina nyingine yoyote ya taka, kama Waziri atakavyoamua.

**Uwezo wa jumla wa mamlaka ya Serikali za Mitaa kupunguza taka**

139 (1) Bila ya kuathiri madaraka yaliyotolewa kwa mujibu wa sheria yoyote iliyoandikwa kuhusu usimamizi wa taka, kila mamlaka ya serikali za mitaa itakuwa na madaraka yanayostahili kwa madhumuni ya kuzuia au kupunguza taka ngumu, taka vimiminika, gesi taka na taka zenye madhara.

(2) Kwa madhumuni ya usimamizi wa taka, Waziri anaweza kumshauri Waziri mwenye dhamana ya masuala ya serikali za mitaa, kumwelekeza au kumpa mtu yeyote madaraka iliyo nayo mamlaka ya serikali za mitaa ambayo

imeshindwa kutimiza wajibu wake au kutumia uwezo huo kuhusu jambo lolote lililobainishwa chini ya Sehemu hii.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha (2) kwenye shauri linalostahili, Waziri, katika hali inayofaa, anaweza kuelekeza au kumpa mtu yeyote madaraka kutumia mamlaka hayo kuhusu jambo lolote lililoagizwa kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii.

## SEHEMU YA X
## VIWANGO VYA UBORA WA MAZINGIRA

**Uzingatiaji wa viwango**

140 (1) Kamati ya Taifa ya Viwango vya Mazingira ya Shirika la Viwango Tanzania iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Shirika la Viwango Tanzania ya mwaka 1975, itaandaa, kupitia na kuwasilisha kwa Waziri pendekezo la viwango na vigezo vya mazingira kuhusu-
(a) ubora wa maji;
(b) umwagikaji wa taka vimiminika;
(c) ubora wa hewa;
(d) udhibiti wa kelele na uchafuzi unaotokana na mtikisiko;
(e) mitikisiko itokanayo na sauti hafifu;
(f) ubora wa udongo;
(g) udhibiti wa harufu zenye madhara;
(h) uchafuzi wa mwanga;
(i) mawimbi ya umeme sumaku na vijiwimbi; na
(j) kiwango kingine chochote cha ubora wa mazingira.

(2) Kamati ya Taifa ya Mazingira itahakikisha kwamba viwango vimechapishwa kwenye *Gazeti la Serikali* na angalau katika magazeti mawili ya kawaida yachapishwayo kila siku, moja likiwa kwa Kiswahili na lingine likiwa kwa Kiingereza, kwa nia ya kukaribisha maoni yatakayotolewa kwa maandishi kuhusu viwango vilivyopendekezwa ndani ya muda unaoweza kuwekwa.
(3) Baada ya kuidhinishwa kwa ubora wa viwango na vigezo vya mazingira, Waziri atavibainisha katika *Gazeti la Serikali*.
.

**Uzingatiaji wa viwango**

141 Kila mtu anayefanya shughuli yoyote atapaswa kuzingatia ubora wa viwango na vigezo vya mazingira.

**Utekelezaji wa ubora wa viwango vya mazingira**

142 (1) Katika kutekeleza ubora wa viwango na vigezo vya mazingira, Baraza linaweza-
(a) kuagiza au kuendesha uchunguzi kuhusu uchafuzi au uchafu wa mazingira unaoshukiwa, ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa sampuli, kumbukumbu na data;
(b) kuingia, kukagua na kuchambua mahali popote, eneo, jengo au gari lolote, boti, ndege au kichukuzi chochote chenye umbo la aina yoyote, shughuli ambayo inaaminika kwamba inasababisha au inaweza

kusababisha ukiukwaji wa viwango vya mazingira;

(c) kuchukua hatua muhimu;

(d) kufuatilia mkolezo wa utoaji na hali ya vichafuzi vinavyotolewa;

(e) kuandaa miongozo ili kupunguza gesi zinazosababisha ongezeko la joto la dunia na utoaji wa gesi taka nyinginezo na kubainisha teknolojia inayofaa kwa upunguzaji wa uchafuzi wa hewa; au

(f) kufanya au kutenda jambo lolote ambalo ni muhimu kwa upelembaji na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya sheria nyingine yoyote, mtu yeyote atakayeruhusu au kusababisha uchafuzi au utoaji unaozidi viwango vya ubora na vigezo vya mazingira kama ilivyotajwa kwa mujibu wa Sheria hii, atakuwa anatenda kosa.

(3) Baraza litaendeleza ushirikiano wa karibu na mamlaka ya serikali za mitaa, Mamlaka ya Idara ya Afya ya Jamii, Wakala wa Mionzi, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Chakula na Madawa na asasi nyingenezo kwa madhumuni ya utekelezaji wa ubora wa viwango vya mazingira.

**Viwango vya ubora maji**

143 Kamati ya Taifa ya Viwango vya Mazingira-

(a) itabainisha vigezo na utaratibu wa kupima viwango vya ubora wa maji;

(b) itaweka kima cha chini sana cha ubora wa viwango vya maji yote ya Tanzania;

(c) itaweka kima cha chini sana cha ubora wa viwango kwa matumizi tofauti ya maziwa, ikiwa ni pamoja na:

(i) maji ya kunywa;

(ii) maji kwa matumizi ya kilimo;

(iii) maji kwa ajili ya burudani;

(iv) maji kwa ajili ya uvuvi na wanyama pori;

(v) maji kwa viwanda;

(vi) maji kwa mazingira; na

(vii) maji kwa madhumuni mengine yoyote.

**Viwango vya kumwaga vimiminika taka majini**

144 Kamati ya Taifa ya Viwango vya Mazingira-

(a) itaweka viwango kuhusu umwagikaji wa mtiririko wowote wa maji machafu kwenye mito, maziwa na bahari nchini Tanzania;

(b) itaweka vipimo vya kushughulikia mtiririko wa maji machafu katika hatua za mwanzo kabla ya kumwagwa moja kwa moja ndani ya mfumo wa mifereji ya maji taka; na

(c) itabainisha mahitaji ya mwendeshaji wa mtambo wowote au shughuli yoyote kuendesha kazi hiyo kwa namna ambayo itaona inafaa katika kushughulikia mtiririko wa maji machafu katika hatua za mwanzo kabla ya kumwagwa moja kwa moja kwenye mito na maziwa.

**Viwango vya obora wa hewa**

145 Kamati ya Taifa ya viwango vya Mazingira-

(a) itabainisha vigezo na utaratibu muhusu upimaji wa ubora wa hewa;

(b) itaweka viwango vya ubora wa hewa inayozunguka;

(c) itaweka viwango vya ubora wa hewa unaofaa kwenye sehemu za kazi;

(d) itaweka viwango vya utoaji taka kwa vyanzo mbalimbali vya taka;

(e) itabainisha vigezo na miongozo kuhusu udhibiti wa uchafu wa hewa kutoka vyanzo vya vitu jongevu na tuli; na

(f) ubora wa viwango kuhusu utokaji wowote wa hewa.

**Viwango vya kudhibiti harufu yenye madhara**

146 Kamati ya Taifa ya Viwango vya Mazingira-

(a) itabainisha taratibu za upimaji na udhibiti wa harufu yenye madhara;

(b) itaweka viwango vya chini kwa madhumuni ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira kwa harufu yenye madhara; na

(c) itaweka miongozo kuhusu vipimo na uondoaji wa harufu yenye madhara inayotokana ama na shughuli za binadamu au mazingira halisi.

**Viwango vya kudhibiti uchafuzi kwa kelele au mtikisiko**

147 Kamati ya Taifa ya Viwango vya Mazingira

(a) itabainisha taratibu kuhusu vipimo na uchunguzi wa uchafuzi kwa kelele na mitikisiko;

(b) itaweka viwango vya chini kuhusu utoaji uchafuzi kwa kelele na mitikisiko kwenye mazingira;

(c) itaweka vigezo na taratibu kuhusu vipimo vya uchafuzi kwa kelele na mtikisiko kutoka vyanzo vilivyopo na vya siku zijazo;

(d) itabainisha miongozo kuhusu uondoaji kelele zisizo na maana au mtikisiko unaofanyika kwenye mazingira;

(e) itaweka viwango vya chini vya utoaji wa kelele na mtikisiko vinavyofaa kwenye maeneo ya ujenzi, mitambo, magari, vyombo vya anga pamoja na vipaza sauti, na kwenye shughuli za kiviwanda na kibiashara;

(f) itachukua hatua madhubuti kuhusu uondoaji na udhibiti wa kelele kutoka kwenye vyanzo vilivotajwa kwenye aya (e); na

(g) itapima viwango vya kelele inayotoka kwenye vyanzo vilivyotajwa kwenye aya (e).

**Viwango kuhusu mitikisiko itokanayo na sauti**

148 Kamati ya Taifa ya Viwango vya Mazingira-

(a) itabainisha taratibu kuhusu vipimo na uchunguzi kuhusu viwango vya mitikisiko itokanayo na sauti;

(b) itaweka viwango vya chini kuhusu utoaji wa mitikisiko itokanayo na sauti kwenye mazingira kutoka kwenye vyanzo vilivyopo na vya siku zijazo;

(c) itaweka vigezo na taratibu kuhusu upimaji wa mitikisiko itokanayo na sauti; na

(d) itabainisha miongozo ya upunguzaji wa mitikisiko itokanayo na sauti

iliyotajwa kwenye aya (b)

**Viwango kuhusu upunguzaji wa mionzi**

149 Kamati ya Taifa ya Viwango vya Mazingira

(a) itaweka viwango kuhusu upunguzaji wa uionishi na mionzi mingineyo kwenye mazingira;

(b) itaweka vigezo na taratibu kuhusu upimaji wa uionishi na mionzi mingine;

(c) itatoa taarifa ya ilani na ulinzi kwa umma na mazingira dhidi ya hatari ya kujianika wazi mbele ya maunzi yenye mionzi au maunzi ionishi, na itabainisha taratibu za kiusalama za akuwalinda watu ambao shughuli zao daima zinakabiliwa na athari za mionzi; na

(d) itafanya mambo yote ambayo ni ya lazima kwa Upelembaji na udhibiti wa uchafuzi utokanao na mionzi.

**Viwango vya bora wa udongo**

150 Kamati ya Taifa ya Viwango vya Mazingira-

(a) itaweka vigezo na taratibu kuhusu vipimo na uchunguzi wa viwango vya ubora wa udongo;

(b) itaweka viwango vya chini kuhusu usimamizi wa ubora wa udongo;

(c) itatoa miongozo kuhusu utunzaji, utumizi bora wa udongo wowote, utambuzi wa aina mbalimbali za udongo na upigaji marufuku wa shughuli zinazoweza kuathiri ubora wa udongo; na

(d) itafanya mambo ambayo ni ya lazima katika upelembaji na udhibiti wa athari kwa udongo.

## SEHEMU YA XI
## AMRI ZA UREJESHWAJI, UPITISHAJI NJIA NA UHIFADHI WA MAZINGIRA

**Amri ya urejeshwaji wa mazingira**

151 (1) Kwa kuzingatia masharti yaliyo ndani ya Sheria hii, Baraza linaweza kutoa amri kwa mtu yeyote itakayohusiana na jambo lolote juu ya usimamizi wa mazingira itakayojulikana kama amri ya urejeshwaji wa mazingira.

(2) Amri kuhusu urejeshwaji wa mazingira itatolewa kwa madhumuni ya-

(a) kumtaka mhusika kurejesha mazingira yaliyoharibika;

(b) kumzuia mhusika asifanye shughuli yoyote inayoweza kuharibu mazingira;

(c) kulipisha fidia kutoka kwa mtu anayeharibu mazingira ili kuwalipa waathirika ambao mazingira yao yameharibiwa au maisha yao yameathiriwa na uharibifu huo wa mazingira na kitendo ambacho ndicho kimesababisha kutolewa kwa amri hiyo.

(d) kumtoza mhusika kodi ambayo itakadiriwa na Baraza kuwa ni gharama sahihi inayoweza kutumiwa na mtu yeyote au asasi iliyoidhinishwa ili urejeshwaji wa mazingira yaliyoharibiwa.

(3) Amri ya urejeshwaji wa mazingira inaweza kuwa na masharti na

mashuruti na inaweza kutoa maagizo kwa mhusika kadiri itakayokuwa kwa ajili kuwezesha amri hiyo kufikia madhumuni yaliyotajwa ndani ya kifungu cha (2).

(4) Bila ya kuathiri madhumuni ya jumla yaliyotajwa ndani ya kifungu cha (3), amri ya urejeshwaji wa mazingira inaweza kumtaka mhusika;

(a) kuchukua hatua zitakazozuia kuanza au kuendelea kwa uchafuzi au chanzo kinachosababisha uchafuzi wa mazingira;

(b) urejeshwaji wa ardhi ikiwa ni pamoja na kubadilisha udongo, kupanda upya miti na mimea mingine, na urejeshwaji huo unaweza kuzingatia hali halisi ya kijiolojia, mambo ya kale au mandhari ya kihistoria, ardhi au eneo husika au bahari inayopakana nayo kadri itakavyokuwa kwenye vielelezo katika amri;

(c) kuchukua hatua za kuzuia, kuanza, au kuendelea kwa majanga ya mazingira au chanzo kinachoweza kusababisha majanga ya mazingira;

(d) kuacha kufanya shughuli yoyote inayosababisha, au inayoweza kuchangia uchafuzi au kuleta majanga ya mazingira;

(e) kuondoa au kupunguza uharibifu kwenye ardhi au mazingira au miundombinu iliyopo kwenye eneo husika;

(f) kuzuia uharibifu kwenye ardhi au kwenye mazingira, vyanzo vya maji chini ya ardhi, mimea na wanyama waliomo ndani, au chini au juu ya ardhi au baharini, au ardhi au mazingira ya eneo lililo mkabala na ardhi au bahari iliyotajwa kwenye amri;

(g) kuondoa takataka au taka yoyote ambayo imerundikana kwenye ardhi au bahari iliyotajwa kwenye amri na kutupa takataka au taka hizo kwa kuzingatia masharti ya amri; na

(h) kulipa fidia yoyote iliyotajwa kwenye amri.

(5) Katika kutekeleza mamlaka kwa mujibu wa Sehemu hii, Baraza-

(a) litaongozwa na misingi ya usimamizi wa ubora wa mazingira kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii; na

(b) litawaeleza watu waliopewa amri hiyo haki waliyo nayo ya kukata rufaa kwenye vyombo vilivyotajwa vyenye mamlaka ya kusilikiza rufaa.

**Maudhui ya amri ya urejeshwaji wa mazingira**

152 (1) Amri ya urejeshwaji wa mazingira itafafanua wazi na kwa ufasaha kuhusu

(a) shughuli husika

(b) walengwa;

(c) muda ambao amri itaanza kutekelezwa;

(d) hatua ambayo lazima ichukuliwe ili kurekebisha uharibifu wa mazingira

katika muda usiozidi siku thelathini au muda zaidi ya hapo kama ilivyobainishwa katika amri husika;

(e) uwezo wa Baraza kuingia kwenye ardhi yoyote na kuchukua hatua iliyotajwa katika aya (d);

(f) adhabu zinazoweza kutolewa iwapo hatua katika aya (d) hazikuchukuliwa; na

(g) haki ya mtu aliyepewa amri ya urejeshwaji wa mazingira kukata rufaa dhidi ya amri hiyo kwenye Baraza la Rufaa au chombo chochote kilichobainishwa, isipokuwa pale amri hiyo inapokuwa imetolewa na mahakama yenye mamlaka, katika hali hiyo itakuwepo haki ya rufaa kwenda kwenye mahakama ya juu.

(2) Mkaguzi wa Mazingira anaweza kukagua au kuagiza ukaguzi ufanyike kuhusu shughuli yoyote kwa madhumuni ya kufahamu kama shughuli hiyo ina madhara kwa mazingira, na anaweza kutumia ushahidi utakaopatikana kwenye ukaguzi huo kutoa uamuzi wowote kuhusu ama kutekelezwa au kutotekelezwa kwa amri ya urejeshwaji wa mazingira.

**Utoaji wa amri ya urejeshwaji wa mazingira**

153 Pale ambapo Baraza litakuwa na sababu za kutilia mashaka kwamba madhara yametokea au yanaweza kutokea kwenye mazingira kutokana na shughuli za mtu yeyote, linaweza kumpa mtu huyo amri ya urejeshwaji wa mazingira au kuzuia uharibifu wa mazingira katika muda wa siku thelathini tangu kutolewa kwa amri kama ilivyobainishwa kwenye amri hiyo.

**Ushauri kabla ya kutoa amri ya urejeshwaji wa mazingira**

154 Baraza linaweza kuomba na kuzingatia ushauri wa kiufundi, kitaalamu na kisayansi ambao litaona unafaa ili kufikia uamuzi sahihi kuhusu urejeshwaji wa mazingira.

**Muda wa amri ya urejeshwaji wa mazingira**

155 (1) Amri ya urejeshwaji wa mazingira itaendelea kutumika katika shughuli yeyote kwa kuzingatia sababu iliyofanya amri hiyo itolewe bila kujali kwamba amri hiyo ilikwisha kutekelezwa hapo awali au la.

(2) Mtu aliyepewa amri ya urejeshwaji wa mazingira kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii atapaswa kuzingatia hali na masharti yote yaliyomo kwenye amri.

*(b) Amri ya Utoaji Haki ya Njia*

**Amri ya kutoa haki ya njia ya mazingira na hifadhi**

156 (1) Madhumuni ya haki ya njia ya mazingira yatakuwa ni kuimarisha misingi ya usimamizi wa mazingira ambayo imewekwa kwenye sheria hii kwa kurahisisha uhifadhi na uboreshaji mazingira kwa kuweka sharti moja au zaidi kuhusu matumizi ya ardhi hiyo.

**Sheria Na. 4 ya**

(2) Bila kujali hali ya haki ya njia zitakazowekwa kwa mujibu wa masharti

**mwaka 1999**

ya Sehemu ya XI ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, mahakama inaweza kutoa amri ya haki ya njia au uhifadhi wa mazingira chini ya masharti ya Sheria hii kutokana na maombi yatakayotolewa kwa mujibu wa Sheria hii.

(3) Baraza linaweza kupendekeza kwa Waziri kuhusu upitishaji wa njia kwa madhumuni ya kulinda mazingira.

(4) Iwapo Waziri ameridhika kwamba pendekezo la Baraza linaweza kufanyiwa kazi, atapendekeza kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya ardhi kutoa haki ya njia kwa mujibu wa Sehemu ndogo ya 3 ya Sehemu ya XI ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999.

(5) Waraka au amri ya mahakama kuhusu haki ya njia kwa ajili ya kuhifadhi mazingira itaeleza wazi kuhusu-

(a) hali ya haki ya njia na masharti yake, ukomo na miiko inayohusiana na sababu zilizosababisha waraka huo utolewe;
(b) muda uliotolewa kwa ajili hiyo;
(c) ardhi au sehemu maalumu ya ardhi inayohusika na haki ya njia iliyotolewa;
(d) ardhi inayonufaika na haki ya njia; na
(e) mpango unaojitosheleza kufafanua kuhusu haki ya njia.

(6) Haki ya njia ya mazingira inaweza kuwekwa na baadaye ikawa sehemu ya ardhi tengwa kwa kudumu au kwa kipindi cha miaka kadhaa au kwa maslahi yanayowiana kwa mujibu wa sheria ya kimila kadiri mahakama itakavyoamua.

(7) Bila ya kujali masharti ya sheria yoyote iliyotungwa na Bunge, haki za njia zinazotolewa kwa madhumuni ya kuhifadhi mazingira zitadumu kwa zaidi ya muda wa hakimiliki au upangishaji, isipokuwa kama zitakuwa zimefutwa hapo awali.

**Maombi ya haki ya njia ya uhifadhi mazingira**

157 (1) Mtu yeyote au kundi la watu wanaweza kupeleka maombi yao mahakamani kuomba kupewa haki ya njia moja au zaidi kwa madhumuni ya kuhifadhi mazingira

(2) Mahakama inaweza kuweka masharti kuhusu utoaji huo wa haki ya njia kwa uhifadhi wa mazingira kadiri itakavyoona inafaa zaidi katika kuimarisha lengo la njia kwa uhifadhi wa mazingira**.**

**Utekelezaji wa haki ya njia ya mazingira**

158 (1) Mashtaka kuhusu utekelezaji wa haki ya njia ya mazingira yanaweza kufunguliwa na mtu yule ambaye haki ya njia ya mazingira imetolewa kwa jina lake tu.

(2) Mashtaka kuhusu haki ya njia ya mazingira yanaweza kupelekwa mahakamani ili kuomba:-

(a) kutoa amri ya urejeshwaji wa mazingira, au

(b) kutoa nafuu yoyote iliyopo kwa mujibu wa sheria juu ya haki ya njia kwenye ardhi.

(3) Mahakama inaweza kurekebisha taratibu zinazohusu utekelezaji wa mahitaji ya haki ya njia ya mazingira kadiri itakavyoonekana inafaa.

**Usajili wa haki ya njia ya mazingira**

159 (1) Pale ambapo haki ya njia ya mazingira imetolewa kwenye ardhi ambayo hatimiliki yake imesajiliwa chini ya Sheria iliyotungwa na Bunge, haki ya njia ya mazingira itasajiliwa kwa mujibu wa sheria yenye kubainisha mfumo huo wa usajili wa haki ya njia.

(2) Kwa kuongezea kwenye jambo lolote linaloweza kutakiwa kwa mujibu wa sheria yoyote iliyotungwa na Bunge inayobainisha kwa ujumla usajili wa haki ya njia, usajili wa haki ya njia ya mazingira utajumuisha:-

(a) jina la mwombaji wa njia ya mazingira akiwa ndiye mtu mwenye jina linaloandikishwa;

(b) hali ya haki ya njia na masharti, ukomo na miiko yoyote kwa mujibu wa kutolewa kwake;

(c) muda ambao utatolewa kwa ajili hiyo;

(d) ardhi au sehemu yake maalum inayohusika na njia iliyotolewa;

(e) ardhi inayonufaika na haki ya njia; na

(f) mpango unaotosheleza ufafanuzi kuhusu haki ya njia.

**Fidia kutokana na haki ya njia ya mazingira**

160. (1) Kwa mujibu wa Sheria hii mtu yeyote mwenye maslahi ya kisheria kwenye ardhi inayohusu haki ya njia ya mazingira atakuwa na haki ya kulipwa fidia inayowiana na thamani ya ardhi itakayochukuliwa.

**Sheria Na. 43 ya mwaka 1967 na Sheria Na. 4 ya mwaka 1999**

(2) Fidia kwa thamani yoyote ya ardhi iliyochukuliwa ambayo imetajwa chini ya kifungu cha (1) itatolewa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utwaaji wa Ardhi ya mwaka 1967 na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999.

*(c) Amri za Uhifadhi*

**Utoaji wa amri ya kuhifadhi mazingira**

161 Kwa madhumuni ya usimamizi wa mazingira, pale ambapo itahitajika kuweka haki ya njia kwenye ardhi tengwa, mamlaka ambayo ardhi hiyo ipo chini yake inaweza kumuomba Waziri kutoa amri ya kuhifadhi mazingira kwa ajili ya-

(a) kuhifadhi mimea na wanyama;

(b) kuhifadhi ubora na mtiririko wa maji kwenye bwawa, ziwa au chemchem;

(c) kuhifadhi jambo lolote maarufu la kijiolojia, kifiziolografia, kiikolojia, kiakiolojia au kihistoria kwenye ardhi inayowekewa njia;

(d) kuhifadhi mandhari;

(e) kuhifadhi sehemu ya wazi;

(f) kuruhusu watu kutembea kwenye njia maalumu;

(g) kuhifadhi matuta ya asili na hali halisi ya ardhi iliyowekwa njia;

(h) kuzuia au kuondoa mwanya wa shughuli yoyote kwenye ardhi iliyowekwa njia ambayo inalenga katika uchimbaji wa madini na utafutaji wa madini;

(i) kuzuia au kuondoa mwanya wa shughuli ya kilimo chochote kwenye ardhi iliyowekwa njia;

(j) kuweka na kuendeleza kazi kwenye ardhi iliyowekwa njia ili kupunguza au kuzuia athari kwa mazingira; au

(k) kuweka au kuendeleza ushoroba kwa ajili ya wanyamapori.

## SEHEMU YA XII
## UCHAMBUZI NA KUMBUKUMBU

**Uteuzi wa maabara za uchambuzi na uchukuaji wa sampuli**

162 Baraza, kwa amri iliyochapishwa kwenye *Gazeti la Serikali,* litateua-

(a) Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali;

(b) maabara yoyote teule kwenye chuo kikuu cha umma nchini;

(c) maabara yoyote teule iliyoundwa chini ya, au kwa mujibu wa sheria yoyote iliyotungwa na Bunge; na

maabara zozote teule za binafsi kuwa ndizo maabara ambazo kati ya mambo mengine zinaweza kutumika kwa madhumuni ya uchambuzi na uchambuzi rejea kwa madhumuni ya Sheria hii.

**Uteuzi wa wachambuzi na wachambuzi rejea**

163 (1) Amri inayoteua maabara kwa madhumuni ya uchambuzi inaweza kuteua wachambuzi rejea kutoka miongoni mwa wafanyakazi ndani ya maabara hizo teule au washiriki wao.

(2) Amri inayoteua maabara kwa madhumuni ya Sheria hii itataja kazi maalum za kimazingira zitakazofanywa na maabara hizo, ukomo wa shughuli au kitu ambacho maabara itakifanya na watu walioteuliwa kuwa wachambuziyanayohusu maabara hiyo.

**Hati ya uchambuzi na nguvu yake kisheria**

164 (1) Maabara ambayo imeteuliwa kama maabara ya uchambuzi au uchambuzi rejea, itatoa Hati ya Uchambuzi wa dutu yoyote itakayowasilishwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Hati ya Uchambuzi kitataja mbinu za uchambuzi zilizotumika na kitatiwa saini na mchambuzi au mchambuzi wa rejea kadiri hali itakavyokuwa.

(3) Hati ya Uchambuzi kinapotolewa kwa mujibu wa sehemu hii, itakuwa ni ushahidi wa kutosha kuonyesha ukweili uliotajwa kwenye cheti hicho kwa mujibu wa Sheria hii.

(4) Matokeo ya uchambuzi wowote uliofanywa na maabara yatakuwa wazi kwa kukaguliwa na watu wote wanaohusika baada ya kulipia ada iliyobainishwa.

**Utunzaji wa kumbukumbu kuhusu masuala yanayoathiri mazingira**

165 Baraza, kwa kutoa notisi kwenye *Gazeti la Serikali*, litaeleza:-

(a) shughuli zinazoathiri mazingira ambapo kumbukumbu zake zitapaswa kutunzwa kwa wajibu wa Sheria hii;

(b) maudhui ya kumbukumbu hizo na jinsi ya kuzitunza na kuzitoa; na

(c) upatikanaji wa kumbukumbu hizo kwa bei nafuu kwa ajili ya uhakiki, upelembaji na upelembaji wa tathmini ya mazingira, udhibiti wa uchafuzi, ukaguzi, uchunguzi na kwa madhumuni mengine yoyote yatakayoainishwa

**Uwasilishaji wa kumbukumbu za kila mwaka**

166 (1) Kumbukumbu ambazo zimetunzwa kwa mujibu wa fungu la 159 zitawasilishwa kwenye Baraza kila mwaka.

(2) Baraza litatunza na kuzihifadhi kumbukumbu hizo kwa namna ambayo itazingatia usiri wake.

**Utoaji wa matokeo ya uchambuzi**

167 Kwa kuzingatia usiri, hali itakavyokuwa pamoja na ada yoyote inayoweza kubainishwa, mtu yeyote anaweza kuziona kumbukumbu zozote zilizowasilishwa kwenye Baraza chini ya Sheria hii.

**Majukumu ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuhusu mazingira.**

**Sheria na 3 ya 2003**

168 Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali itapaswa kuliarifu Baraza juu ya ushauri wowote inayoupata kutoka Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Kemikali za Viwandani iliyoundwa chini ya Sheria ya Kemikali za Viwandani na Majumbani (Usimamizi na Udhibiti) ya mwaka 2003, kuhusu masuala yote yanayoonekana kuleta madhara kwa mazingira.

**Kubainisha taratibu za kushirikiana kuhusu kemikali chafuzi**

169 Baada ya kufanya ushauriano na Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya afya, viwanda, kilimo, sayansi na teknolojia, Waziri anaweza kutunga kanuni zinazobainisha mbinu ya ushirikiano baina ya Baraza na vyombo vilivyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Kemikali za Viwandani na Majumbani (Usimamizi na Udhibiti) ya mwaka 2003 kuhusu-

(a) maabara zilizoteuliwa kuwa zinafaa kutoa vyeti vya uchambuzi wa kemikali;

(b) Bodi ya Ushauri ya Wizara; na

(c) Kamati ya Dharura iliyoundwa chini ya fungu la 8 la Sheria ya

Kemikali za Viwandani na Majumbani (Usimamizi na Udhibiti) ya mwaka 2003.

**Wajibu wa kutoa taarifa kwa Baraza**

170 (1) Asasi zifuatazo zitatoa taarifa kwa Baraza juu ya mambo yanayohusiana na majukumu yao yanayoweza kuwa na madhara kwa mazingira:

(a) Taasisi ya Utafiti wa Viuavisumbufu;

(b) Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania;

(c) Mamlaka ya Chakula, Madawa na Vipodozi Tanzania;

(d) Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi; na

(e) Baraza la Tiba ya Wanyama la Tanzania.

**Sheria Na. 3 ya mwaka 2003**

2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha (1) masuala ambayo Baraza litahitaji taarifa yake ni:

(a) maeneo yaliyosajiliwa kwa madhumuni ya Sheria ya Kemikali za Viwandani na Majumbani (Usimamizi na Udhibiti) ya mwaka 2003;

(b) kumbukumbu za kemikali zote zilizozalishwa, zilizoingizwa nchini, zilizosafirishwa nchi za nje, zilizouzwa, zilizohifadhiwa au kutumiwa na kila moja ya asasi iliyotajwa kwenye kifungu cha (1);

(c) kumbukumbu za amri za upigaji marufuku, uzuiaji, au pengine uondoaji wa kemikali za matumiozi ya kawaida ambazo katika kila moja ya asasi zilitotajwa kwenye kifungu cha (1);

(d) kuhusiana na asasi zilizotajwa kwenye kifungu cha (1),

(i) mgawanyo wa wakaguzi na wachambuzi,
(ii) uwekaji wa lebo na ufungaji,
(iii) utupaji wa taka; na
(iv) kuhitimisha shughuli za wa mitambo

**Kumbukumbu za mazingira kuhusu shughuli za uchimbaji wa madini**

171 (1) Bila ya kuathiri utumiaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998, Kamishna wa Madini, kwa kupitia Mratibu wa Mazingira katika Sekta hiyo, atapeleka kwenye Baraza kama kumbukumbu za Serikali nakala za nyaraka zifuatazo zinazohusiana na mazingira:

(a) masuala yote ya mazingira yaliyopo kwenye makubaliano yanayotakiwa kufanywa baina ya Serikali na mmiliki wa hati ya madini au mwombaji wa hati ya madini;

(b) tafiti na tathmini za mazingira zilizofanywa na wataalamu au washauri waelekezi ambazo zinatakiwa kuambatishwa kwenye maombi kwa ajili ya leseni zikionyesha athari yoyote iliyoko kwenye mazingira na jinsi gani mwombaji huyo anapendekeza kuzuia, kuondoa au kupunguza athari yoyote mbaya kwa mazingira au makubaliano ya uendelezaji madini;

(c) masharti yoyote ya aina hiyo kuhusu ulinzi na uhifadhi wa

mazingira ambayo yanaweza kuwekwa kwenye leseni bakishi ya madini;

(d) mipango ya usimamizi wa mazingira au mapendekezo ya kuzuia uchafuzi au mipango ya ushughulikiaji taka, au mipango ya urejeshwaji wa ardhi na maji, au mipango ya kupunguza athari mbaya kwa mazingira zitokanazo na shughuli za uchimbaji wa madini, ambazo zinaweza kuandaliwa na waombaji wa leseni bakishi za madini.

(e) tathmini za athari kwa mazingira kuhusu shughuli za uchimbaji wa madini ulioanzishwa na waombaji wa leseni maalumu za uchimbaji madini kwa Waziri mwenye dhamana ya madini.

(f) mipango ya usimamizi wa mazingira iliyoambatishwa kwenye leseni maalumu za uchimbaji madini

(g) mipango ya usimamizi wa mazingira kwa mradi wowote ambayo imewasilishwa kwa ajili ya kuomba upya leseni na imekataliwa kutokana na athari zake kwa mazingira.

(2) Mkurugenzi wa Mazingira anaweza kutoa maagizo ya jumla au mahususi kwa kushauriana na Kamishna wa Madini kwa Mratibu wa Mazingira katika Sekta hiyo juu ya jambo lolote kuhusu utekelezaji wa masharti ya usimamizi wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998.

(3) Baraza litatunza nakala za kumbukumbu zilizopokewa kwa mujibu wa fungu hili kama kumbukumbu za Serikali na zitakuwa wazi kwa umma kwa kulipia ada iliyobainishwa.

## SEHEMU YA XIII

## TAARIFA, ELIMU NA UTAFITI KUHUSU MAZINGIRA

**Uhuru wa kupata taarifa za mazingira**

172 (1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha (2) na kanuni zilizotangazwa na Waziri, kila raia wa Tanzania atakuwa na uhuru wa kupata taarifa iliyohifadhiwa na Serikali kuhusu utekelezaji wa Sheria hii na kuhusu hali ya mazingira ilivyo na pia kuhusu hatari iliyopo sasa na hapo baadaye kwa mazingira, pamoja na uchafuzi wowote kwenye maji, hewa au kwenye ardhi na pia kuhusu utupaji, na uhifadhi wa taka zenye madhara.

(2) Ombi la taarifa lililotolewa kufuatia maelekezo ya kifungu cha (1) linaweza kukataliwa ikiwa-

(a) taarifa inayoombwa itahusisha nyaraka au data ambazo bado hazijakamilika, au mawasiliano ya ndani, au ikiwa ombi hilo

linaonyesha wazi halina umuhimu au ni la jumla mno;

(b) utulivu na usalama wa taifa utavurugika kutokana na kutolewa kwa taarifa inayoombwa;

(c) ni kwa sababu nzuri ya kulinda siri za biashara au viwanda;

(d) ombi haliko wazi au halitoi uhakika wa kuwezesha kupambanua taarifa inayoombwa;

(e) chombo ambacho ombi hilo limepelekwa kwake, hakina ufahamu wa taarifa inayotafutwa.

(3)Endapo ombi la kupewa taarifa litakataliwa, chombo kilichokataa ombi hilo kitapaswa kutoa sababu za kukataa kwake kwa maandishi.

(4) Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu wataweza kupata taarifa kuhusu utekelezaji wa Sheria hii na hali halisi ya mazingira na pia kuhusu hatari zilizopo kwa mazingira kwa sasa na siku zijazo, ikiwa ni pamoja na uchafuzi wowote kwenye maji, hewa au ardhi, na pia kuhusu utupaji na uhifadhi wa taka zenye madhara ambazo ni muhimu kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii au ya sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge kuhusu ulinzi wa mazingira na utumiaji wa maliasili.

(5) Litakuwa ni kosa la jinai kukataa kutoa taarifa iliyoombwa na Mkurugenzi wa Mazingira au Mkurugenzi Mkuu kwa madhumuni ya kutekeleza kazi zinazoendana na madaraka yao kwa mujibu wa Sheria hii.

**Mamlaka ya Baraza kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za mazingira**

173 Baraza litapaswa-

(a) kukusanya taarifa kuhusu mazingira na maliasili kulingana na data zilizopo;

(b) kwa kuzingatia sheria nyinginezo, kupata data yoyote iliyokusanywa kuhusu mazingira na maliasili;

(c) kuchambua taarifa inayohusu mazingira na maliasili;

(d) kusambaza taarifa kwa umma na kwa watu binafsi wanaohitaji taarifa hiyo;

(e) kuanzisha tafiti kwenye maeneo ya makazi ya watu na hali zinazosababisha athari kwa mazingira na masuala ya maendeleo;

(f) kuendesha kampeni za kutoa taarifa na elimu katika masuala mazingira;

(g) kubadilishana taarifa kuhusu mazingira na Asasi Zisizo za Kiserikali na mashirika ya kimataifa;

(h) kuratibu usimamizi wa taarifa za mazingira kutoka sekta za Wizara

za kisekta;

(i) kumshauri Waziri juu ya upungufu katika taarifa ya mazingira; au

(j) kutayarisha miongozo na kanuni za ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za mazingira kwa kushauriana na Wizara za kisekta.

**Mfumo Mkuu wa Taarifa za Mazingira**

174 Baraza litaandaa na kuendesha Mfumo Mkuu wa Taarifa za Mazingira ambao utaweka kwa pamoja matokeo, data na takwimu kutoka kwenye asasi za umma na binafsi wakati wa kushughulikia usimamizi na uangalizi wa mazingira.

**Taarifa ya Hali ya Mazingira**

175 (1) Mkurugenzi wa Mazingira ataandaa na kutoa taarifa kuhusu hali na usimamizi wa mazingira kila baada ya miaka miwili na taarifa hiyo itawasilishwa mbele ya Bunge.

(2) Mkurugenzi wa Mazingira anaweza kutoa taarifa nyingine yoyote ambayo anaona inafaa kwa kuelimisha umma juu ya mazingira na masuala mengine ya kimazingira

**Elimu na uhamasishaji kuhusu mazingira**

176 (1) Mkurugenzi wa Mazingira, kwa kushauriana na Wizara za Sekta husika, atachukua hatua zinazostahili katika kufungamanisha masuala ya mazingira shuleni, vyuoni, na katika asasi za elimu ya juu.

(2) Mkurugenzi wa Mazingira atapanga na kuendesha programu zenye lengo la kuhamasisha umma kuhusu maendeleo endelevu na usimamizi wa mazingira.

**Utafiti wa mazingira**

177 (1) Baraza litaendesha uchunguzi juu ya hali ya mazingira na linaweza kutafiti na kubashiri mabadiliko ya mazingira na litafanya tafiti zinginezo ambazo zinaweza kuchangia katika kuaanda sera na mipango ya kazi na mikakati inayohusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha (1), Waziri anaweza kuteua asasi yoyote kuwa chombo cha ushauri kitakachohusika na uimarishaji wa utafiti maalumu wa kisayansi uliokusudiwa, utoaji wa taarifa kwenye uwanda wa mazingira, upelembaji na tathmini ya ufanisi wa hatua ambazo zimechukuliwa.

## SEHEMU YA XIV

## USHIRIKISHWAJI WA UMMA KATIKA UAMUZI KUHUSU MAZINGIRA

**Ushirikishwaji wa umma katika uamuzi kuhusu mazingira**

178 (1) Umma una haki ya kupata taarifa kwa wakati mwafaka juu ya kusudio la mamlaka za umma zinapotaka kufanya uamuzi wa kiutawala au kisheria wenye athari kwa mazingira na kuhusu fursa zilizopo katika kushiriki kwao kwenye uamuzi huo.

(2) Umma una haki ya kushiriki katika uamuzi unaohusu uandaaji wa sera ya mazingira, mikakati ya mipango na programu, na kushiriki katika maandalizi ya sheria na kanuni zinazohusu mazingira.

(3) Taarifa zinazohusu uamuzi unaogusa mazingira zinaweza kutolewa kwa umma kabla ya tarehe ambayo uamuzi huo umepangwa kufanyika.

(4) Uhusishwaji wa umma katika kufanya uamuzi kuhusu masuala ya mazingira, utafanyika kupitia-

(a) notisi iliyotolewa kwa wakati na inayoweza kuwafikia watu wengi ikionyesha nia ya kufanya uamuzi huo kama vile uundaji na sera, mipango na programu zinazohusu mazingira;

(b) fursa inayotolewa kwa umma kutoa maoni yao kwa mdomo na kwa maandishi kuhusu sera za mazingira zinazopendekezwa;

(c) kupata taarifa za mazingira kwa mujibu wa Sheria hii, au sheria nyingine yoyote.

(5) Baraza na mamlaka nyingine husika zitaanzisha utaratibu wa kukusanya na kujibu maoni, dukuduku na maswali yaliyotolewa na umma kuhusu mazingira, ikiwa ni pamoja na-

(a) midahalo ya umma kama fursa ya kusikilizwa;

b) taarifa kuhusu mazingira na sehemu za kutolea malalamiko katika asasi zote za umma.

## SEHEMU YA XV
## MIKATABA YA KIMATAIFA

**Mikataba ya kimataifa kuhusu mazingira**

179 (1) Pale ambapo Jamhuri ya Muungano ni mwanachama wa mkataba wa kimataifa au kikanda unaohusu usimamizi wa mazingira, Waziri kwa kushauriana na Wizara husika ya kisekta-

(a) atabuni na kuandaa mapendekezo ya kisheria kwa tafakari ya Wizara husika kwa madhumuni ya utekelezaji wa mikataba hiyo; na

(b) kutambua hatua madhubuti ambazo ni muhimu kwa utekelezaji wa mikataba hiyo.

(2) Pale ambapo Wizara ya Kisekta inahusika kwenye majadiliano ya mkataba wa kimataifa kuhusu masuala ya ulinzi na usimamizi wa kimataifa

kabla ya kuridhiwa kwa mkataba huo na Bunge, Waziri wa Sekta atawasiliana na Waziri kuhusu hoja kuu ya mkataba kwa nia ya kutathmini uwezekano wa athari kwa mazingira.

(3) Waziri atatengeneza utaratibu wa kufanya kazi karibu na jumuiya za kimataifa na kikanda ili kuchangia kuwepo kwa mazingira yenye utulivu, siha duniani kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

(4) Mkurugenzi wa Mazingira atatunza kumbukumbu za mikataba yote ya kimataifa inayohusu usimamizi wa mazingira ambayo Jamhuri ya Muungano ni mwanachama.

**Programu za usimamizi wa mazingira mtambuko kati ya nchi jirani**

180 (1) Kwa kushauriana na Wizara husika, Waziri anaweza kuanzisha mazungumzo na mamlaka husika za nchi jirani kuhusu programu za usimamizi wa mazingira na hatua za kuchukua ili kuepuka na kupunguza athari za mazingira.
(2) Kwa kushirikiana na Wizara za kisekta au Wakala wa Serikali, Mkurugenzi wa Mazingira ataanzisha na kutekeleza programu za usimamizi wa mazingira kwa nchi jirani.

**Kuanzishwa kwa ofisi za kitaifa na viungo**

181 Bila kuathiri masharti yaliyotangulia kwenye sehemu hii, Mkurugenzi wa Mazingira anaweza kuanzisha ofisi ya kitaifa au kiungo cha utekelezaji wa mikataba ya kimataifa kuhusu mazingira.

## SEHEMU YA XVI

## UZINGATIAJI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA

**Uteuzi wa wakaguzi wa mazingira**

182 (1) Waziri atateua wakaguzi wa mazingira kutoka miongoni mwa watumishi wa Baraza.

(2) Waziri anaweza kumteua kwa maandishi mtumishi yeyote wa mamlaka ya serikali za mitaa, wizara au asasi yoyote ya umma kwa jina au wadhifa wake kuwa mkaguzi wa mazingira kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii.

(3) Mkurugenzi wa Mashitaka anaweza kumteua mkaguzi wa mazingira kuwa mwendesha mashitaka baada ya kupendekezwa na Waziri.

**Madaraka ya wakaguzi wa mazingira**

183 (1) Mkaguzi wa mazingira aliyeteuliwa au kupewa wadhifa huo anaweza, kwa kutumia au bila kutumia hati, wakati wowote unaofaa, na kwa msaada wowote wa lazima-

(a) kuingia kwenye jengo lolote, ndani ya gari, ndege, chombo cha majini, ardhi, majini au mahali pengine pasipo kuwa na makazi ya kawaida ya watu;

(b) kusimamisha gari au chombo chochote cha majini au ardhini ambacho anaamini kwa dhati kuwa chombo hicho kinaendeshwa -

(i) kwa kukiuka Sheria hii; na

(ii) kinamwaga au kimekwishamwaga kitu chochote kinachochafua mazingira kinyume cha Sheria hii;

(c) kuchukua sampuli;

(d) kupiga picha za kawaida na video;

(e) kuandika kumbukumbu au kutoa nakala za taarifa kwa kutumia mbinu yoyote;

(f) kuhitaji waraka wowote, kumbukumbu au kitu kingine kinachotakiwa kutunzwa kwa mujibu wa Sheria hii, na waraka mwingine wowote unaohusiana na madhumuni ya ukaguzi kwa ajili ya kutoa nakala ua kuchukua sehemu ya waraka huo, ili mradi hakuna kitakachotolewa bila stakabadhi;

(g) kukagua, kukamata na kuchukua nakala za nyaraka zozote ambazo zinaweza kutumika kwa ushahidi kwa mujibu wa Sheria hii;

(h) kufanya uchunguzi wa makini kwa mdomo au kwa maandishi dhidi ya mtu yeyote;

(i) kukamata chombo chochote cha majini , gari, ndege au mtambo wowote ambao Mkaguzi anazo sababu za msigi za kuamini kwamba chombo hicho kimetumiwa katika kutenda kosa chini ya Sheria hii;

(j) kuagiza kuondolewa kwa taka zozote au kitu chochote kilichowekwa au kumwagwa kinyume na Sheria hii.

(2) Wakati akitekeleza masharti ya kifungu cha (1), mkaguzi wa mazingira ataonyesha kitambulisho chake cha kazi iwapo ataombwa na mkazi yeyote kufanya hivyo, na ataeleza sababu ya kufanya ukaguzi huo.

(3) Mtu yeyote atakayetakiwa na mkaguzi wa mazingira wakati akitekeleza masharti ya kifungu cha (1), kwa haraka anapaswa kukubaliana na matakwa ya mkaguzi huyo.

**Makosa yanayohusiana na Tathmini ya Athari kwa Mazingira**

184 Mtu yeyote ambaye:-

(a) atashindwa kuwasilisha muhtasari wa mradi kwa kukiuka masharti ya fungu la 86 (1);

(b) atashindwa kuandaa taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kama inavyotakiwa kwa mujibu wa sharti lolote la Sheria hii; au

(c) kwa kukusudia atatoa maelezo ya uongo kuhusu taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira iliyowasilishwa kwa mujibu wa Sheria hii, atakuwa ametenda kosa, na iwapo atapatikana na hatia, atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni kumi, au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka saba jela au vyote.

**Makosa yanayohusiana na kumbukumbu**

185 Mtu yeyote ambaye;

(a) atashindwa kutunza kumbukumbu zinazohusu shughuli, bidhaa, mazao ziada na taka kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) kwa makusudi, atabadilisha taarifa zozote zinazotakiwa kwa mujibu wa Sheria hii, atakuwa ametenda kosa, na iwapo atapatikana na hatia, atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka saba jela au vyote viwili.

**Makosa yanayohusiana na viwango vya mazingira**

186 Mtu yeyote ambaye;

(a) atakiuka viwango au miongozo yoyote ya mazingira ambayo haina adhabu iliyobainishwa mahususi; au

(b) atakiuka sharti lililobainishwa kwenye Sheria hii na ambalo halina adhabu iliyoelezwa mahsusi atakuwa ametenda kosa, na iwapo atapatikana na hatia, atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka saba jela au vyote viwili.

**Makosa yanayohusu uchafuzi wa mazingira**

187- (1) Mtu yeyote ambaye:-

(a) atamwaga vitu vyovyote vya hatari, mafuta, michanganyiko ya mafuta kwenye ardhi, maji, hewa au mazingira oevu kinyume na masharti ya Sheria hii;

(b) atachafua mazingira kinyume na masharti ya Sheria hii; au

(c) atamwaga kichafuzi chochote cha mazingira kinyume na masharti ya Sheria hii,

atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni tatu na isiyozidi shilingi milioni hamsini au kifungo kisichozidi miaka kumi na miwili jela au vyote viwili.

(2) Pamoja na adhabu yoyote ambayo mahakama inaweza kutoa kwa mtu aliyetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu cha (1), Mahakama inaweza kumwamuru mtu huyo-

(a) kulipa gharama zote za kusafisha mazingira yaliyochafuliwa na kuondoa uchafu; au

(b) kusafisha mazingira yaliyochafuliwa na kuondoa madhara ya uchafuzi kadiri Baraza litakavyoridhika.

(3) Bila ya kuathiri vifungu vya (1) na (2), mahakama inaweza kumwamuru mchafuzi wa mazingira kugharimia uharibifu au madhara ya uchafuzi huo kwa watu wengine kwa kulipa fidia ya kutosha, urejeshwaji au uakarabati.

**Makosa yanayohusu bioanuwai**

188 Mtu yeyote ambaye-

(a) anafanya biashara;

(b) anamiliki;

(c) anaghasi makazi,

ya sehemu ya bioanuwai kwa kukiuka miongozo na hatua zilizobainishwa katika mafungu ya 66, 67 na 68 au masharti mengine chini ya Sheria hii, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka mitano jela au vyote viwili kwa pamoja.

**Makosa yanayohusu urejeshwaji, haki ya njia na kuhifadhi mazingira**

189 Mtu yeyote ambaye-

(a) atashindwa, atazembea au kukataa kutekeleza amri ya urejeshwaji wa mazingira katika hali ya awali kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) atashindwa, atazembea au kukataa kutekeleza amri ya haki ya njia chini ya Sheria hii; na

(c) atashindwa, atazembea au kukataa kuzingatia amri ya kuhifadhi mazingira iliyotolewa chini ya Sheria hii,

atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia, atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka mitano jela au vyote viwili.

**Makosa yanayohusu takataka**

190 (1) Mtu yeyote atakuwa anatenda kosa endapo, bila ya kuwa na sababu inayokubalika au uhalali-

(a) anatupa takataka yoyote ndani au juu ya eneo lolote linalotumiwa na umma; au

(b) anatupa takataka yoyote ndani au juu ya eneo la ardhi ya mtu binafsi bila ridhaa ya mwenye kumiliki eneo hilo; au

(c) anatupa takataka yoyote ndani au juu ya ardhi ya mtu binafsi ambaye si mkazi wa Tanzania bila kujali kwamba mtu huyo

ametoa ridhaa yake au la; au

(d) anatupa takataka yoyote isiyokuwa ya kikaboni ndani au juu ya ardhi yoyote mbali na ardhi iliyotengwa au kuidhinishwa kama eneo la kutupia taka;

(e) baada ya kutupa takataka yoyote iwe kwa bahati mbaya au vinginevyo ndani au juu ya eneo la umma, ama ndani au juu ya ardhi ya mtu binafsi bila ya ridhaa ya mmiliki wa ardhi hiyo, ataliacha jalala la taka pale hata baada ya kuombwa na Mkaguzi wa Mazingira kuliondoa; au

(f) anakataa au anashindwa kutekeleza kifungu 121; au

(g) anakataa au anashindwa kutekeleza kifungu 122; au

(h) anakataa au anashindwa kutekeleza notisi iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu 122 au anakataa au anashindwa kutekeleza uamuzi wa mamlaka inayotoa kibali kwa mujibu wa kifungu hicho,

na iwapo atapatikana na hatia, akiwa mtu binafsi, atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni moja, na ikiwa ni asasi au shirika litatozwa faini isiyozidi shilingi milioni tano.

(2) Pale ambapo mtu atatiwa hatiani kwa kukiuka kifungu hiki licha ya adhabu iliyotolewa, mahakama itamwamuru mkosaji chini ya usimamizi na kwa kuridhika kwa mtu aliyeteuliwa na mahakama, kusafisha na kuondoa takataka zilizotupwa kwa muda na mahali kama itakavyobainishwa katika amri, na katika kutoa amri hiyo, mahakama itaagiza pia kwamba iwapo mkosaji atashindwa kuzingatia amri hiyo atapewa adhabu zaidi ya kulipa faini isiyozidi shilingi laki tano.

(3) Pale ambapo mahakama itamtia hatiani mtu kwa kosa la kukiuka kifungu hiki, mahakama inaweza, ikiona inafaa, zaidi ya kutoa adhabu itamwamuru mkosaji kulipa fidia kwa mamlaka ya umma yenye dhamana ya udhibiti au usimamizi wa eneo hilo la umma, ama kama itakavyokuwa, kwa mmiliki wa ardhi binafsi ambapo kosa lilitendwa, kiasi cha fedha ambacho mahakama itaona kinafaa kulipia gharama ya kuondoa takataka, na kiwango kitakachotolewa na mahakama, kitachukuliwa kuwa ni deni la hukumu litakalolipwa na mkosaji kwa mamlaka au mmiliki, na linaweza kukaziwa kwa utaratibu wowote ambao unatumika kutekeleza hukumu au amri za kawaida za mahakama kuhusu malipo kwenye mashauri ya madai.

**Adhabu za jumla** 191 Mtu yeyote anayetenda kosa kwa kukiuka kifungu chochote cha Sheria hii, na ambacho hakina adhabu iliyobainishwa, akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini elfu na isiyozidi shilingi milioni hamsini, au kifungo kisichopungua miezi mitatu au

kisicho zidi miaka saba jela ama vyote viwili.

**Makosa ya madai** 192 (1) Kutiwa hatiani kwa kosa lililotendwa kinyume na Sheria hii, hakutazuia mtu au asasi yoyote isifunguliwe kesi ya madai ambayo inaweza kufunguliwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Mtu hatachukuliwa kuwa ametenda kosa kinyume na kifungu (1) ikiwa mtu huyo atathibitisha kwamba alitenda kosa hilo bila kujua au kwa kurubuniwa na kwamba alifanya kila alivyoweza kujizuia kutendeka kosa hilo kwa kuzingatia kila hali.

**Kuchukuliwa, kufutwa kazi za jumuia na amri nyingine** 193 (1) Mahakama ambayo mtu ameshitakiwa kwa kukiuka Sheria hii au kanuni yoyote iliyotungwa chini ya Sheria hii inaweza kuamuru, licha ya amri nyingine, kwamba-

(a) baada ya mshitakiwa kutiwa hatiani; au
(b) iwapo imeridhika kwamba kosa limetendwa bila ya kujali kuwa hakuna mtu aliyetiwa hatiani kwa kosa hilo,

inaweza pia kuamuru kwamba vitu, vifaa na zana vilivyotumika kutenda kosa zichukuliwe na Serikali na vitolewe kwa utaratibu ambao mahakama itaamua.

(2) Wakati wa kutoa amri kwa mujibu wa kifungu (1), mahakama inaweza kuamuru pia gharama ya kutolewa kwa vitu, vifaa au zana zilizotajwa kwenye kifungu cha (1), zilipwe na mshitakiwa.

(3) Mahakama inaweza pia kuamuru leseni, kibali au idhini yoyote iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria hii na ambayo inahusiana na kosa ifutwe.

(4) Licha ya faini iliyotolewa na mahakama, mahakama inaweza kuamuru mshitakiwa kufanya kazi za jumuiya, ambazo zitakuza hifadhi ya mazingira.

(5) Bila ya kuathiri ujumla wa fungu hili, mahakama inaweza kutoa amri ya urejeshwaji wa mazingira dhidi ya mshtakiwa kwa mujibu wa Sheria hii, kanuni, miongozo au viwango vilivyowekwa na Sheria hii.

**Kuafikiana kwenye makosa** 194 (1) Mkurugenzi Mkuu au mkaguzi wa mazingira, kwa kuzingatia Sheria hii, iwapo hali inaonyesha kwamba mtu au asasi iliyosajiliwa au isiyosajiliwa imetenda kosa kinyume na Sheria hii, na mtu au asasi hiyo imekiri kutenda kosa hilo na kukubali kulipa faini, Mkurugenzi Mkuu au mkaguzi wa mazingira anaweza kupokea kiasi cha fedha pamoja na zana, kifaa, gari au kitu kingine kama kipo ambacho kimetukima kutenda kosa hilo.

(2) Kwa kuzingatia mafungu ya Sheria hii yanayoidhinisha

kuchukuliwa kwa hatua yoyote licha ya faini ambayo imetolewa kwa mujibu wa amri ya Baraza la Rufaa la Mazingira au mahakama, hakuna shauri lolote la jinai au, kwa kadiri itakavyokuwa, shauri la madai litakalofunguliwa dhidi ya mtu ambaye amelipa faini kwa utaratibu wa maafikiano.

**Amri ya kizuizi ili kulinda mazingira**

195 (1) Iwapo Baraza lina sababu za msingi kuamini kwamba mtu anafanya au atafanya shughuli, au anamiliki au atamiliki ama kudhibiti kitu chochote kinachoweza kuwa na madhara makubwa kwa mazingira au afya za watu, linaweza kutoa amri ya kizuizi kwa mtu huyo.

(2) Amri ya kizuizi inaweza kumwamuru mtu huyo-

(a) kuandaa mpango wa dharura kwa maandishi unaoweza kupunguza au kuondoa madhara hayo;

(b) kuwasilisha nakala ya mpango huo kwa Baraza;

(c) kuwa na vifaa, suhula muhimu na wafanyakazi wenye ujuzi wa kukabili madhara hayo;

(d) kuutekeleza mpango huo, mara baada ya kutokea tukio au hali iliyogunduliwa; na

(e) kuchukua hatua nyingine zozote ambazo ni za lazima kuhakikisha kwamba dharura yoyote inakabiliwa kwa ufanisi.

(3) Mtu yeyote aliyepewa amri ya kizuizi atapaswa kutimiza masharti ya amri hiyo kwa tarehe iliyotajwa kwenye amri na kama hakuna tarehe iliyotajwa, mtu huyo atapaswa kutimiza amri hiyo mara moja.

(4) Mtu anayekiuka kifungu (3) atakuwa ametenda kosa, na iwapo atapatikana na hatia, atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi mwaka mmoja jela, na iwapo mtu huyo atashindwa kuzingatia masharti yaliyobainishwa kwenye amri ndani ya muda uliowekwa, mtu huyo atatozwa faini ya ziada isiyopungua shilingi laki moja kila siku au sehemu ya siku baada ya tarehe iliyotajwa kwenye amri wakati ambao kosa lilikuwa likiendelea.

(5) Mtu yeyote aliyepewa amri ya kizuizi anaweza kupeleka maombi ya mapitio ya amri hiyo kwa Waziri kwa utaratibu uliowekwa na Waziri.

**Amri ya kizuizi kwa shughuli zenye madhara makubwa kwa mazingira**

196 (1) Iwapo Baraza lina sababu za msingi kuamini kwamba shughuli inasababisha au inaweza kusababisha madhara makubwa kwa mazingira au afya za watu, linaweza kutoa amri ya kizuizi kwa-

(a) mmiliki, meneja au mtu mwenye kudhibiti eneo husika, gari, chombo cha majini, ndege au zana ambapo shughuli hiyo inafanyika au itafanyika;

(b) mtu yeyote aliyesababisha au aliyeruhusu shughuli hiyo kufanyika.

(2) Amri ya kizuizi inaweza kumwamuru mtu aliyepewa kuchukua hatua yoyote ambayo itasaidia kuepuka, kurekebisha au kupunguza madhara makubwa, na bila kuwa na ukomo kwa ujumla wa kifungu (1),kuchukua hatua yoyote ili-

(a) kukomesha shughuli ambayo inasababisha au inaweza kusababisha madhara makubwa;

(b) kudhibiti shughuli hiyo;

(c) kutathimini ukubwa wa athari uliopo au unaotarajiwa;

(d) kurekebisha madhara yaliyosababishwa na shughuli; au

(e) kuzuia marudio ya shughuli hiyo au madhara hayo.

(3) Mtu yeyote aliyepewa amri ya kizuizi atapaswa kutimiza mashati ya amri hiyo kwa tarehe iliyotajwa kwenye amri na kama hakuna tarehe iliyotajwa, mtu huyo atapaswa kutimiza amri hiyo mara moja.

(4) Mtu anayekiuka kifungu (3) atakuwa ametenda kosa, na iwapo atapatikana na hatia, atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi mwaka mmoja jela, na iwapo mtu huyo atashindwa kutimiza masharti yaliyobainishwa kwenye amri ndani ya muda uliowekwa, mtu huyo atatozwa faini ya ziada isiyopungua shilingi laki moja kila siku au sehemu ya siku baada ya tarehe iliyotajwa kwenye amri wakati ambao kosa lilikuwa likiendelea.

(5) Mtu yeyote aliyepewa amri ya kizuizi, anaweza kupeleka maombi ya mapitio ya amri hiyo kwa Waziri kwa utaratibu uliowekwa na Waziri.

**Amri ya dharura ya kulinda mazingira**

197 (1) Mkaguzi yeyote wa mazingira anayeona umwagaji wa vichafuzi kwenye mazingira kwa kiasi, mrundikano au namna ambayo haina madhara kwa afya au mali ya binadamu, au inasababisha au inaweza kusababisha madhara makubwa kwa mazingira au afya za watu, anaweza kutoa amri ya kizuizi kwa-.

(a) mmiliki, meneja au mtu mwenye kudhibiti eneo husika, gari, chombo cha majini, ndege au zana ambapo umwagaji huo ulifanyika au unafanyika;

(b) mtu yeyote ambaye wakati uvujaji unatokea alikuwa ndiye mmiliki, meneja au mtu mwenye kudhibiti eneo husika, gari, chombo cha majini, ndege au zana ambapo umwagaji ulifanywa;au

(c) mtu yeyote aliyesababisha au aliyeruhusu umwagaji huo.

(2) Amri ya dharura ya ulinzi wa mazingira inaweza kumwamuru mtu aliyepewa kuchukua hatua yoyote ambayo itasaidia kupunguza au kuondoa hatari au madhara na bila kuwa na ukomo kwa ujumla wa kifungu kilichotajwa awali, kuchukua hatua yoyote ili-

(a) kukomesha umwagaji;

(b) kudhibiti umwagaji;

(c) kusafisha au kuondoa uchafu au vitu vingine kutoka mahali popote;

(d) kuzuia marudio ya umwagaji huo.

(3) Mtu yeyote aliyepewa amri ya dharura ya ulinzi wa mazingira atapaswa kutimiza masharti ya amri hiyo kwa tarehe iliyotajwa kwenye amri na kama hakuna tarehe iliyotajwa,mtu huyo atapaswa kutimiza amri hiyo mara moja .

(4) Mtu anayekiuka kifungu (3) atakuwa ametenda kosa, na iwapo atapatikana na hatia, atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi mwaka mmoja jela, na iwapo mtu huyo atashindwa kutimiza masharti yaliyobainishwa kwenye amri ndani ya muda uliowekwa, mtu huyo atatozwa faini ya ziada isiyopungua shilingi laki moja kila siku au sehemu ya siku baada ya tarehe iliyotajwa kwenye amri wakati ambao kosa lilikuwa likiendelea.

(5) Mtu yeyote aliyepewa amri ya dharura ya ulinzi wa mazingira, anaweza kupeleka maombi ya mapitio ya amri hiyo kwa Waziri kwa utaratibu uliowekwa na Waziri.

**Amri ya kutimiza masharti ya mazingira**

198 (1) Iwapo Baraza lina sabababu ya kuamini kwamba sharti lolote la leseni iliyotolewa kuendesha shughuli yoyote limekiukwa, Baraza linaweza kumpa mmiliki wa leseni hiyo amri ya kutimiza masharti ya leseni hiyo, inayomwamuru mtu huyo kurekebisha ukiukwaji huo kwa muda uliowekwa kwenye amri na iwapo marekebisho hayakufanyika, Baraza linaweza kuishauri mamlaka ya utoaji wa leseni kuifuta leseni hiyo.

(2)Amri ya utekelezaji inaweza-

(a) kusitisha mara moja kwa muda leseni au vinginevyo kama Baraza litakavyoona inafaa kwa madhumuni ya kuzuia au kupunguza hatari inayoweza kutokea yenye madhara makubwa kwa mazingira au kwa afya ya binadamu; na

(b) kumwamuru mmiliki wa leseni kuchukua hatua zilizobainishwa ili

kuzuia au kuepuka madhara hayo.

(3) Iwapo mmiliki wa leseni atashindwa kutimiza amri iliyotolewa, Baraza linaweza-

(a) kuchukua hatua muhimu ili kurekebisha ukiukwaji na kulipa gharama kutoka kwa mmiliki wa leseni;
(b) kuishauri mamlaka husika kubadili masharti ya leseni;au
(c) kusababisha leseni hiyo ifutwe.

(4) Mtu yeyote aliyepewa amri ya kutimiza masharti ya mazingira atapaswa kutekeleza masharti ya amri hiyo kwa tarehe iliyotajwa kwenye amri na kama hakuna tarehe iliyotajwa, mtu huyo atapaswa kutimiza amri hiyo mara moja.

(5) Mtu anayekiuka kifungu (4) atakuwa ametenda kosa, na iwapo atapatikana na hatia, atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi mwaka mmoja jela, na iwapo mtu huyo atashindwa kutimiza masharti yaliyobainishwa kwenye amri ndani ya muda uliowekwa, mtu huyo atatozwa faini ya ziada isiyopungua shilingi laki moja kila siku au sehemu ya siku baada ya tarehe iliyotajwa kwenye amri wakati ambao kosa lilikuwa likiendelea.

(6) Mtu yeyote aliyepewa amri ya kutekeleza masharti ya mazingira, anaweza kupeleka maombi ya mapitio ya amri hiyo kwa Waziri kwa utaratibu uliowekwa na Waziri.

**Amri ya gharama**

199 (1) Iwapo mtu yeyote atashindwa kutimiza sharti lolote kwa mujibu wa Sehemu hii, Baraza linaweza kuamuru kuchukuliwa hatua zinazofaa, na kutoa amri ya gharama inayomtaka mtu huyo kulifidia Baraza kwa hatua zilizochukuliwa.

(2) Mtu yeyote aliyepewa amri ya gharama, katika kipindi cha siku thelathini baada ya kupokea amri hiyo, anaweza kupeleka maombi kwa Waziri ili afanye mapitio ya amri hiyo kwa kuzingatia taratibu zilizobainishwa.

(3) Iwapo hakuna maombi ya mapitio ya amri ya gharama yaliyowasilishwa ndani ya muda uliobainishwa kwenye kifungu cha (2), amri hiyo ya gharama inaweza kutekelezwa kama amri iliyotolewa na mahakama.

**Makosa yanayohusu Wakaguzi wa Mazingira**

200 Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote-

(a) kumzuia mkaguzi wa mazingira kutekelezaji wajibu wake kwa mujbu wa Sheria hii;
(b) kushindwa kutimiza amri au masharti halali yaliyotolewa na mkaguzi wa mazingira kwa mujibu wa Sheria hii;

(c) kumkataza mkaguzi wa mazingira kuingia kwenye ardhi au eneo lolote ambalo ana madaraka ya kuingia kwa mujibu wa Sheria hii;
(d) kujifanya kuwa mkaguzi wa mazingira;
(e) kumzuia mkaguzi wa mazingira kupata kumbukumbu zilizotunzwa kwa mujibu wa Sheria hii;
(f) kushindwa kutaja jina lake au kudanganya jina au anwani yake kwa mkaguzi wa mazingira wakati akitekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria hii; au
(g) kupotosha au kutoa taarifa za uongo kwa mkaguzi wa mazingira kinyume cha Sheria hii,

iwapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miaka saba jela au vyote viwili kwa pamoja.

**Makosa yanayohusu watendaji wakuu wa asasi na mashirika**

201 (1) Iwapo shirika litatenda kosa kinyume cha Sheria hii, kila Mkurugenzi au mshirika, au mtu yeyote anayehusika katika usimamizi wa asasi au shirika hilo, atakuwa ametenda kosa, isipokuwa tu pale mtu huyo atakapothibitisha kwamba-
(a) kosa lilifanyika bila ya ridhaa yake au kwa kurubuniwa; na
(b) mtu huyo alifanya kila aliloweza ili kuzuia kufanyika kwa kosa hilo kama ilivyotazamiwa afanye kwa kuzingatia hali halisi ya wajibu na mazingira yote.

(2) Kila mkurugenzi au mshirika ama mtu mwingine yeyote anayehusika katika usimamizi wa asasi au shirika lililopewa leseni au amri kwa mujibu wa Sheria hii, anapaswa kuchukua hatua zote muhimu ili kuzuia Asasi au Shirika hilo lisikiuke masharti ya leseni au amri.

(3) Mtu anayekiuka kifungu cha (2), atakuwa ametenda kosa, na iwapo atapatikana na hatia, atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi mwaka mmoja jela au vyote viwili.

**Haki ya kushitaki ya mtu binafsi na asasi au shirika**

202 Mtu binafsi au mashirika kisheria yanaweza kushtaki au kuomba nafuu inayostahili kuhusu ukiukaji, uvunjaji au kutishia ukiukaji ama uvunjaji wa fungu lolote la Sheria hii au unaohusu matumizi ya vifaa, vitu, au maliasili kwa-
(a) maslahi binafsi ya mtu au asasi hiyo;
(b) maslahi au kwa niaba ya mtu ambaye kwa sababu za kimsingi yeye hawezi kushitaki;
(c) maslahi au kwa niaba ya kikundi au kundi la watu ambao maslahi yao yameathiriwa;
(d) maslahi ya umma;na
(e) maslahi ya mazingira au makazi mengine.

**Utetezi** 203 (1) Isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo katika Sheria hii, utakuwa utetezi kwa mtu aliyeshitakiwa iwapo atathibitisha kuwa alichukua kila hadhari inayostahili na kufanya kila aliloweza kuzuia kutendeka kwa kosa kama ambavyo ingeweza kufanywa na mtu kwa kuzingatia hali zote.

(2) Haitakuwa utetezi wa shitaka kwa mujibu wa Sheria hii, iwapo mshitakiwa alishindwa kutimiza amri yoyote au kufanya kitendo ama shughuli yoyote au kuacha kufanya jambo na mtu mwingine ambalo lilisababisha kukiukwa kwa Sheria hii.

## SEHEMU YA XVII
## BARAZA LA RUFAA LA MAZINGIRA

**Kuanzishwa Baraza la Rufaa na wajumbe wake** 204 (1) Litaanzishwa Baraza la Rufaa la Mazingira ambalo litakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa za kuweza kuteuliwa kuwa Jaji;
(b) Wakili mmoja wa Mahakama Kuu ya Tanzania aliyependekezwa na Chama cha Wanasheria cha Tanganyika;
(c) Mjumbe mmoja mwenye sifa za juu kitaaluma na ujuzi wa sheria za mazingira; na
(d) Wajumbe wengine wawili wenye umilisi katika masuala ya mazingira.

(2) Wajumbe waliotajwa kwenye aya (b), (c) na (d) watateuliwa na Waziri.

(3) Mwenyekiti na Wajumbe wengine watashika madaraka kwa muda wa miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

(4) Uteuzi wa wajumbe wa Baraza la Rufaa utafanyika kwa nyakati tofauti ili kuhakikisha kuwa tarehe za ukomo wa uteuzi wao wa kushika madaraka unatofautiana.

(5) Mwenyekiti wa Baraza la Rufaa anaweza kuwaalika watu wenye stadi au ujuzi maalumu wa masuala ya mazingira ambayo yanajadiliwa au kuchunguzwa na Baraza la Rufaa ili kuwa kama washauri wa Baraza pale Baraza la Rufaa litakapohitaji stadi au ujuzi mahsusi unaohitajika kwa ajili ya kutolea uamuzi.

**Vyanzo vya fedha vya Baraza la Rufaa** 205 Vyanzo vya fedha za Baraza la Rufaa vitahusisha-

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Bunge; na

(b) fedha zitakazotolewa na Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira .

**Mamlaka ya Baraza la Rufaa**

206 (1) Baraza la Rufaa litatekeleza wajibu wa kusikiliza rufaa kwa mujibu wa Sheria hii kuhusu masuala yaliyoletwa mbele yake kwa mujibu wa kifungu cha (2).

(2) Mtu yeyote ambaye hataridhika na-

(a) uamuzi wowote wa Waziri ;

(b) kuwekwa au kushindwa kuwekwa kwa shuruti yoyote, ukomo au kizuizi kinachotolewa chuni ya Sheria hiiau kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii; na

(c) uamuzi wa Waziri wa kuidhinisha au kutoidhinisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira,

anaweza, katika muda wa siku thelathini toka siku ya tukio ambalo haridhiki nalo, kukata rufaa kwenye Baraza la Rufaa kwa utaratibu uliowekwa na Baraza husika.

(3) Baada ya kusikiliza rufaa, Baraza la Rufaa linaweza-

(a) kuridhia, kubadili au kuondoa amri, notisi, agizo au uamuzi unaolalamikiwa; au

(b) kutoa amri nyingine yoyote na kwa gharama ambazo litaona zinafaa.

(4) Iwapo rufaa itakuwa imekubaliwa, Baraza la Rufaa linaweza kutoa amri yoyote ambayo litaona ni ya lazima kulingana na shauri lililoletwa kwenye rufaa.

(5) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha (2) Baraza la Mazingira pale linapoona kwamba suala linalohusu fasili ya Sheria hii na ambalo halina ubishi au haliwezi kuleta mgongano baadaye, linaweza kuwasilisha suala hilo kwenye Baraza la Rufaa kwa maelekezo.

**Uendeshaji wa Baraza la Rufaa**

207 (1) Akidi ya kikao itatimizwa na Mwenyekiti na wajumbe wengine wawili wa Baraza la Rufaa.

(2) Mwenyekiti ataendesha vikao vyote vya Baraza la Rufaa, na asipokuwepo, mjumbe yeyote atakayechaguliwa na wajumbe waliopo, ataendesha kikao hicho.

(3) Mjumbe wa Baraza la Rufaa ambaye atakuwa na maslahi binafsi kwenye shauri linalosikilizwa katika kikao cha Baraza la Rufaa, hatoshiriki katika uendeshaji wa shauri hilo.

**Sheria Na. 49 ya 1966, Na. 7 ya 1967 na Na. 9 ya 1985**

(4) Baraza la Rufaa litajiwekea utaratibu wa kuendesha mashauri yake na halitalazimika kufuata taratibu za kisheria au ushahidi kama zilivyo katika Sheria ya Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai ya mwaka 1985, Kanuni za Taratibu za Mashauri ya Madai ya mwaka 1966 na Sheria ya Ushahidi ya mwaka 1967.

(5) Mtu yeyote anayehusika kwenye shauri lililoko mbele ya Baraza la Rufaa anaweza kuhudhuria yeye mwenye au kuwakilishwa na wakili ama mwakilishi anayetambulika kisheria.

(6) Baraza la Rufaa kwa utaratibu wa uendeshaji lililojiwekea linaweza:-

(a) kumwamuru mtu yeyote ahudhurie kikao cha Baraza la Rufaa mahali popote pale;
(b) kuamuru kuletwa kwenye Baraza la Rufaa waraka wowote unaohusu shauri lililo mbele yake au uchunguzi unaohusu ukiukwaji wa Sheria hii kadiri litakavyoona ni lazima au inafaa;
(c) kuchukua ushahidi wa kiapo, na kwa madhumuni hayo, linaweza kusimamia viapo; na
(d) kwa utashi wake au kwa kuombwa, kumuita mtu yeyote kutoa ushahidi.

(7) Mtu yeyote ambaye-

(a) atashindwa kuhudhuria kwenye Baraza la Rufaa baada ya kutakiwa kufanya hivyo;
(b) atakataa kuapishwa na Baraza la Rufaa au atakataa kutoa kitu au waraka wowote anapotakiwa kufanya hivyo kisheria;
(c) atatoa ushahidi au taarifa ya uongo kwa makusudi ambayo italipotosha Baraza la Rufaa; na
(d) ataingilia uendeshaji wa kikao chochote cha Baraza la Rufaa au atatenda kosa lolote la kudharau Baraza la Rufaa,

atakuwa ametenda kosa kinyume cha Sheria hii.

**Maamuzi ya Baraza la Rufaa**

208 (1) Baraza la Rufaa, baada ya kusikiliza rufaa au shauri lolote lililowasilishwa mbele yake, Baraza -

(a) litachunguza shauri hilo na litatoa uamuzi kwa utaratibu wa agizo, amri au mapendekezo;
(b) litaziarifu pande husika kuhusu uamuzi wake; na
(c) litataja muda ambamo maamuzi yaliyotolewa itapaswa yawe yametekelezwa.

(2) Maamuzi ya Baraza la Rufaa yatakuwa na nguvu ya kisheria na yanaweza kukaziwa sawa na amri za mahakama.

**Kutaka rufaa Mahakama Kuu**

209 (1) Yeyote kati ya pande husika ambaye hajaridhishwa na uamuzi au amri yoyote ya Baraza la Rufaa iliyotolewa kwa mujibu wa sheria, anaweza kukata rufaa Mahakama Kuu katika kipindi cha siku thelathini tangu siku ambayo uamuzi au amri hiyo ilipotolewa.

(2) Kila rufaa iliyopelekwa Mahakama Kuu itasikilizwa na kuamuliwa na jopo la majaji watatu.

(3) Uamuzi wa Mahakama Kuu kuhusu rufaa yoyote kwa mujibu wa fungu hili ni wa mwisho.

**Kinga ya kisheria kwa wajumbe wa Baraza la Rufaa**

210 (1) Mwenyekiti au wajumbe wengine ama maofisa wa Baraza la Rufaa hawatahusishwa wala kushitakiwa katika mahakama yoyote kwa kitendo chochote walichofanya au walichoacha kufanya kwa nia njema wakati wakitekeleza majukumu yao kama wajumbe ama maofisa wa Baraza la Rufaa, bila kujali mipaka ya mamlaka yao.

(2) Hakuna ofisa au mtumishi mwingine wa Baraza la Rufaa mwenye mamlaka ya kutoa hati halali, amri, au nyaraka nyingine za mahakama ambaye atawajibishwa au kushitakiwa kwenye mahakama yoyote kwa kutekeleza agizo lililoko kwenye hati, amri au shughuli ambayo angepaswa aitekeleze kwa mujibu wa mipaka ya mamlaka ya Baraza la Rufaa.

**Malipo ya wajumbe wa Baraza la Rufaa la Mazingira**

211 Mwenyekiti na Wajumbe wa Baraza la Rufaa watapewa malipo na posho kama itakavyoelekezwa na Waziri.

**Uteuzi wa Msajili**

212 (1) Jaji Mkuu atamteua ofisa yeyote wa mahakama kuwa Msajili wa Baraza la Rufaa.

(2) Msajili atatekeleza majukumu kama atakavyopewa na Mwenyekiti kwa mujibu wa shughuli za Baraza la Rufaa.

## SEHEMU YA XVIII

## MFUKO WA TAIFA WA DHAMANA YA HIFADHI YA MAZINGIRA

**Kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira**

213 (1) Kutaanzishwa Mfuko ambao utajulikana kama Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira ambamo kutaingizwa fedha zote zitakazopokewa na Mfuko.

(2) Vyanzo vya mapato yatakayoingia kwenye Mfuko huo vitakuwa-

(a) kiasi cha fedha ambacho Bunge linaweza kuidhinisha;

(b) kiasi cha fedha ambacho chaweza kulipwa kwenye Mfuko kwa njia ya msaada, zawadi, mikopo au ruzuku toka Serikalini, wakala, watu binafsi au Serikali nyingine au mashirika ya kimataifa;

(c) kiasi kingine cha mali ambacho kwa namna yoyote chaweza

kulipwa au kuwekwa kwenye Mfuko kutokana na suala lolote lililo chini ya mamlaka na majukumu ya mfuko;

(d) mapato yoyote yaliyozalishwa kutoka kwenye mradi wowote unaofadhiliwa na Mfuko ambapo gharama zake muhimu zinaweza kulipwa kutoka kwenye mradi wowote ule; na

(e) kodi ambayo ukubwa wake utawekwa na Waziri kwenye kanuni kutoka kila tozo la ada iliyobainishwa chini ya Sheria hii.

(3) Kutatolewa malipo kutoka kwenye Mfuko, kiasi chochote cha fedha kitakachotumika kugharimia usimamizi wa mazingira na kazi za kiutawala.

**Madhumuni ya Mfuko**

214 (1) Madhumuni ya Mfuko yatakuwa ni-

(a) kuwezesha kufanyika utafiti unaolenga kuboresha mahitaji ya usimamizi wa mazingira;

(b) kuimarisha uwezo kiutendaji na kimiundombinu;

(c) kutoa tuzo za uhifadhi wa mazingira;

(d) kuchapisha majarida ya uhifadhi wa mazingira;

(e) kutoa ufadhili wa masomo ya ngazi za juu;

(f) kuboresha na kusaidia kupitia ruzuku programu za usimamizi wa mazingira za jumuia;

(g) kulipia gharama za mikutano ya Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira na Bodi ya Wadhamini; na

(h) Bodi ya Wadhamini, kwa pendekezo la Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira, inaweza kuamua kwamba, baadhi ya misaada iliyotolewa kwenye Mfuko itumike mahsusi kama zawadi na tuzo kwa washindi katika uhifadhi wa mazingira na kutumiwa na mshindi wa tuzo kwa kusimamia mazingira tu.

**Muundo na utawala wa Mfuko**

215 (1) Mfuko utakuwa chini ya Bodi ya Wadhamini na utasimamiwa kiutawala na Bodi yenyewe.

(2) Bodi ya Wadhamini itateuliwa na Waziri na itaundwa na watu wenye wasifu uliobainishwa kwenye Jedwali la Nne la Sheria hii.

(3) Mkurugenzi wa Mazingira atakuwa ndiye Ofisa Masuula wa Mfuko na kwa kuzingatia maelekezo yoyote mahsusi kutoka kwenye Bodi ya Wadhamini atasimamia Mfuko huo kwa mujibu wa taratibu za utunzaji wa fedha za umma.

**Hesabu za mwaka na ukaguzi wa hesabu za**

216 (1) Bodi ya Wadhamini itahakikisha kunawekwa na kutunzwa vitabu madhubuti vya utunzaji wa mahesabu na kumbukumbu kuhusu-

**Mfuko**

(a) mapato na matumizi ya fedha na mambo yote ya kifedha yanayofanywa na Mfuko;
(b) mali na madeni ya Mfuko na itahakikisha kwamba kila mwaka kunatolewa mizania ya mapato na matumizi na maelezo kwa kina kuhusu mapato na matumizi ya Mfuko pamoja na mali na madeni yote.

**Sheria Na. 6 ya mwaka 2001**

(2) Ndani ya miezi sita baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha, hesabu pamoja na mizania ya mapato na matumizi ya Mfuko kwa mwaka huo wa fedha vitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001.

(3) Mara baada ya hesabu za Mfuko kukaguliwa, na kwa vyovyote ikiwa si baada miezi sita baada ya ukaguzi huo kufanyika, Bodi ya Wadhamini itawasilisha kwa Waziri nakala ya taarifa ya hesabu zilizokaguliwa pamoja na nakala za maelekezo kutoka kwa Wakaguzi.

(4) Mapema kadiri itakavyowezekana baada ya kupokea nakala ya taarifa ya mahesabu na nakala ya maelezo yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kifungu cha (3), Waziri atawasilisha Bungeni nakala ya taarifa hiyo pamoja na nakala ya maelezo ya wakaguzi.

## SEHEMU YA XIX
## MASUALA YA FEDHA

**Vyanzo vya fedha vya Baraza**

217 Vyanzo vya fedha kwa Baraza vitakuwa ni-
(a) kiasi cha fedha ambacho Bunge linaweza kukiidhinisha;
(b) kiasi cha fedha ambacho kinaweza kupokewa na Baraza kama msaada, zawadi, ruzuku, mkopo au urithi;
(c) ada yoyote ambayo inaweza kutozwa na kulipwa kwa Baraza;
(d) mapato yoyote yanayotokana na mradi wowote unaofadhiliwa na Baraza baada ya kulipwa kwa gharama za mradi; na
(e) chanzo kingine chochote halali cha mapato.

**Akaunti ya Benki na utengaji wa fedha**

218 (1) Baraza litafungua na kuendesha akaunti moja au zaidi kwenye benki za biashara.

(2) Mapato yote na mali pamoja na makusanyo yote ya Baraza yaliyopatikana kwa mujibu wa fungu la 217 yatatumika katika kukidhi malengo ya Baraza.

**Uwezo wa Baraza wa**

219 (1) Kwa idhini ya Waziri wa Fedha, Bodi inaweza kukopa kutoka

**kukopa na kudhamini mikopo**

asasi yoyote kwa ajili ya matumizi ya Baraza kwa kuzingatia masharti ya ulipaji wa mikopo na riba.

(2) Bodi, kwa maslahi ya umma, na kwa idhini ya Waziri inaweza kujipatia fedha kwa kuweka rehani mali, tuzo, kwa kuzuiwa mali na mapato yake ya sasa au ya baadaye, au sehemu yake, na kwa kukabidhi hati za dhamana, hisa, hati madai, na kwa njia nyinginezo ambazo Bodi itaona zinafaa, au kudhamini ulipaji wa riba ya mkopo uliotolewa kwa mtu yeyote anayejihusisha na usimamizi wa mazingira nchini Tanzania.

**Vitegauchumi vya Baraza**

220 Bodi inaweza kuwekeza sehemu yoyote ya fedha ilizo nazo kwenye akaunti yoyote ya Baraza, iwapo fedha hizo hazihitajiki wakati huo kwa shughuli za Baraza.

**Bajeti ya mwaka na nyongeza yake**

221 (1) Katika muda si chini ya miezi miwili kabla ya mwanzo wa kila mwaka wa fedha, katika kikao cha Bodi itapitishwa bajeti kamilifu ambayo chini ya Sheria hii inatambulika kama "Bajeti ya Mwaka," itakayotaja kiasi cha fedha ambacho kinatarajiwa-

(a) kukusanywa; na
(b) kutumiwa,

na Baraza ndani ya mwaka huo wa fedha, na pale inapobidi Baraza linaweza kupitisha bajeti ya nyongeza ndani ya mwaka wowote wa fedha.

(2) Iwapo katika mwaka wowote wa fedha Baraza litahitaji kutumia fedha ambazo haziko kwenye bajeti, au kiasi cha fedha cha ziada nje ya bajeti ya mwaka wowote wa fedha, Bodi, kwenye kikao chake itapitisha bajeti ya nyongeza kwa kuitolea maelezo ya kina.

**Hesabu na ukaguzi wa fedha**

222 (1) Bodi itahakikisha kumeandaliwa na kutunzwa vitabu mahsusi vya kutunza hesabu na kumbukumbu za-

(a) mapato na matumizi ya Baraza, ikiwa ni pamoja na mambo mengine ya shughuli za kifedha; na
(b) mali na madeni ya Baraza na itahakikisha kuwa kila mwaka wa fedha inaandaliwa mizania ya mapato na matumizi ikieleza kwa kina mapato na matumizi ya Baraza pamoja na mali na madeni yake kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya utunzaji wa hesabu kwa mtindo wa makusanyo.

(2) Ndani ya miezi sita baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha, hesabu pamoja na mizania ya mapato na matumizi ya Baraza yatakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka

2001.

(3) Kila mizania iliyokaguliwa itapelekwa na kuwasilishwa kwenye kikao cha Bodi na kama itapitishwa na Bodi, itapewa hati ya uthibitisho kwamba imepitishwa.

(4) Mapema baada ya hesabu ya Baraza kukaguliwa na kwa vyovyote ikiwa si zaidi ya miezi sita tangu mwaka wa fedha upitie, Bodi itawasilisha kwa Waziri nakala ya taarifa ya hesabu ambazo yamekaguliwa pamoja na nakala ya maelezo ya wakaguzi kuhusu taarifa hiyo.

**Taarifa ya Mwaka** 223 (1) Baraza litahakikisha taarifa ya mwaka imeandaliwa na kuwasilishwa kwa Waziri ndani ya miezi sita baada ya kila mwaka wa fedha kupita ikiwa na maelezo ya kina kuhusu shughuli na uendeshaji wa Baraza kwa mwaka huo.

(2) Taarifa hiyo itaambatishwa na-

(a) nakala ya hesabu za Baraza zilizokaguliwa pamoja na taarifa ya Mkaguzi kuhusu hesabu hizo; na

(b) maelezo kuhusu utekelezaji wa maagizo yote yaliyotolewa na Waziri kwenye Baraza kwa mwaka husika, na taarifa nyingine kama Waziri atakavyoagiza.

(3) Baraza pia litawasilisha kwa Waziri taarifa zingine kuhusu mambo yake ya fedha kama Waziri atakavyohitaji kwa maandishi.

(4) Mara baada ya taarifa kuwasilishwa kwake, Waziri atawasilisha Bungeni hesabu za Baraza zilizokaguliwa pamoja na maelezo ya mkaguzi kuhusu hesabu na taarifa ya mwaka ya Baraza, kama vipo.

## SEHEMU XX
## MASHARTI YA JUMLA NA MASUALA YA MPITO

**Sheria hii kuifunga Serikali** 224 Isipokuwa tu kama itaelezwa mahsusi vinginevyo, Serikali itafungwa na masharti ya sheria hii, pamoja na kanuni na amri zilizotungwa au kutolewa chini ya Sheria hii.

**Haki ya kesi za madai** 225 Pamoja na mfumo wa Sheria hii au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge kuhusu usimamizi wa makosa, utaratibu wa kutiisha kwa njia ya kesi za madai utaendelea kutoa nafasi kwa watu walioathiriwa na ukiukwaji wa Sheria hii kuhusu kufidiwa na mkiukaji wa sheria hii kupitia kesi za madai.

.

**Fidia za aina mbalimbali kwa** 226 Ili kusimamia viwango na wajibu kuhusu mazingira , fidia mbali mbali kwa mtu aliyeathirika au anayeelekea kuathirika, zitajumuisha-

**mwathirika**

(a) katazo la muda au la kudumu la kimahakama ;
(b) amri mahsusi za utendaji;
(c) faini na adhabu;
(d) fidia;
(e) amri za urejeshwaji wa hali ya awali, kuhifadhi, kupitisha haki ya njia;
(f) amri za uzingatiaji;
(g) kifungo; na
(h) unafuu mwingine wowote kama itakavyoamuriwa na Baraza la Rufaa au mahakama au hatua zozote za kiutawala zitakazobainishwa na Waziri.

**Dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira**

227 (1) Waziri atabainisha kwenye kanuni shughuli au michakato inayotishia mazingira ambapo dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira inaweza kuhitajika.

(2) Dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira itawekwa kwa Mkurugenzi wa Mazingira kama amana ya matumizi mazuri ya mazingira mpaka pale itakaporudishwa kwa mweka amana hiyo.

(3) Dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira itarejeshwa kwa mwendeshaji wa shughuli au mchakato baada ya kukidhi masharti yaliyowekwa na Waziri.

(4) Mkurugenzi wa Mazingira atampatia mwendeshaji wa shughuli au mchakato fursa ya kusikilizwa kabla ya kuchukua dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira.

(5) Dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira itachukuliwa yote au sehemu yake iwapo Mkurugenzi wa Mazingira ataona kwamba vitendo vya mwendeshaji vinakiuka masharti ya Sheria hii, ikiwa ni pamoja na masharti ya hati yoyote, leseni yoyote au kibali kilichotolewa kwa mujibu wa Sheria hii.

(6) Pale ambapo dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira itachukuliwa kwa mujibu wa kifungu cha (5), dhamana hiyo itatumika kukarabati mazingira yaliyoharibiwa.

**Haki ya kufidiwa**

228 (1) Ili kuepuka utata, Waziri atatunga kanuni zinazobainisha haki ya kulipwa fidia kwa wale ambao wataathirika wakati wakilinda mazingira.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka viwango vya kuhifadhi mazingira na

kusababisha uharibifu wowote, atalipa fidia kwa madhara na gharama za kurekebisha uharibifu huo.

**Utayari wa kukabiliana na dharura za kimazingira**

229 (1) Waziri ataandaa miongozo ya usimamizi wa dharura za kimazingira ikiwa ni pamoja na-

(a) umwagikaji na uvujaji mkubwa wa mafuta na gesi;

(b) umwagikaji wa dutu nyinginezo zenye madhara;

(c) ajali za viwandani;

(d) janga asilia na janga linalotokana na mabadiliko ya tabianchi kama vile – mafuriko, tufani, ukame na uvamizi mkubwa wa visumbufu au udukizi wa spishi ngeni za wanyama na mimea;

(e) mfumuko wa wakimbizi; na

(f) moto.

(2) Waziri atashirikiana na Idara ya Maafa, asasi za Kiserikali na za binafsi, mashirika husika pamoja na watu binafsi kwa nia ya kuandaa mpango wa kukabiliana na dharura za kimazingira unaofaa katika kukabiliana na hatari inayoweza kutokea kwenye jingo, nyumba au eneo lolote la ardhi.

**Kanuni**

230 (1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kifungu cha (1), kanuni zilizotungwa kwa mujibu wa kifungu cha (1) zinaweza-

(a) kuruhusu utoaji, urekebishaji na ufutaji wa leseni yoyote iliyotolewa chini ya Sheria hii;

(b) kubainisha ada na kodi zitakazotozwa chini ya Sheria hii;

(c) kuweka ulinzi wa spishi yoyote mahususi ya wanyama na mimea;

(d) kuweka udhibiti au uzuiaji wa upatikanaji wa rasilimali jeni za Tanzania na kuweka viwango vya ada zitakazolipwa na wale watakaoruhusiwa kuzipata;

(e) kuweka taratibu za kuingiza nchini na kuuza nje ya nchi “plasima jemu”;

(f) kuweka udhibiti wa utengenezaji, uingizaji nchini, uuzaji nje, usafirishaji, ukusanyaji, usafishaji, uhifadhi, urejelezaji au utupaji wa dutu ambazo zinaweza kuwa na madhara kwa mazingira na afya ya jamii;

(g) kuweka utaratibu wa utupaji wa takataka kwa jumla;

(h) kuweka utaratibu wa kufanya tathmini ya athari kwa mazingira

na kubainisha ukubwa wa miradi na shughuli zilizobainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria hii;

(i) kuweka utaratibu wa kudhibiti upunguaji wa tabaka la ozoni;

(j) haki ya kufidiwa kwa wale wanaoathirika wakati wa kulinda mazingira;

(k) kubainisha utaratibu na namna ya kuandaa, kupokea na kutekeleza mpango tekelezi wa mazingira;

(l) kuweka utaratibu wa kuwa na usimamizi endelevu wa ardhi oevu lindwa;

(m) kuweka utaratibu wa ulinzi na usimamizi fungamani wa ukanda wa pwani;

(n) kuweka utaratibu wa kuhifadhi bioanuwai mahali asilia au nje ya hapo;

(o) kuweka utaratibu na hatua kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa;

(p) kuweka utaratibu wa usimamizi wa vichafuzi dumufu vya kiogani;

(q) kuweka utaratibu wa kuhakiki mazingira;

(r) kuweka utaratibu kwa kufanya tathmini ya mazingira kimkakati; na

(s) kubainisha jambo lolote litakalohitajika au kuruhusiwa kutolewa ufafanuzi chini ya Sheria hii.

**Kufutwa kwa Sheria Na. 19 ya mwaka 1983**

231 (1) Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira ya 1983 imefutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 1983, teuzi, amri, notisi au chochote kitakachotolewa au kuundwa chini ya Sheria iliyofutwa, kitahesabika kuwa kimefanywa chini ya Sheria hii, na kitaendelea kutambulika na kuwa na nguvu kisheria hadi wakati teuzi, amri na notisi hizo au kitu chochote kilichotolewa au kufanywa kitakapofutwa, kuondolewa au vinginevyo kwa nguvu ya waraka au amri iliyotolewa chini ya au kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii.

(3) Bila kuathiri vifungu (1) na (2), uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, wajumbe wa Bodi ya Baraza utaendelea kutambuliwa, na ajira zote pamoja na mikataba ya ajira iliyowekwa kuhusu utekelezaji wa majukumu au kwa kutumia madaraka yaliyopewa Baraza kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii vitachukuliwa kama vile vimefanyika au kutumika chini ya masharti ya Sheria hii.

(4) Kifungu hiki hakitatumika kwa vyovyote vile kumzua mwajiriwa au mteuliwa ama kujiuzulu au kuachishwa kazi.

**Mgongano na sheria nyinginezo**

232 Pale ambapo masharti ya Sheria hii yatakuwa yanapingana au kuhitilafiana na fungu lingine lolote la sheria nyingine inayohusu usimamizi wa mazingira, masharti ya Sheria hii ndiyo yatakayotumika.

**Sheria kutafsiriwa kwa Kiswahili**

233 Mara tu baada ya Sheria hii kuidhinishwa Waziri, mapema kadiri itakavyowezekana, atahakikisha kwamba Sheria hii imetafsiriwa kwa Kiswahili na tafsiri hiyo itatangazwa kwenye *Gazeti la Serikali* ambalo litasambazwa kwa umma na kwa namna nyingine yoyote ambayo itawawezesha raia wa Tanzania kuifikia tafsiri hiyo kwa urahisi.

## MAJEDWALI

## JEDWALI LA KWANZA

***Limetengenezwa chini ya Fungu la 11 (3)***

## MUUNDO, KIKAO NA UTARATIBU WA KAMATI YA TAIFA YA USHAURI WA MAZINGIRA

**Muundo wa Kamati**

1. Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira itaundwa na;

(a) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya masuala ya mazingira ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Mkurugenzi wa Mazingira ambaye atakuwa Katibu;

(c) Kamishna wa Madini;

(d) Mkurugenzi wa Misitu;

(e) Mkurugenzi wa Wanyamapori;

(f) Mkurugenzi wa Rasilimali Maji;

(g) Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao;

(h) Mkurugenzi wa Nishati;

(i) Mkurugenzi wa Maendeleo ya Makazi;

(j) Mkurugenzi wa Barabara;

(k) Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa;

(l) Mkurugenzi wa Viwanda;

(m) Mkurugenzi wa Huduma ya Tiba ya Wanyama;

(n) Mkuu wa Kitengo cha Taifa cha Maafa;

(o) Kamishna wa Ardhi;

(p) Mkurugenzi wa Uvuvi;

(q) Mkurugenzi wa Mifugo;

(r) Mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(s) Mwakilishi kutoka Wizara yenye dhamana ya Masuala ya Maendeleo ya Jamii;

(t) Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Usimamizi wa Mazingira;

(u) Mkurugenzi wa Huduma za Kinga kutoka Wizara ya Afya;

(v) Mkemia Mkuu wa Serikali;

(w) Mwakilishi kutoka asasi za elimu ya juu;

(x) Mwakilishi kutoka vikundi mbalimbali vya kiraia; na

(y) Mwakilishi kutoka asasi za sekta binafsi.

**Makamu Mwenyekiti**

2 Katika kikao cha kwanza, wajumbe wa Kamati watateua miongoni mwao Makamu Mwenyekiti.

**Kipindi cha kushika madaraka**

3 Wajumbe wa Kamati, isipokuwa tu wale walioteuliwa kwa nyadhifa zao, watashika madaraka kama wajumbe wa Kamati kwa miaka mitatu, na iwapo muda wao wa kuwa wajumbe hautakoma kutokana na ukiukaji wa maadili au kutokuhudhuria vikao vitatu vya Kamati mfululizo bila sababu, watastahili kuteuliwa tena kwa kipindi kimoja zaidi.

4 (1) Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira itakutana kwa nyakati na mahali ambapo Mwenyekiti ataamua kwa kushaurinana na Katibu.

(2) Kikao cha kawaida cha Kamati kitaitishwa na Mwenyekiti kwa notisi itakayoelezea mahali, tarehe na wakati wa kufanya kikao hicho pamoja na ajenda zake zitakazotumwa kwa kila mjumbe, kazini au nyumbani kwake, ndani ya siku kumi na nne kabla ya tarehe ya mkutano.

(3) Mwenyekiti, au kama hayupo, mjumbe aliyechaguliwa kukaimu nafasi ya Mwenyekiti, ataitisha kikao maalumu cha Kamati kwa maandishi yaliyotiwa saini na wajumbe wa Kamati wasiopungua watatu na kabla kikao hicho maalumu hakijafanyika, kila mjumbe atapelekewa, kazini au nyumbani kwake, ajenda za kikao angalau siku tatu kabla ya tarehe ya kikao.

(4) Kikao cha Kamati kitaendeshwa na Mwenyekiti, au kama hayupo, kitaendeshwa na mjumbe aliyechaguliwa na wajumbe waliohudhuria kikao hicho.

**Waalikwa** 5 Bila kuathiri aya ya 1, Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira anaweza kumwalika mtu yeyote atakayeonekana kuwa anao uwezo wa kuisaidia Kamati katika kutoa maamuzi yake.

**Akidi** 6 Akidi kwenye kikao chochote cha Kamati itakuwa nusu ya wajumbe wa Kamati nzima.

**Kamati ndogo ndogo** 7

1. Kamati inaweza kuunda kamati nyingine ndogondogo kama itakavyoona inafaa ili kuiwezesha kutekeleza vyema kazi zake.
2. Kamati pamoja na kamati zozote ndogondogo zitakuwa na uwezo wa kualika mtu yeyote kuhudhuria kikao cha kawaida au maalumu cha Kamati au cha kamati ndogo , na mwalikwa wa aina hiyo atakuwa na haki na wajibu wa mjumbe wa Kamati au wa kamati ndogo isipokuwa hatakuwa na haki ya kupiga kura.

**Mgongano wa maslahi** 8 Mjumbe ambaye ana maslahi yoyote binafsi ama moja kwa moja au vinginevyo kwenye suala lolote litakalofikishwa kwenye Kamati au kamati ndogo atatakiwa, mapema iwezekanavyo, kumfahamisha Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti kuhusu maslahi hayo, na hatashiriki katika kufikia uamuzi wowote kuhusu suala hilo, na, isipokuwa tu kwa ridhaa ya wajumbe wengi waliohudhuria kikao hicho, hatatakiwa kuchangia maoni yake kwenye kikao hicho.

**Utaratibu wa kuendesha shughuli za Kamati** 9 Kwa mujibu wa masharti ya Jedwali hili, Kamati itajiwekea taratibu za kuendesha shughuli zake.

**Taarifa za shughuli za** 10 Kamati itaandaa taarifa ya mwaka itakayobainisha shughuli za sasa na za baadaye.

**Kamati**

## JEDWALI LA PILI

*Limetengenezwa chini ya fungu la 20 (2)*

## UTARATIBU WA BODI WA UENDESHAJI SHUGHULI ZAKE

| | | |
|---|---|---|
| **Makamu Mwenyekiti** | 1 | Wanakamati miongoni mwao watamteua mjumbe mmoja kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi na atashika nafasi hiyo kwa mwaka mmoja toka tarehe ya uteuzi kwa masharti kwamba ataendelea kuwa mjumbe, na ataweza kuteuliwa tena. |
| **Kipindi cha madaraka** | 2 | (1) Isipokuwa tu kama uteuzi wake utasitishwa na Rais au na Waziri au vinginevyo akiacha kuwa mjumbe, mjumbe wa Bodi aliyeteuliwa na Rais atashika madaraka kwa kipindi kilichotajwa na Rais kwa upande wa Mwenyekiti, au Waziri kwa upande wa mjumbe mwingine yeyote, au pale ambapo hakuna muda uliotajwa, kipindi cha madaraka kitakuwa miaka mitatu kuanzia tarehe ya uteuzi, na aliyekuwa madarakani ataweza kuteuliwa tena.<br>(2) Mjumbe yeyote aliyeteuliwa chini ya aya ya 1(a) au (c) atakuwa na hiyari ya kujiuzulu madaraka yake wakati wowote kwa kutoa notisi kwa maandishi kwa Rais, au kama itakavyokuwa, kwa Waziri, na atahesabika amejiuzulu kuanzia tarehe iliyotajwa kwenye notisi, au kama tarehe haikutajwa kwenye notisi, kuanzia tarehe ambayo notisi ilipopokewa na Rais au Waziri.<br>(3) Kama mjumbe wa Bodi aliyeteuliwa kutokana na wadhifa wake atashindwa kwa sababu yoyote ile kuhudhuria kikao chochote kile, anaweza kumteua mtu yeyote kwa maandishi kutoka Wizarani kwake au kutoka Shirika lake ahudhurie kikao hicho kwa niaba yake. |
| **Kuachishwa na kukoma ujumbe** | 3. | Uteuzi wa mjumbe wa Bodi unaweza kusitishwa na Mamlaka ya Uteuzi iwapo mjumbe:-<br>(a) atatangazwa kisheria kuwa mufilisi au kama atakuwa na |

makubaliano ya kudaiwa na wadai wake;

(b) atatiwa hatiani kwa kosa la jinai na kuhukumiwa kwenda jela kwa kwa miezi sita bila kupewa chaguo la faini;

(c) atapoteza uwezo kimwili au kiakili kutokana na ugonjwa wa muda mrefu na kushindwa kumudu majukumu yake kama mjumbe wa Bodi; au

(d) atashindwa au kukosa uwezo wa kumudu majukumu ya madaraka yake kama mjumbe kwa sababu nyingine yoyote ile.

**Wajumbe Mbadala** 4 Iwapo mjumbe atafariki dunia au atajiuzulu, au vinginevyo ataacha madaraka kabla ya kumalizika kwa muda wake, mamlaka ya uteuzi itateua mtu mwingine wa kushika madaraka hayo kwa kipindi kilichobaki..

**Uendeshaji wa mikutano** 5 (1) Mwenyekiti ataendesha vikao vyote vya Bodi.

(2) Endapo Mwenyekiti hatakuwepo kwenye kikao chochote cha Bodi, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao.

(3) Endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wote hawatakuwepo kwenye kikao chochote cha Bodi, wajumbe waliohudhuria watamchagua Mwenyekiti wa muda kutoka miongoni mwao ambaye ataendesha kikao.

(4) Mwenyekiti au mtu atakayeendesha kikao cha Bodi atakuwa na haki ya kupiga kura ya turufu mbali na kura yake mwenyewe iwapo kura zitafungana wakati wa kupiga kura.

**Mikutano na taratibu za Bodi** 6 (1) Kwa kuzingatia aya ndogo ya (2), Bodi itafanya vikao vyake vya kawaida mara tatu kwa mwaka kutafakari shughuli zake.

(2) Ikibidi, Bodi inaweza kuitisha kikao cha dharura wakati wowote endapo itaombwa kwa maandishi kufanya hivyo na nusu ya wajumbe wote.

(3) Mwenyekiti, au kama hayupo nchini, Makamu Mwenyekiti, anaweza kuitisha kikao maalumu cha Bodi baada ya kuombwa kwa maandishi kufanya hivyo na angalau wajumbe watano..

(4) Katibu wa Bodi atampatia kila mjumbe taarifa kamili kuhusu wakati na mahali muafaka pa kufanyia mkutano.

(5) Bodi inaweza kualika mtu yeyote asiye mjumbe kushiriki katika mjadala wa kikao chochote cha Bodi, lakini, mwalikwa huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

**Akidi** 7 Akidi ya kikao chochote cha Bodi itakuwa nusu ya wajumbe wote.

**Uamuzi wa Bodi** 8

(1) Kwa kuzingatia masharti yanayohusu upigaji wa kura, masuala yote yataamuliwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1) uamuzi unaweza kufanywa na Bodi bila kukutana kwa kusambaza nyaraka husika kwa wajumbe, pamoja na utoaji wa maoni ya wajumbe walio wengi kwa maandishi.

**Kuandika na kutunza kumbukumbu** 9

(1) Bodi itahakikisha kwamba, kumbukumbu za shughuli pamoja na za vikao na maamuzi yake yote zinaandikwa na kuhifadhiwa na kwamba, kumbukumbu za kila kikao cha Baraza zitasomwa na kuthibitishwa au kufanyiwa marekebisho na kuthibitishwa kwenye kikao cha Bodi kinachofuata na zitatiwa saini na mtu anayeendesha kikao.

(2) Iwapo hakuna uthibitisho kuonyesha kwamba hakuna makosa ya uandishi, kumbukumbu zozote zilizotiwa saini na mtu aliyeendesha kikao cha Bodi zitahesabika kuwa ni kumbukumbu sahihi za kikao hicho.

| | | |
|---|---|---|
| **Nafasi zilizo wazi n.k. kutoathiri kumbukumbu za mkutano** | 10 | Uhalali wa jambo au kumbukumbu za Bodi hazitaathiriwa na kuachwa wazi kwa nafasi za wajumbe wake, au na upungufu wowote uliotokea kwenye uteuzi wa mjumbe yeyote. |
| **Amri, miongozo** | 11 | Amri , miongozo, notisi au nyaraka zingine zote zilizotolewa na Bodi au kwa niaba ya Bodi zitatiwa saini na-<br>(a) Mwenyekiti; au<br>(b) Katibu au ofisa yeyote au maofisa wa Bodi walioidhinishwa kwa maandishi na Katibu. |
| **Lakiri ya Baraza** | 12 | Lakiri ya Bodi haitawekwa kwenye Waraka wowote isipokuwa tu kama ni mbele ya Mwenyekiti au Katibu au Ofisa mwingine wa Bodi na angalau mjumbe mmoja wa Bodi. |
| **Bodi kujiwekea utaratibu wake** | 13 | Kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili Bodi itaweza kujiwekea utaratibu wake yenyewe. |

**JEDWALI LA TATU**

***Limetengenezwa chini ya fungu la 81***

**AINA YA MIRADI INAYOHITAJI TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA**

1. Miradi ya Jumla-
   (a) shughuli yoyote isiyoendana na mazingira halisi ya mahali husika;
   (b) jengo lolote lenye ukubwa usioshabihiana na mazingira ya mahali husika;
   (c) mabadiliko makubwa katika mtumizi wa ardhi.

2. Maendeleo Mijini.
3. Usafirishaji.
4. Mabwawa, mito na vyanzo vya maji.
5. Unyunyiziaji toka angani.
6. Uchimbaji madini, au kokoto au mchanga
7. Shughuli za misitu.
8. Kilimo pamoja na ufugaji.
9. Viwanda vya usindikaji na vya kutengeneza bidhaa.
10. Miundombinu ya umeme.
11. Usimamizi wa haidrokaboni, pamoja na uwekaji au uhifadhi wa gesi asilia na mafuta ya kuendeshea mashine na yale yenye asili ya kulipuka.
12. Utupaji taka.

13. Maeneo ya hifadhi za asili.
14. Mitambo ya kuzuia nguvu za nyuklia.
15. Maendeleo makubwa katika bioteknolojia pamoja na uingizaji na majaribio ya viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya ya nasaba kijeni.
16. Shughuli yoyote nyingine kama itakavyoainishwa kwenye kanuni.

## JEDWALI LA NNE

***Limetengenezwa kwa mujibu wa fungu la 215***

## MUUNDO NA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA BODI YA WADHAMINI WA MFUKO

**Muundo wa Bodi ya Wadhamini**

1 (1) Kwa mujibu wa masharti ya aya ndogo ya (2) Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ambao idadi yao haitapungua saba na wala kuzidi tisa itaundwa na-

(a) Mwenyekiti ambaye atakuwa mtu mwenye staha na maadili mema na ambaye amewahi kushika nyadhifa za juu Serikalini au ni mtu maarufu nchini Tanzania atakayeteuliwa na Rais;

(b) Ofisa Mwandamizi kutoka Wizara yenye dhamana ya masuala ya fedha;

(c) Ofisa Mwandamizi kutoka Wizara yenye dhamana ya masuala ya mazingira;

(d) Mjumbe kutoka kwenye asasi za mafunzo ya usimamizi wa mazingira;

(e) Mhasibu aliyesajiliwa;

(f) Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(g) Mjumbe kutoka Asasi Zisizo za Kiserikali zinazojishughulisha na usimamizi wa mazingira.

(h) Mwakilishi kutoka Wizara yenye dhamana ya masuala ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na

(i) Mwakilishi wa asasi za utafiti wa usimamizi wa mazingira.

(2) Wajumbe wasiopungua watatu watakuwa wanawake

| | | |
|---|---|---|
| **Makamu Mwenyekiti** | 2 | Wadhamini watamchagua Makamu Mwenyekiti miongoni mwao ambaye atashika madaraka kwa miaka miwili lakini anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha miaka miwili zaidi kwa masharti kwamba ataendelea kuwa Mdhamini. |
| **Muda wa kushika madaraka** | 3 | Wadhamini watashika madaraka kwa miaka mitatu na isipokuwa tu kama ujumbe wao utasitishwa kutokana na utovu wa nidhamu au sababu nyingine ya kuridhisha, wataweza kuteuliwa kwa kipindi kingine zaidi. |
| **Mahudhurio ya wajumbe kwa nyadhifa zao** | 4 | Wakati wa kujadili masuala yanayohusu usimamizi wa mfuko ofisa mwenye dhamana ya masuala ya fedha ya mfuko atahudhuria kikao cha Wadhamini kama mjumbe kwa wadhifa wake. |
| **Kuitisha mikutano** | 5 | (1) Kwa mujibu wa masharti ya aya ndogo ya (2) kikao cha kawaida cha Wadhamini kitaitishwa na Mwenyekiti kwa notisi inayoeleza kuhusu tarehe, wakati, ajenda na mahali pa kikao pamoja na makabrasha husika ya kikao vitapelekwa kwa kila Mdhamini mahali pake pa kazi, au nyumbani kwake si chini ya siku kumi na nne kabla ya tarehe ya kikao hicho.<br>(2) Mwenyekiti au kama yeye hayupo, Makamu Mwenyekiti au Kaimu Mwenyekiti, atapaswa kuitisha kikao maalumu cha Wadhamini baada ya kupokea notisi ya maandishi lililotiwa saini na Wadhamini wasiopungua watatu. |

| | | |
|---|---|---|
| **Akidi** | 6 | Akidi ya kikao chochote cha Wadhamini itakuwa nusu ya wajumbe waliopo madarakani. |
| **Mgongano wa maslahi** | 7 | Mjumbe ambaye ana maslahi yoyote binafsi, ama moja kwa moja au vinginevyo kwenye suala lolote litakalowasilishwa kwenye Bodi ya Wadhamini, atapaswa kumwarifu mapema iwezekanavyo Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti kuhusu maslahi hayo, na hatatakiwa kuchangia maoni yake kwenye kikao hicho. |
| **Bodi kujiwekea utaratibu wake** | 8 | Kwa mujibu wa masharti ya Jedwali hili Wadhamini wanaweza kujiwekea utaratibu wa uendeshaji wa shughuli zao. |

**Imepitishwa na Bunge tarehe 11 Novemba 2004**

DAMIAN S. FOKA
**KATIBU WA BUNGE**